

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 9 Juni, 2020**

*(Bunge lilianza Saa Nane Kamili Mchana)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Naomba tukae. Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

#### AZIMIO LA BUNGE

Azimio la Bunge la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa namna alivyoongoza Taifa katika mapambano dhidi ya Janga la Ugonjwa wa Corona (Covid – 19).

#### MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 386

#### Upungufu wa Vituo wa Afya Tabora

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Jimbo la Tabora mjini lina Kata 29 lakini - lina kituo cha kimoja tu cha afya.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Vituo vya Afya katika Manispaa ya Tabora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, halmashauri ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali, vikijumuisha Hospitali mbili, Kituo cha Afya kimoja na Zahanati 22. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati ya Ituru na Igombe. Vilevile Serikali imetenga shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Tabora. Serikali itaendelea kujenga, kuratabati na kupanua vituo vya kutolea huduma za afya Manispaa ya Tabora kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 387

**Hitaji la Umeme Shule za Sekondari Langali – Mvomero**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Langali haina umeme hali hiyo imekuwa kero kubwa kwa wanafunzi hasa wakati wa mitihani kwani hushindwa kusoma nyakati za usiku:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Shule ya Sekondari Langali ili kuondoa adha wanayopata wanafunzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) imefanya tathmini na kubaini kuwa takribani nguzo sita (6) zinahitajika ili kufikisha umeme katika shule hiyo. Aidha, uwekaji wa mifumo ya umeme katika shule unaendelea ambapo kazi hiyo imekamilika katika jengo la utawala la shule. Halmashauri imepanga kutumia mapato ya ndani ili kuingiza umeme katika shule hiyo na kuwaondolea adha wanafunzi.

Na. 388

**Hitaji la Vituo wa Afya - Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Jimbo la Tunduru Kusini lina Vituo vya Afya vitatu kati ya Kata kumi na tano zilizopo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya Afya katika Kata ya Nafasi, Malumba, Mbati, Lukumbule, Mchesi, Namasakata, Ligoma, Mischel, Touwemacho na Mchuruka?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kituo cha Afya Mtina kama vituo vingine vya Nkasale na Mchoteka?

(c) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ya kujenga Kituo cha Afya Nalasi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa Pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya

Tunduru shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Vituo vya Afya Mkasale (milioni 400), Mchoteka (milioni 400) na Mkasale (milioni 500). Vituo hivi kwa sasa vimekamilika. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imeitengenea Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha maboma manne ya Zahanati za Chikomo, Angalia, Namiungo na Legeza Mwendo.

Na. 389

**Mahitaji ya Kikao cha Pamoja kati ya Serikali  
na Wafugaji**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Wafugaji wa ng'ombe wa Wilaya za Biharamulo, Bukombe, Ngara, Karagwe na Chato wanahitaji kuwa na kikao kazi na Serikali ili kuoanisha mawazo na jitihada walizonazo kupitia umoja wao na jitihada za Wataalam wa Serikali na watunga Sera (wanasiasa) kwa kuwa ni muhimu kuwa na suluhu ya changamoto inayoanzia chini (*bottom up approach*)badala ya Serikali na wataalam kudhani kuwa wana ufahamu kwa niaba ya wafugaji wenyewe katika kila kitu kinachowahusu wafugaji:-

Je, Serikali ipo tayari kukutana nao kwa mtindo huo ambaao wafugaji wanaamini utaleta tija?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara imetembelea wilaya 21 za Kanda ya Ziwa ambazo ni Misenyi, Kyerwa, Muleba, Bukoba, Sengerema, Ukerewe, Illemba, Misungwi, Magu, Kishapu, Kahama, Bukombe, Buchosa, Chato, Geita, Bunda, Itilima, Karagwe, Meatu, Maswa, Serengeti na Tarime kwa lengo la kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wafugaji.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hizo Viongozi na Watalamu wamepita wakifanya yafuatayo; kupeleka teknolojia mbalimbali za Ufugaji bora na endelevu; kuwapa elimu na maarifa mapya wafugaji kwa njia ya Mafunzo Rejea, Mashamba darasa ya malisho bora; Kampeni za Uogeshaji na chanjo mbalimbali za mifugo na matumizi sahihi ya madawa na viwatilifu vya mifugo; ufugaji wa kuku wa kisasa na asili, uhamasishaji na uanzishwaji wa vyama vya Ushirika, wafugaji kujua sheria, manuni na miongozo mbalimbali wanapotekeleza majukumu yao; matumizi bora ya ardhi kwa wafugaji. Utatuzi wa migogoro mbalimbali ya muda mrefu ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Pia, kila walipopita Viongozi wakuu wa Wizara wananchi wamepokea majibu ya hoja mbalimbali na maelekezo ya hatua za utekelezaji wa hoja zao.

Mheshimiwa Spika, wizara inapokea kwa furaha sana hitaji hili la wafugaji wa Biharamulo, Bukombe, Ngara, Karagwe na Chato ambao wana idadi ya ng'ombe zaidi ya 685,000. Ni makusudio ya Wizara kuona kuwa Wataalamu wetu wanawafikia Wafugaji, hivyo kwa uhitaji huu sasa tumefarijika kupata ushirikiano huu kutoka kwenye Wilaya hizo 5 ambao utaleta tija kwenye Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kuwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari kukutana na Wafugaji wa wilaya hizo; Wizara itafanya mawasiliano na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa mara baada ya Bunge la Bajeti kukamilika ili kupanga ratiba ya vikao katika wilaya hizo 5.

Na. 390

**Kuhusu ‘Uvunaji wa Maji Katika Mbuga Inayozunguka  
Mji wa Itigi’**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Wakati akijibu swalilangu la nyongeza Bungeni Naibu Waziri wa Kilimo aliahidi kuwa ataleta wataalam wa

umwagiliaji ili kuvuna maji katika Mbuga inayozunguka Mji wa Itigi.

Je, ni lini wataalam hao watakuja kufanya utafiti huo kwani wananchi wanasubiri kwa hamu kuona maji hayo yanavunwa ili kuепusha mafuriko yanayotokea kila kipindi cha mvua?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la mheshimiwa Yahaya Omari Massare Mbunge wa jimbo la Manyoni Magharibi kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kuvuna maji katika mbuga inayozunguzuka Mji wa Itigi, Serikali inatarajia kutuma wataalamu wa umwagiliaji kufanya utafiti katika kipindi cha mwezi Juni 2020 kabla ya mwaka wa Fedha 2019/2020 kumalizika.

Aidha, ujenzi wa bwawa la kuvuna maji katika mbuga hiyo utaanza baada ya taarifa ya wataalamu, upembuzi na usanifu kufanyika pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha zoezi hilo; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kufanikisha utafiti wa kubaini maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha Umwagiliaji pamoja na maeneo yote yanayofaa kwa uvunaji wa maji ili yatumike kwa kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa maji katika mbuga hii inayozunguka mji wa Itigi utawezesha wakulima wa Kata za Kitaraka, Itigi Mjini, Tambukareli, Itigi Majengo, Sanjaranda, Ipande, Aghondi na Idodyandole katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kuепukana na mafuriko lakini pia itasaidia maji hayo yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji katika eneo hilo.

Na. 391

### **Tatizo la Maji Mwanza**

**MHE. SUSSANE P. MASSELE** aliuliza:-

Kutokana na uhalisi wa Jiji la Mwanza hasa kuwepo kwa milima kumekuwepo na shida ya upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo.

Je, Serikali itamaliza lini tatizo la maji kwa wakazi wa maeneo ya miinuko katika Jiji la Mwanza hasa kwa kuwa na mashine zenyne uwezo wa kusukuma maji kila mahali?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swalii la Mheshimiwa Susan Peter Masseele, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo ya miinuko katika Jiji la Mwanza. Katika kutatua changamoto hii, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya Maji kuititia Programu ya *Lake Victoria Water and Sanitation (LVWATSAN)* inayolenga kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza. Miradi hii inatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo ambaoni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank, EIB*) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*Agence Française de Développement, AFD*) kwa gharama ya TZS Billioni 276,925 (*Euro Million 104.5*)

Mheshimiwa Spika, moja ya miradi iliyotekelizwa kuititia Programu hii ni mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa wakazi wa Jiji la Mwanza waishio katika maeneo yenye miinuko. Kuititia mradi huu, jumla ya matenki saba (7) ya kuhifadhi maji yenye ujazo tofauti yamejengwa katika maeneo yafuatayo; Nyasaka (ujazo wa litu 1,200,000), Nyegezi (Ujazo wa litu 1,200,000),

Mjimwema/Nyakabungo (Ujazo wa lita 1,200,000), Kitangiri/Ibanda (Ujazo wa Lita 500,000), Nyamhongolo (Ujazo wa lita 500,000) na Bugarika (matenki mawili yenye ujazo wa lita 700,000 na 250,000). Aidha, mabomba ya kusafirishia na kusambaza maji yenye urefu wa jumla ya kilomita 64.8 yalitandikwa na wateja 20,000 waliunganishwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia mradi huu, vituo vipyta vitatu (3) vya kusukuma maji (*Booster Pumping Stations*) kuelekea kwenye matenki yaliyotajwa awali vimejengwa katika maeneo ya Nyasaka, Nyegezi na Bugando/Bugarika, pia uimarishaji na uboreshaji wa vituo vikuu vya kusukuma maji vya Mabatini, Nyegezi na Kona ya Bwiru umefanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira MWAUWASA imepanga kujenga tenki lenye ujazo wa lita 2,000,000 kwenye mlima wa Buswelu maarufu kama "Mlima wa DC". Tenki hili kwa kiasi kikubwa litatatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye maeneo ya Buswelu, Masanza, Mlimani City, Kiseke-Buyombe, Bujingwa na Kahama.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, Serikali iko kwenye hatua za mwisho kwa ajilli ya kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chanzo kipyta cha Maji katika eneo la Butimba. Mradi huu wa chanzo kipyta utetekelezwa kwa mfumo wa kusanifu na kujenga (*Design and Build*) ambapo, kutegemeana na usanifu wa mwisho, chanzo hiki kitakuwa na uwezo wa kuzalisha kiasi cha lita 60,000,000 kwa siku, uzalishaji ambao kwa kiasi kikubwa utatua kero zote za upatikanaji wa maji kwa Jiji la Mwanza.

Na. 392

### **Kuungeza Kina cha Gati ya Bandari ya Kyamkwikwi**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) ilijenga Gati la kisasa kuegesha meli katika Bandari ndogo ya Kyamkwikwi.

(a) Je, ni lini shughuli ya kuongeza kina cha Gati hilo itaanza ili kuruhusu meli kubwa katika Bandari hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga Gati la kisasa katika kisiwa cha Goziba?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) imeingia mkataba na Kampuni ya *ANOVA Consult Company Ltd* ili kuhuisha Mpango Kabambe wa Mamlaka (*National Ports Master Plan*). Mpango huu unatoa mwongozo wa kimkakati wa kuendeleza na kuboresha bandari nchini zikiwemo bandari za mwambao wa bahari ya Hindi na katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kazi hii ilianza Mwezi Novemba, 2019 na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango tajwa hapo juu, Serikali kuititia *TPA* imeingia Mkataba na Kampuni ya *NIRA Consulting S.P.A* ikishirikiana na Kampuni ya *Intercontinental* kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina katika bandari za Ziwa Victoria. Kazi hii ilianza mwezi Februari, 2020 na inatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2021.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa kazi hizi kutatoa mwelekeo wa kubaini maeneo yanayohitaji kujengewa magati na pia kutambua magati yaliyopo yanayohitaji kuongezwa kina ili kuruhusu meli kubwa kutia nanga.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote waishio katika visiwa vilivypo katika Ziwa Victoria ikijumuisha bandari ndogo ya Kyamkwikwi na pia Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa kuwa

kukamilika kwa Pembuzi tajwa hapo juu, kutatoa fursa nzuri na dira katika kuendeleza bandari nchini.

Na. 393

### **Ujenzi wa Barabara ya Itoni – Ludewa**

**MHE. LUCIA M. MILOWE** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa ulianza mwaka 2013 na ulikuwa ujengwe kwa kilometra 50 tu kwa Loti ya kwanza, lakini hadi sasa barabara hiyo haujakamilika:

Je, ni kwa nini ujenzi huo haujakamilika?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda sehemu ya Lusitu Mawengi (km 50) kwa kiwango cha zege ulianza rasmi tarehe 14 Desemba, 2016 na ulikuwa ukamilike tarehe 14 Aprili, 2019. Hata hivyo, kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la kazi na mabadiliko ya hali ya hewa yasiyotarajiwa, Mkandarasi ameongezewa muda wa kukamilisha kazi hadi tarehe 30 Oktoba, 2020. Hadi sasa kufikia Machi, 2020 Mkandarasi amefanya kazi ya upanuzi wa barabara, kujenga madaraja na kukamilisha km 11.9 kwa kiwango cha zege.

Na. 394

### **Kuboresha Makazi ya Askari Magereza (Nachingwea)**

**MHE. HASSAN E. MASALA** aliuliza:-

Hali ya nyumba za askari Magereza wilayani Nachingwea ni mbaya sana.

Je, nini mpango wa Serikali juu ya uboreshaji wa makazi hayo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Elias Masala Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa lipo tatizo la uchakavu wa nyumba za maafisa na askari katika Gereza la Wilaya Nachingwea kama ilivyo kwenye Magereza mengine nchini. Ni nia ya Serikali kuendelea kuzifanyia ukarabati mkubwa nyumba hizo ili kuboresha makazi ya askari. Hata hivyo kasi ya kuzifanyia ukarabati nyumba hizo imekuwa ni ndogo kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hivyo Serikali itaendelea kuzifanyia ukarabati nyumba hizo kadri hali ya Bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha maafisa na askari wanakuwa na makazi bora na yenye viwango , Serikali kupitia Jeshi la Magereza inaendelea kutekeleza mpango wa kujenga nyumba kwa njia ya ubunifu katika vituo mbalimbali vya magereza nchini ikiwemo Gereza(W) Nachingwea ambapo kila Mkuu wa kituo ameелеkezwa kufyatua matofali yasiyopungua 30,000 kwa msimu, na kupatiwa ramani za ujenzi wa nyumba hizo. Hadi kufikia Aprili, 2020 jumla ya nyumba 393 zimejengwa Nchi nzima. Kati ya hizo nyumba 129 zimeshakamilika na nyumba 264 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Na. 395

**Kuweka Zuijio la Kuoa kwa Wanaume ambao  
Hawajatahiriwa**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED aliuliza:-**

Imethibitika kuwa saratani ya mlango wa kizazi inasababishwa na virusi vinavyopatikana kwa Wanaume ambao hawajatahiriwa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka zuio la kuo a kwa Wanaume ambao hawajatahiriwa?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli saratani ya mlango wa kizazi inasababishwa na kirusi cha *Human Papilloma*. Kirusi hiki kwa sehemu kubwa huambukizwa kwa njia ya kujamiihana na mtu mwenye maambukizo.

Mheshimiwa Spika, si wanawake wote walioambukizwa kirusi cha *Human Papilloma* watapata saratani ya mlango wa kizazi, ila ni wale tu watakao kuwa na maambukizi ya kirusi hiki kwa muda mrefu "*persistence infection*" ndiyo wataishia kupata mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na yasipogundulika na kupatiwa matibabu wataishia kupata saratani ya mlango wa kizazi. Vilevile, ifahamike kwamba vipo vichocheo vingine ambavyo pia vinachangia kuwa na uwezekano wa kupata saratani ya mlango wa kizazi ikiwa ni pamoja na kuanza kufanya ngono katika umri mdogo, kuwa na wapenzi wengi, uvutaji wa tumbaku na kwa wanao ishi na maambukizo ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mkakati wa kuweka zuio la kuo a kwa wanaume ambao hawajatahiriwa. Aidha, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeweka mikakati dhidi ya kujikinga na kirusi hiki ikiwemo utoaji wa chanjo dhidi ya kirusi cha papilloma kwa wasichana wa umri ya miaka 9-14 kote nchini, sambamba na chanjo tunahakikisha tunatoa elimu juu ya kubadilisha tabia, ikiwepo pia kuhamasisha kufanya tohara kwa wanaume, kwani wanaume waliofanyiwa tohara hawapo kwenye hatari ya kuwa na kirusi hiki (cha Papiloma) kinachosababisha saratani.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanawake ambao wameshapata maambukizo ya kirusi cha papilloma tunahamasisha kufanya uchunguzi wa kutambua uwepo wa mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na kuwapatia tiba ya ugandishaji kwa kutumia kimiminika cha gesi ya *carbon dioxide*.

**SPIKA:** Katibu tena.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**AZIMIO LA BUNGE**

**Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa namna alivyoliongoza Taifa katika Mapambano Dhidi ya Janga la Ugonjwa wa *Corona (COVID-19)***

**SPIKA:** Ahsante sana. Baada ya utangulizi huo wa Katibu wa Bunge sasa nimuite mtoa hoja. Mtoa hoja tafadhali hapo hapo ulipo.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Azimio la Bunge la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa namna alivyoliongoza Taifa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa *Corona (Covid-19)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa namna alivyoliongoza Taifa letu katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na virusi vya *Covid 19* maarufu *Corona*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Ofisi yako kwa kuruhusu kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha hoja ya kutambua na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wetu kwa jitihada, mbinu, mikakati madhubuti alioitumia katika kukabiliana na ugonjwa hatari wa *Corona* ambao umekuwa ni tishio kwa uhai na usalama wa wananchi hapa nchini na dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ugonjwa wa *Corona*, Mheshimiwa Rais alitumia mbinu na mikakati mbalimbali ikiwemo kukataa kabisa kuiga mtindo (*fashion*) wa kufunga mipaka na kuwafungia wananchi wake wasitoke nje tofauti na viongozi wa Mataifa mengine waliofunga mipaka ya nchi yao na kuwazuia watu kutoka nje (*lockdown*).

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kufunga mipaka na kuwafungia wananchi ndani siyo jambo rahisi wala la kukurupuka, kwani uamuzi wa namna hiyo ungeumiza sana uchumi, wananchi na Taifa letu kama ambavyo imetokea kwa Mataifa mengine. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais wetu hakufanya hivyo na badala yake alibuni mbinu na mikakati ya kipekee katika kukabiliana na janga la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutambua madhara ya kufunga mipaka na kuwafungia watu wetu ndani, wapo baadhi ya Wanasiasa katika nchi yetu waliotaka Rais wetu aige mtindo huo ambao umesababisha mateso makubwa kwa wananchi kwenye nchi zilizotumia mtindo huo. Nafarijika kuona kwamba Mheshimiwa Rais wetu hakufanya hivyo kwa maslahi mapana ya usalama wa wananchi na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na janga la *Corona*, Rais wetu alionyesha uongozi thabiti ambao umewezesa kukabiliana na maambukizi ya virusi vya *Corona* bila kuwatesa wananchi na bila kuathiri shughuli za kiuchumi za nchi yetu. Mathalan, mbinu na mikakati alioitumia Mheshimiwa Rais wetu ilizingatia hali halisi na uwezo wa kiuchumi kwa wananchi ambao wengi wao kipato chao ni cha kujikimu (*hand to mouth on daily basis*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, Rais wetu aliruhusu shughuli za kiuchumi na baadhi ya shughuli za kijamii ziendelee kwa tahadhari ya kuwahimiza wananchi kuzingatia maelekezo na miongozo ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, mbinu na mikakati alioitumia Mheshimiwa Rais wetu katika kukabiliana na janga la *Corona* ni pamoja na:-

(i) Kuunda Kamati maalum iliyoongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kikosi kazi cha kudhibiti na kukabiliana na janga la *Corona*. (*Makofii*)

(ii) Kutenga hospitali na maeneo maalum ya kutoa huduma kwa watu walioambukizwa na virusi vya *Corona*. (*Makofii*)

(iii) Kufunga kwa muda shule za Awali, Msingi, Sekondari, Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu. (*Makofii*)

(iv) Kusitisha shughuli zote za michezo, mikusanyiko, warsha na makongamano. (*Makofii*)

(v) Kuwaondoa hofu Watanzania na badala yake kuwataka wachukue ugonjwa wa *Corona* kama magonjwa mengine jambo ambalo kwa kiasi kikubwa lilipunguza hofu na tataruki iliyokuwepo katika jamii. (*Makofii*)

(vi) Kukemea unyanyapaa (*stigma*) kwa wagonjwa wa *Corona* na miili ya watu waliopoteza maisha kwa ugonjwa wa *Corona*. Tulishuhudia Rais wetu akitoa tamko na kutaka wagonjwa wa *Corona* wahudumiwe kama wagonjwa wengine. Aidha, Rais wetu alielekeza mamlaka zake kuruhusu Ndugu kuzima miili ya watu wao waliopoteza uhai kwa ugonjwa wa *Corona* kwa kufuatia mila na desturi zetu.

(vii) Kuruhusu shughuli za ibada kufanyika kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na *WHO* na watalaam wa Wizara ya Afya.

(viii) Kumontanguliza Mwenyezi Mungu kwa kuomba viongozi wa dini kuwahimiza Watanzania kufunga na kumwombaa Mwenyezi Mungu aliepushe Taifa na janga la ugonjwa wa *Corona*.

(ix) Kuwataka Watanzania kutumia mbinu mbadala kama vile kutumia dawa za asili ikiwemo kujifikiza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mbinu na mikakati hiyo, Taifa letu limeweza kudhibiti ugonjwa wa *Corona* na ndio maana idadi ya wagonjwa na kasi ya kuenea kwa virusi vyaa *Corona* imeshuka sana. Sasa hatusikii tena visa vipyaa vyaa wagonjwa wa *Corona* wala vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wa *Corona*.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwasilishe Azimio la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna alivyoliongoza Taifa katika Mapambano dhidi ya janga la ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na virusi vyaa *Covid 19* kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, mbinu na mikakati aliyoitumia Rais wetu kukabiliana na janga la *Corona* ni mbinu rafiki na halisi kwa aina ya uchumi na maisha ya wananchi wetu;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati hiyo imesaidia kuwalinda wananchi kuokoa maisha ya watu wengi waliouqua ugonjwa wa *Corona* na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa huo;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati aliyoitumia Rais wetu imesaidia kulinda wananchi na uchumi wa nchi yetu;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati aliyoitumia Mheshimiwa Rsis imeipa nchi yetu sifa na kuwa mfano wa kuigwa (*model*) na baadhi ya Mataifa makubwa duniani na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa; (*Makof*)

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Rais na Serikali yake imeweza kukabiliana na janga la *Corona* kwa kutumia fedha zetu tofauti na nchi nyingine, zime lazimika kukopa kutoka kwenye Taasisi za kifedha duniani; (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imempelekea Rais wetu. Samahani... (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali hii imempelekea Mheshimiwa Rais wetu kuruhusu Vyuo vifunguliwe kuanzia tarehe 1 Juni, 2020 na wanafunzi wa Kidato cha Sita kurudi mashulenii kuijandaa na mitihani yao ya Taifa;

Mheshimiwa Spika, vilevile Rais wetu ameruhusu shughuli mbalimbali za michezo, burudani ziendelee kwa kuzingatia miongozo maalum iliyotolewa na Wizara ya Afya. Hatua hi Imerudisha furaha na kuimarisha afya zetu, afya ya watu wetu baada ya kuwa kwenye kifungo cha kukosa burudani kwa kipindi ambacho shughuli hizo zilisimamishwa.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Rais wetu ameruhusu kufunguliwa kwa anga la nchi yetu na hivyo kutoa fursa kwa ndege za Kimataifa kuleta watalii na uwekezaji mbalimbali nchini. Hatua hii ni siahara tosha kwamba siyo muda mrefu uchumi wetu utarudi katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upekee wa mbinu na mikakati ya kukabiliana na janga la *Corona* alioitumia Mheshimiwa Rais wetu kwa kuzingatia maelezo ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufulsi kwa namna alivyoliongoza Taifa katika mapambano ya janga la *Corona* la Homa ya Mapafu unaosababishwa na virusi vyta *Covid 19* kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, mbinu na mikakati alioitumia Rais wetu ya kukabiliana na janga la *Corona* ni mbinu rafiki na halisi kwa aina ya uchumi wa maisha ya wananchi wetu;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati hiyo imesaidia kuwalinda wananchi kuokoa maisha ya watu wengi waliougua ugonjwa wa *Corona* na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa huo;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati aliyoitumia Rais wetu imesaidia kulinda uchumi wa wananchi na uchumi wa nchi yetu;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati aliyoitumia Rais wetu imeipa nchi yetu sifa ya kuwa mfano wa kuigwa (*role model*) na baadhi ya Mataifa makubwa duniani na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa;

NA KWA KUWA, Rais na Serikali yake imeweza kukabiliana na janga la *Corona* kwa kutumia fedha zake tofauti na nchi nydingine ambazo zililazimika kukopa fedha nydingi kwa ajili ya kukabiliana na janga hili;

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati iliyotumiwa na Rais wetu imewezesha shughuli za kiuchumi na baadhi ya shughuli za kijamii kuendelea kama kawaida; na

NA KWA KUWA, mbinu na mikakati aliyoitumia Mheshimiwa Rais imewezesha Bunge kuendelea na majukumu yake kwa kujadili, kupitisha Bajeti ya Serikali, Miswada ya Sheria na hoja mbalimbali muhimu kwa wananchi kwa ustawi wa nchi yetu;

KWA HIYO BASI, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa 19, Kikao cha 41 cha Tarehe 9 Juni, 2020 linaazimia kwa dhati kumpongeza Jemadari, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa namna alivyoliongoza Taifa na mbinu za mikakati aliyoitumia kukabiliana na ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na virusi vya *Covid 19* maarufu kama *Corona*. Mbinu na mikakati hiyo imeifanya nchi yetu kutoyumba kiuchumi na kuwezesha shughuli za maendeleo kuendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kutoa hoja. Ahsante.

**AZIMIO LA KUMPONGEZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, KWA NAMNA ALIVYOLIONGOZA TAIFA KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA JANGA LA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Kanuni ya 54 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016)

---

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupidisha Azimio la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa namna alivyoliongoza Taifa letu katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya *Covid19* maarufu kama Corona.

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na ofisi yako kwa kuruhusu na kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha Hoja ya kutambua na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu kwa jithada, mbinu, mikakati madhubuti aliyotumia katika kukabiliana na ugonjwa hatari wa Corona ambao umekuwa tishio kwa uhai na usalama wa wananchi hapa nchini na dunia nzima.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na ugonjwa wa Corona Rais wetu alitumia mbinu na mikakati mbalimbali ikiwemo kukataa kabisa kuiga mtindo (fashion) wa kufunga mipaka na kuwafungia wananchi wake wasitoke nje tofauti na viongozi wa Mataifa mengine waliofunga mipaka ya nchi zao na kuzuia watu wao kutoka nje (*lockdown*).

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa kufunga mipaka na kuwafungia wananchi ndani sio jambo rahisi wala la

kukurupuka kwani uamuzi wa namna hiyo ungeumiza sana uchumi wa wananchi na taifa letu kama ambavyo imetokea kwa mataifa mengine. Ndio maana Rais wetu hakufanya hivyo na badala yake alibuni mbinu na mikakati ya kipekee ya kukabiliana na janga la Corona.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kutambua madhara ya kufunga mipaka na kuwafungia watu wetu ndani, wapo baadhi ya wanasiasa katika nchi yetu waliotaka Rais wetu aige mtindo huo ambao umesababisha mateso makubwa kwa wananchi kwenye nchi zilizotumia mtindo huo. Nafarijika kuona kwamba Rais wetu hakufanya hivyo kwa maslahi mapana ya usalama wa wananchi na nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabilana na janga la Corona Rais wetu ameonesha uongozi thabiti ambaو umewezesha kukabiliana na maambukizi ya virusi nya Corona bila kuwatesa wananchi na bila kuathiri shughuli za kiuchumi za nchi yetu. Mathalani, mbinu na mikakati aliyotumia Rais wetu ilizingatia hali halisi ya uwezo wa kiuchumi wa wananchi ambaو wengi wao kipato chao ni cha kujikimu yaani *hand to mouth on daily basis*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hali hiyo, Rais wetu aliruhusu shughuli za kiuchumi na baadhi ya shughuli za kijamii ziendelee kwa tahadhari na kuwahimiza wananchi kuzingatia maelekezo na miongozo ya wataalam.

**Mheshimiwa Spika**, Mbinu na mikakati aliyotumia Rais wetu kukabiliana na janga la Corona ni pamoja na:

**Mosi**, kuunda Kamati Maalum iliyoongozwa na Waziri Mkuu na Kikosi kazi cha kudhibiti na kukabiliana na janga la Corona;

**Mbili**, kutenga hospitali na maeneo maalum ya kutoa huduma kwa watu walioambukizwa virusi nya corona;

**Tatu**, kufunga kwa muda shule za awali, msingi na sekondari, vyuo nya katni na vyuo vikuu;

**Nne**, kusitisha shughuli zote za michezo, mikusanyiko, warsha na makongamano;

**Tano**, kuwaondoa hofu watanzania na badala yake kuwataka wauchukulie ugonjwa wa corona kama magonjwa mengine jambo ambalo kwa kiasi kikubwa lilipunguza hofu na tataruki iliyokuwepo katika jamii;

**Sita**, kukemea unyanyapaa (stigma) kwa wagonjwa wa Corona na miili ya watu waliopoteza maisha kwa ugonjwa wa corona. Tulishuhudia Rais wetu akitoa tamko la kutaka wagonjwa wa corona wahudumiwe kama wagonjwa wengine. Aidha, Rais wetu aliekeza mamlaka zake kuruhusu ndugu kuzika miili ya watu wao waliopoteza uhai kwa ugonjwa wa corona kwa kufuata mila na desturi zetu;

**Saba**, kuruhusu shughuli za ibada kufanyika kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na WHO na wataalam wa Wizara ya Afya;

**Nane**, kumtanguliza Mungu kwa kuwaomba viongozi wa dini na kuwahimiza watanzania kufunga na kumwomba Mwenyezi Mungu aliepushe taifa letu na janga la ugonjwa wa corona; na

**Tisa**, kuwataka watanzania kutumia mbinu mbadala kama vile kutumia dawa za asili ikiwemo kujifukiza.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mbinu na mikakati hiyo, taifa letu limeweza kuudhibiti ugonjwa wa corona ndio maana idadi ya wagonjwa na kasi ya kuenea kwa virusi vya corona imeshuka sana. Sasa hatuskii tena visa vipyta vya wagonjwa wa corona wala vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wa Corona.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo imepelekea Rais wetu kuruhusu vyuo vifunguliwe kuanzia tarehe 1 Juni, 2020 na wanafunzi wa kidato cha sita kurudi mashulenii kujiardaa na mitihani yao ya taifa.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Rais wetu ameruhusu shughuli mbalimbali za michezo na burudani ziendelee kwa kuzingatia miongozo maalum inayotolewa na Wizara ya Afya. Hatua hii itarudisha furaha na kuimarisha afya za watu wetu baada ya kuwa kwenye kifungo cha kukosa burudani kwa kipindi ambacho shughuli hizo zilisimamishwa.

**Mheshimiwa Spika**, halikadhalika, Rais wetu ameruhusu kufunguliwa kwa anga la nchi yetu na hivyo kutoa fursa kwa ndege za kimataifa kuleta watalii na wawekezaji mbalimbali nchini. Hatua hii ni ishara tosha kwamba si muda mrefu uchumi wetu utarudi katika hali ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na upekee wa mbinu na mikakati ya kukabiliana na janga la corona iliyotumiwa na Rais wetu na kwa kuzingatia maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna alivyoliongoza Taifa katika Mapambano dhidi ya janga la ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Covid-19 kama ifuatavyo:

**KWA KUWA**, mbinu na mikakati aliyotumia Rais wetu kukabiliana na janga la corona ni mbinu rafiki na halisi kwa aina ya uchumi na maisha ya wananchi wetu;

**NA KWA KUWA**, mbinu na mikakati hiyo imesaidia kuwalinda wananchi na kuokoa maisha ya watu wengi waliouagua ugonjwa wa Corona na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa huo;

**NA KWA KUWA**, mbinu na mikakati aliyotumia Rais wetu imesaidia kulinda uchumi wa wananchi na uchumi wa nchi yetu;

**NA KWA KUWA**, mbinu na mikakati iliyotumiwa na Rais wetu imeipa nchi yetu sifa na kuwa mfano wa kuigwa (model) na baadhi mataifa makubwa duniani na jumuiya mbalimbali za kimataifa;

**NA KWA KUWA**, Rais na Serikali yake imeweza kukabiliana na janga la Corona kwa kutumia fedha zetu tofauti na nchi nyingine ambazo zimelazimika kukopa fedha nyingi kwa ajili ya kukabiliana na janga hili;

**NA KWA KUWA**, mbinu na mikakati iliyotumiwa na Rais wetu imewezesha shughuli za kiuchumi na baadhi ya shughuli za kijamii kuendelea kama kawaida;

**NA KWA KUWA**, mbinu na mikakati aliyotumia Rais imewezesha Bunge Kuendelea na majukumu yake ya kujadili na kuitisha Bajeti ya Serikali, Miswada ya Sheria na hoja mbalimbali muhimu kwa maisha ya wananchi na ustawi wa nchi yetu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa, Kikao cha Arobaini na Moja cha tarehe 9 Juni, 2020 linaazimia kwa dhati kumpongeza Jemedari, Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna alivyoliongoza Taifa na mbinu na mikakati aliyotumia kukabiliana na janga la ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Covid-19 maarufu kama Corona, mbinu na mikakati hiyo imefanya nchi yetu kutoyumba kiuchumi na kuwezesha shughuli za maendeleo kuendelea kama kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru sana na naomba kutoa hoja.

Esther M. Mmasi (Mb)  
**VITI MAALUM (CCM)**

09 Juni, 2020

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja litolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono sana. Ahsante sana Mheshimiwa Ester Mmasi kwa kuwa mtoa hoja

kwa siku ya jioni ya leo, hoja muhimu sana ambayo kipekee inatutaka sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano tuazimie kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna anavyoliongoza Taifa katika mapambano dhidi ya janga la ugonjwa wa *Corona* (*Covid 19*).

Basi sasa moja kwa moja tunaingia katika uchangiaji, tuweze kuona tunaendeleaje. Ningependa mchangiaji wa kwanza awe Mheshimiwa Riziki Lulida. Mheshimiwa Riziki kama uko tayari hapo nikupe heshima ya kuwa mchangiaji wa kwanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Hamidu Bobali ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru sana. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema na afya aliyenijalia. Nawaombeni Wabunge wenzangu tukiongozwa na wewe Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge na Watanzania wote wanaotusikiliza sasa hivi, Mungu awabariki sana na Mungu awaongoze katika kila liliokuwa jema katika kuiongoza nchi yetu na kutuepusha na hii *Covid19* kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, sina la kusema zaidi ya kutoa shukurani nydingi sana. Tulitegemea sana Tanzania sasa hivi tungekuwa tunalia vilio vingi sana. Pongezi zangu za dhati zinakwenda sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Kwa nini nasema hivi?

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Tanzania tulikuwa tunahitaji kupata kiongozi wa aina yake; kiongozi ambaye anawahurumia Watanzania, kiongozi ambaye ana maamuzi akijua haya maamuzi yako katika mazingira rafiki kwa Watanzania, kiongozi ambaye hana kiburi. Mtu ye yeyote ambaye hamtegemei Mwenyezi Mungu, basi ana kiburi, lakini Mheshimiwa Rais alihakikisha kuwa anavua nafasi yake ya Urais na kumtegemea Mwenyezi Mungu na alikiepusha kiburi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kama Riziki, nasema, mimi mwenyewe binafsi na familia yangu na wananchi wangu wa kutoka Mkoa wa Lindi, tunampongeza kwa dhati kwa huruma ambayo ameionyesha. Natamani kulia, lakini sisemi sana, Mungu atakuwa shahidi kwa hili. Mheshimiwa Rais amepitia kipindi kigumu sana. Anapitia kipindi ambacho yeche ana ujasiri wa kutaka Watanzania watoke, lakini anakutana na kundi ambalo linataka kumdhooifisha akate tamaa, haiwezekani. Ni lazima tumuunge mkono na tupambane na wale ambao hawataki kuisaidia nchi hii, wanataka kururudisha nyuma Tanzania yenye maendeleo chini ya Rais Jemedari, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli inawezekana.

Mheshimiwa Spika, nazungumza kama Mbunge Mpinzani, lakini penye ukweli sitakuwa mnafiki, nimeshindwa. Ukweli utabakia ukweli; maana nilizungumza siku moja ndani ya Bunge hili, nitaogopa kushika *Quran* halafu niwe mwongo. Nami nimeshika *Quran* ili niwe mkweli. Leo bila Mwenyezi Mungu tusingekuwepo humu ndani, tulishapata hofu kuwa Bunge zima tungekufa, lakini ametutoa hofu na ameifanya nchi imeondokana na hofu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaichukulia *Corona Viruses* kama UKIMWI, kama Malaria na kama magonja mengine ambayo binadamu wa kawaida anaweza akafa. Leo tungekuwa ndani tungekuwa wapi saa hizi? Halafu bado wanatuchomekea madeni na mikopo; kopeni ili tuzidi kuingia katika janga la dhiki ya kuingiza nchi katika umasikini. Hii haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, vilevile mimi kama Mbunge kwa nini nampongeza? Katika kipindi hiki kigumu ameamua kufanya kazi kwa ugumu wake. Mfano, leo Lindi tumepata fursa kubwa sana; Wanalindi kama sijawatetea na kumpongeza kwa niaba yao, watapata wapi fursa kama hii? Katika kipindi kifupi, Lindi Mkoa ambao ulikuwa mwisho kiumasikini, amesaini mkataba mkubwa wa LNG. Leo wananchi wa Lindi wamelipwa shilingi bilioni 5.2 ili kuwaleta wawekezaji wakiwa huru.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda Lindi, niliyoyaopna Lindi toka nimeanza kuingia Bungeni sijaona. Ameweka uwazi mara tatu:-

(i) Wale wanaolipwa fidia, Wanasheria walikuwepo pale kwa ajili ya kuwasimamia, endapo atakuwa haridhiki Mwanasehria amsikilize.

(ii) Afisa Ardhi yuko pale; kama amemwandikia heka 10 au amepunguza ama ameongeza anatakiwa atoe majibu mbele ya watu bila kukaa pambeni;

(iii) La mwisho, mimi kama Mbunge kwenda kusimamia kuona: Je, haki za Wanalindi ambazo tulizipigania muda mrefu zimepatikana? Nilikuwepo nami mwenyewe ndio umenipeleka Lindi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hali hiyo ya maendeleo ya Mkoa wangu wa Lindi niseme hapana! Nitakuwa mnafiki, siwezi kukubali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wanalindi wametoka pale wamefurahi, tunaenda kupata mradi wa kwanza mkubwa wa maendeleo ya viwanda ambao utatuletea ajira kubwa Tanzania nzima na Wanalindi wataipata ile fursa. Fursa ile ambayo tulikuwa tunaitegemea tuwapelekee mboga za majani, tuwapelekee chakula, tungeipata wapi wakati tulikuwa tunaangalia miradi Mwanza, Dodoma? Leo fursa imekwenda Lindi, kuchele!

Mheshimiwa Spika, leo tunaizungumzia juzi tarehe 4, nimekwenda tena Lindi kwenda kuzidua mradi mkubwa wa gesi asilia, na wameongea shahidi walikuwepo wenzangu kuwa hata mtu una nyumba ya udongo utafungiwa mtambo wa gesi na utakuwa unaweza kutumia gesi katika nyumba yako ya udongo na makuti kwa vile haikumtenga kuwa lazima wewe tajiri ndiwe utapata fursa hii, hata yule masikini amekuwa ndani yake.

Mheshimiwa Spika, nikuambie la mwisho, Lindi mradi wa REA umekwenda kwa asilimia 90. Nataka nizungumzie kwa majina maana wataona mimi hapa nazungumza kwa unafiki, sitaki unafiki. Kutoka mchingga mpaka kijiweni umeme, kutoka Chikonji mpaka Nagaru umeme, kutoka Ngongo mpaka Milola umeme, kutoka Mkwajuni mpaka vipingi umeme, majimbo yote mpaka Liwale kote kuna umeme. Jamani tuache dharau na chuki ambazo hazina maana.

Mheshimiwa Spika, tuongee yaliyokuwa na ukweli, ukiongea ukweli utakuwa mpenzi wa Mwenyezi Mungu; tusirudi kwa kutaka watu wachache ambao wanaona lakini wanajifanya hawana macho. Kila kilicho kituzuri wanakiona lakini wanakipuuzia lakini Mungu atawashinda kwa vile tupo pamoja naye kuhakikisha utawala wake huu tumuunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza katika Bunge liliopita kuwa jamani kama ingewezekana fedha hizi ambazo zilitaka ziende kwenye uchaguzi zitumike zaidi kwa ajili ya haya maendeleo ambayo ameyakusudia. Sitaki kuonea mengi kwa vile ninayo yaona shule tunaziona, hospitali tunaziona, miradi mikubwa tunaiona, lakini watu wanafumba macho eti kuhakikisha wao wanaowapa maneno yale wanaona wasibishe. Wao wana sayansi, waliokuwa na sayansi kubwa; leo Corona iko Marekani ina maana wale hawakumshiba Mwenyezi Mungu, na kwavile hawakumshiba Mwenyezi Mungu amewaonyesha kwamba mimi bado niko hai.

Mheshimiwa Spika, Marekani leo wana corona kuliko Tanzania watu ambao ni malofa, masikini lakini Mungu ametuona zaidi. Sasa leo azungumze maandamano yanayofanyika Marekani ya kuwapinga watu weusi na kuwanyanyasa watu weusi wako wapi humu ndani zaidi kukimbia kimbia Bunge? Wataendelea kulikimbia Bunge tutabakia Bungeni tutafanya kazi kwa asili na haki ya Watanzania na mpaka mwisho wa Tanzania tujuwe kabisa hii ni nchi yetu maendeleo yetu na Rais wetu atatusaidia kutukomboa kutoka kututoa katika umasikini.

Mheshimiwa Spika, utanisamehe sana kuwa mimi ninaongea siyo ninaongea ninaongea kuhakikisha kuwa nina mfahamu Rais wangu tangu akiwa Waziri wa Ujenzi, bajeti zake zikija hapa ilikuwa hakuna mtu anayepinga kwa maana moja kuwa maono ya Mwenyezi Mungu yalionekana tangu siku nydingi. Ilikuwa akija hapa hakuna mtu aliyekuwa anataka kupingana naye, Wizara mbili zilikuwa hazipati taabu, Wizara yake na akija hapa Mheshimiwa Mwingi. Mheshimiwa Hussein Mwinyi kokote anapokwenda alikuwa hapati taabu; hii yote ni mfano hai kuwa hawa watu ni watu waliotukuka, na tuwaombee duwa sana, tumuombe dua sana Mheshimiwa Rais afanye kazi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na ndiyo maana akubagua dini, hakubagua muislamu, a mkristo hata buza, ameakikisha watu wote Watanzania, mpaka mpagani anapata haki ndani ya nchi yake.

Mheshimiwa Spika, sina la zaidi ya kusema Mungu ibariki Tanzania, Mungu Mbariki Mheshimiwa Magufuli, Mungu wabariki Watanzania wote tuwe naye twende naye pamoja ili mafanikio haya tunayoyataka ndiyo haya tunayataka, tunataka maendeleo yaliyotukuka na duniani yote inaiona Tanzania ni mfano katika Afrika. Tuachane na watu wanaotukatisha tamaa waende mbele lakini Mwenyezi Mungu atutangulize katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema pale nawashukuruni sana ahsanteni sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida kwa kutuwekea msingi wa majadiliano yetu, hakika tumefarijika sana kwa maneno yako. Nilishakutaja Mheshimiwa Senator Mwambaliaswa utafuatiwa na Mheshimiwa Bobali halafu tutaendelea.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naupongeza sana uongozi wa Bunge wewe mwenyewe Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge kwa kufikiria kuleta azimio hili mbele ya Bunge leo, ninawashukuru sana kwa maono haya. Napenda kumpongeza mtoa hoja, umeitoa vizuri na hoja yako imenyooka.

Mheshimiwa Spika, mimi ni muhana wa hoja hii, mimi kama unavyojuwa ilibidi nijitege kwa wiki mbili kwa sababu nilimpoteza rafiki yangu mpenzi, sijui kama ni kwa ugonjwa huu au kwa magonjwa mengine. Ninakushukuru sana wewe uliniangalia vizuri mpaka baada ya wiki mbili nimeendelea kufanya kazi kama walivyonituma wananchi wa Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa azimio linasema Mheshimiwa Rais yeye ametumia mbinu tatu kubwa kupambana na janga hili. Ya kwanza alimtumia Mwenyezi Mungu, ya pili mbinu za kisayansi, la tatu mbinu za Kiafrika mbinu za Kitanzania. Naomba kwa ruhusa yako nianze na neno la Mungu kabla sijaendelea kwa ruhusa yako nasoma neno ambalo nilisoma hatu wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kitabu cha Mambo ya Nyakati wa Pili, nianzie Mlango wa Kumi na Moja. Kwa msaada wa Mungu nasoma;

*"Hivyo Selemani akamaliza Nyumba ya Bwana na Nyumba ya Mfalme na yote yallyomwingia Selemani moyoni mwake ayafanye Nyumbani mwa Bwana na nyumbani mwake mwenyewe akayafanikisha. Bwana akamtokea Selemani usiku (Mungu kamtokea selemani usiku); "akamwambia, nimesikia uliyoyaomba, na mahali hapa nimejichagulia kuwa nyumba ya zabihu" (anasema Mwenyezi Mungu) "nikizifunga mbingu isiwe mvua mimi Mwenyezi Mungu, tena nikiamuru nzige kula nchi" (kama nzige waliovamia mwaka huu) au "nikiwapelekeea watu wangu tauni" (kama corona), sasa anaendelea; "ikiwa watu wangu niliowahita kwa jina langu wakijinyenyekesha na kuomba nakunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya basi nitasikia kutoka mbinguni na kuwasamehe zambi yao na kuiponya nchi yao". (Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, baada ya janga hili kutupata nchi nyangi za wakubwa mbinu yao kubwa ya kwanza ilikuwa ni kufunga mipaka na kuwafungia wananchi wao ndani ya nyumba yao, na wakataka dunia nzima iinge hiyo hiyo, iinge kufunga mipanga na kuwafungia wananchi wao ndani ya nyumba kwa miezi miwili mitatu. Kwetu sisi huku Afrika wakawa wanatuletea na vifaa vyta kutumia ambavyo hatujui vimetoka wapi? Pia wanatu-*entice* tuchukuwe mikopo ya kupambana na janga hili; badala ya kutupa misaada mikopo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alikataa, alikataa kufuata ya kwao kama ilivyosema Azimio akafuata ya kwake ambayo yanababu za msingi nyangi tu kama ilivyosema Azimio niongeze sababu nyagine tatu nne kama ilivyosema Azimio watanzania wengi hapa kwetu hapa ni daywaka unawafungia ndani ya nyumba unawahuwa anataka apate shilingi 2,000 kwa leo apelike nyumbani wakale alafu hao unawafungia ndani ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, ya pili Mheshimiwa Rais alishasema wakati huu kwetu hapa Tanzania wakati wa kilimo, tunalima tupate mavuno, mazao ya kula mwaka kesho na miaka inayofuata unawafungia ndani wakulima ili mwaka kesho njaa jje ituuwe, alikataa Mheshimiwa Rais. Pia Tanzania Mwenyezi Mungu ametubariki sana, tumezungukwa na nchi zaidi nane, Mheshimiwa Rais akasema kama tukifunga mipaka tutawatesa wananchi wa nchi hizo nane, akakataa. Pia Mheshimiwa Rais anasema *lockdown* hii mpaka lini? kwa sababu ugonjwa huu umekuja, tunao, utakuwepo; ndiyo maana Mheshimiwa Rais akatumia mbinu zake kama Azimio linavyosema.

Mheshimiwa Spika, tumeiga mno, mimi naompongeza sana Mheshimiwa Rais, tumeiga mno, tumeiga kutembea, tumeiga kuvala, tumeiga kusema, tumeiga hata kula chakula kwa umma, unakula samaki kwa umma na kijiko una kula kuku kwa umma na kijiko, tumeiga kwamba kwenye sherehe unavaa nguo nyeupe, kwenye msiba unavaa nguo nyeusi tumeiga, tumeiga, wanatusukumia tu rangi yetu nyeusi

kwenye msiba tunava nguo nyeusi, kwenye sherehe tunavaa nguo nyeupe. Ifike mahala tubadilike, mashela yawe ya harusi yawe blue, meusi, mekundu au kijani; tubadilike.

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa kwamba historia ipo inasema hawa wakubwa hawa tunajua kabisa kuna mabara mawili matatu ambayo si yao waliyavamia, wananchi wa nchi zile hawajui walikowapeleka, wako wanatanua huko. Sasa hivi baada ya kuona huko kumejaa kwenye mabara ambayo walinyanganya macho yao yako Afrika, watatumia kila mbinu kama alivyosema Mheshimiwa Rais; wanatupa vifaa ambavyo hujawi zimetoka wapi wanataka ardhi yetu, wanataka rasilimali zetu. Kwa hiyo waafrika naomba tuamke tujuwe kwamba watu wanataka nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, bwana Yesu alipozaliwa hawakuntambua, mpaka leo hawamtambui, wanasema kwao atakuja; na utaona kwamba anavyoishi wanamatatizo sana mpaka kesho kutwa mtume Muhammad Swalalwahu Aleihi Wassalam alikozaliwa walimkataa akakimbia wakampokea kwingine.

Mheshimiwa Spika, umeona nchi nyangi hapa Afrika wanataka waongozwe na Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Nchi nyangi hapa Afrika wanataka wangekuwa na Rais kama Dkt. John Pombe Magufuli. Watanzania Mungu ametupa kifaa hiki tukitumie tusije tukawa kama wenzetu.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuunga mkono mia kwa mia azimio hili, lakini vile vile niseme kwa lugha ya kwako, muwaha bmulungu dahavyeka kachipela mtemi mswanu chintumamile sandeni. (*Makof!*)

**SPIKA:** Sikujuwa kama *Senator* anafahamu kigogo; amekiongea vizuri sana; kwamba Mwenyezi Mungu ametupatia mtawala mwema. Tumshukuru Mungu na tushirikiane naye. Ahsante sana Mheshimiwa *senator*, na tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri sana.

Mheshimiwa Hamidu Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini, Baba Paroko.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa Namna Alivyoshughulikia Janga hili la Corona.

Mheshimiwa Spika, kwanza niliweke wazi msimamo wangu juu ya jambo hili la corona. *Specifically mimi ninaunga mkono kumpongeza Mheshimiwa Rais; na nitatoa sababu tatu kubwa.*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaeleza kwanini namuunga mkono juu ya jambo hili la corona. Mimi bado kijana nimetoka shule juzi juzi tu na nilisomea maswala ya *Leadership*. Nitataka kunukuu maneno machache aliyoyasema John Maxwell kwenye sifa za kiongozi bora (*leadership qualities*) nitazitaja kwa uchache, alizitaja kumi na tano kwa lugha ya kwao, *"honest and interpreter, confidence, inspire others, commitment and passion, good communicator, decision making and capability, accountability, delegation and empowerment, creativities and innovation, impasse, resilience, emotion intelligence, humanity, transparency vision and purpose"*

Mheshimiwa Spika, nimezitaja hizi kumi na tano lakini nitazielezea walau chache kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameshughulikia janga la corona.

Mheshimiwa Spika, moja ya sifa kubwa ya hizi ambazo nimezisema ni sifa ya *innovation*, kuwa mbunifu, kubuni. Na katika sifa ya *innovation* John Maxwell anasema kiongozi mzuri ni yule anayetengeneza njia akaifuata ile njia na pia akaionesha wengine waifuate. Hii ni sifa inayotofautisha kiongozi (*a leader and follower*) na wale watu wanaomfuata. Kwa mujibu wake yeche Maxwell ndiyo maana halisi ya kiongozi.

Mheshimiwa Spika, laiti kama nchi leo ingekuwa tumeamua kufanya *lockdown* leo tungkuwa tunazungumza maafa makubwa ya watu kupoteza maisha kwa njaa, na shida zingine. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono azimio hili kwa sababu tatu kama nilivyosema; kwanza kitendo cha kukataa mikopo ni jambo la kizalendo; madeni tuliyonayo ni makubwa. Kama kweli mikopo hii ilikuwa na faida na tija hiki ni kipindi ambacho watoaji wa mikopo wangetusamehe kwanza tulionayo halafu ndipo wakatuambia twende tukachukuwe mikopo yao. Lakini huku unalipa bilioni mia sita hadi mia saba kwa mwezi alafu baadaye anakwambia njoo uchukuwe mkopo mwingine; huu ulikuwa ni ukandamizaji wan chi masikini na zile zinazoendelea kama nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, dhana ya *lockdown* kwa Tanzania ni dhana mfu kabisa. Hauwezi ku-*apply lockdown* Tanzania, hata nchi zingine za Kiafrika hauwezi ku-*apply lockdown* nchi za Kiafrika.

Mheshimiwa Spika, mimi najiuliza hivi huko kunakofanyika *lockdown* mbona leo kuna fanyika maandamano ya George Floyd; watu karibu milioni tatu milioni nne wapo barabarani wanaandamana hiyo *lockdown* inafanyika wapi sasa?

Mheshimiwa Spika, kuachia shughuli za dini ziendelee hii ni sababu ya tatu kabisa mbayo mimi naunga mkono. Taifa lisilokuwa na hofu ya Mungu; mimi ni muislam, na sisi katika imani tumeelezwa panapotokea majanga kuna dua za kuomba na kuna namna ya kufanya. Sasa inatokea majanga ninyi ndiyo mnafunga misikiti, mnafunga makanisa, hamwendi kuabudu; huyo Mungu mnamuombea wakati gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye suala la kuachia shughuli za dini ziendelee kuendelea hili ni jambo ambalo limesababisha mimi niunge mkono Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais. Na katika hili; hili ni Bunge la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, ningependa *appeal* na kutoa pendekero; hata wale wenzetu wa Saudi Arabia ambako mwezi mmoja mbele kuna ibada ya Makkah wangeachia wangefungua ile misikiti watu wakaenda wakaabudu tukafanya ibada ya kumuomba Mwenyezi Mungu kwa sababu ni njia mojawapo unapopata matatizo kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, Jambo lingine, ningetoa wito kwa Mheshimiwa Rais atumie nafasi yake ya kuwa MwenyeKITI wa SADC kuonesha njia ya kuwaeleza Marais wengine wa SADC nini kinapaswa kufanyika kwa wakati huu ili kuweza kupambana na janga hili; watumie *model* ya Tanzania ili kuweza kuokoa uchumi wa eneo la kusini mwa Afrika, nchi wanachama wa SADC; hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, unaona leo watu wanapata shida, jana nilikuwa naangalia kwenye TV madereva wa Tanzania wale wanaobeba magari kupeleka kule Rwanda wakifika mpakani wanaacha magari halafu wanachukuliwa na madereva wa nchi nydingine wanapeleka huko Iakini madereva wa kule wanaingia mpaka bandarini Dar es Salaam. Hawa wakwetu wakifika wanakwenda wanapimwa na wanawekwa kwenye eneo maalumu; nimesikia watu wa TATOA jana wanazungumza; Iakini wa kwao wanakuja mpaka bandarini Dar es salaam wanakuja wanachukuwa wanaondoka.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Rais atumie jukwaa alilonalo la kuwa MwenyeKITI wa SADC awaeleze. Mimi sina shaka kwasababu kwa jimbo kama la kwangu la Mchinga sijawahi kusikia kisa na hajjawahi kutokea kisa cha mgonjwa wa Corona hata kimoja mpaka sasa. kwaHiyo nazungumza *with authority* kwamba sisi Mchinga hatujawahi kupata kesi ya Corona mpaka sasa na maisha ya kawaida yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni la msingi sana ni kuhusu hofu, hofu, ugonjwa huu kama si yale maneno ya kutia moyo aliyekuwa anayatoa Mheshimiwa Rais, leo

tungewapoteza watu wengi sana hapa wakati ule tunakuja Bungeni hapa kabla ya haya mambo mengine hizi hatua zingine hazijachukuliwa mtu unajikuta unatetema yani mwili wote unatetemeka hivi unajiliza hivi naumwa, lakini ukienda kupimwa pale *temperature* 32, 33 tangia tumeambiwa kwamba jamani ishini maisha ya kawaida hakuna mwili kutetema, hakuna nini, tunakwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaamini kwamba inawezekana kuna wapendwa wetu tumewapoteza kwa sababu ya kuwa na hofu. Hii ndio kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ni *Chief Comforter* wa nchi na alipotutoa hofu alitekeleza wajibu wake wa kuwa ndio *Chief Comforter* kwenye nchi yake. (*Makofj*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa viongozi wengine wa kiafrika, huu ni wakati wa kujifunza. Jana nilikuwa naangalia *theories*, nilikuwa nasoma, naangalia kwenye *video* mbalimbali, wanazngumzia ugonjwa wenyewe wa *Corona*, nikasikitika sana. Ukiwaangalia wanasayansi wengine wanasema, kuna wanasayansi wa nchi moja wamegundua kwamba ugonjwa wenyewe kumbe siyo wa *virus*, unasababishwa na *bacteria*; wengine wanatuambia ni *virus*; na wengine wanatuambia hata zile mashine zilizokuwa zinawekwa zilikuwa hazina msaada wowote kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye hali ya mazingira ya *contradiction* kama haya, hakuna haja ya kutesana. Nchi za kiafrika zingefungua mipaka tukaendelea kwa sababu tulishatabiriwa wiki nne mbele watu wangekuwa wanadondoka barabarani. Mimi niko Dodoma hapa sasa nina karibu mwezi wa tatu sijawahi kumwona mtu amedondoka barabarani. Huu ni ushahidi ungetumika kwa nchi nyiningine za kiafrika kuendelea kuiga mfumo wa Tanzania kwa sababu sijaona huyo mtu anayedondoka na wala sioni dalili ya kudondoka huko. (*Vigegele*)

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba ugonjwa umeisha au haupo, lakini kwa taarifa tulizonazo na haya

tunayoyashuhudia, kwa sababu kila mtu anaweza akaiangalia familia yake ni nani ameguswa, ni nani ameguswa. Vifo viro na vilikuwepo hata kabla ya *Corona* na bado viro na vitaendelea kuwepo. Kwa hiyo, nafikiri nchi za kiafrika zingeweza kutumia *formula* hii tuliyotumia sisi Tanzania, ingeweza kutusaidia kabisa kwenda huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, wapo marafiki zetu ukizungumza nao, uki-*chat* nao kwenye *WhatsApp* kwenye *Facebook* wanakwambia sisi huku tunapata shida, tuna njaa, wa nchi jirani, hatuwezi kuzisema, lakini unaona kabisa wananchi wanapitia kwenye wakati mgumu kwa sababu tu ya viongozi hawataki kufanya *decision* na hii ndiyo shida. (*Makof/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa vile sisi tumepata *decision maker* amefanya *decision* ya namna hii tunamshukuru na katika mazingira ya ki-*corona* mimi napongeza sana Mheshimiwa Rais katika hatua alioichukua. Niweke wazi kabisa, nimesema napongeza kama mtoa hoja alivyosema, hatua alizozichukua Mheshimiwa Rais juu ya *Corona* isiwe watu wameni-*quote* vibaya. Ninapongeza Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua alizochukua juu ya janga la *Corona*. Hapa ndipo panapokuja dhana ya Waswahili kwamba asiyeshukuru kwa kidogo, hata kwa kikubwa hawezikushukuru. Pia hapa ndipo inapokuja dhana ya neno la Kiswahili, "Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni." (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokipongeza hapa ni *mechanism* aliyoitumia Mheshimiwa Rais kupambana na *Corona*. Kwa hiyo, nataka watu wani-*quote* kwa mtindo huo. Maana yake isije wengine wakasema leo Mbunge wa CUF ndio akubali kila kazi, sasa hayo mambo mengine yana mjadala wake na namna nyingine ya kuyasema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naunga mkono Azimio hili. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamidu Bobali kwa mchango wako mzuri sana. Hakika uliyoyasema ni kweli tupu. Tunaku heshimu sana kwa hilo.

Mheshimiwa Baba Paroko atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Mheshimiwa Selasini tafadhalii.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kukushukuru sana kunipa fursa nami niweze kuchangia Azimio hili. Shida niliyo nayo sijui nitaanzia wapi kwa sababu nimeporwa maneno mengi sana, lakini nianze kwa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Rais Nickson wa Marekani aliwahi kusema kwamba Rais ni mtu anayechaguliwa na watu kwa ajili ya watu. Kama kuna Mtanzania yeyote ambaye alidhani kwamba Rais Dkt. Magufuli ni Malaika, alikosea sana. Ni mtu kama sisi, lakini bahati nzuri Mungu akamtanguliza kuntuongoza, ndiyo maana tuko hapa leo tunajadili uongozi wake kadri Mwenyezi Mungu alivyompa uvuvio.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Mheshimiwa Bobali amesema kwamba Rais ni *comforter in chief*. Ngoja niseme kwa Kiswahili. Rais sio kwamba ni Amiri Jeshi Mkuu peke yake, Rais ni mfariji mkuu. Sasa miaka mitano hapa ziko hoja tumesema hapana. Ndugu zangu, hapa tumesema hapana kwa hoja nydingi tu. Sasa hata hii nayo tunasema hapana! (*Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, hii mimi nasema, ninampongeza Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa sababu amesimama katika viatu vyake sawasawa kuliondolea Taifa hili hofu.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu bila shaka yoyote, hofu imewaua Watanzania wengi sana; waliokuwa na *pressure*, Kisukari, joto lilipopanda kidogo tu *Corona*, wakaondoka bila kuchekiwa bila kufanya chochote. Jithada alizofanya Rais kulileta Taifa pamoja katika janga hili haziwezi kupita bila kuungwa mkono. (*Vigelegele/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vita yoyote inahitaji ushirikiano na kwa wale Wabunge vijana ninawakumbusha vita ya Kagera. Tulihamasishwa na Mwalimu; mwenye kunde, mwenye maharage, mwenye gari, mwenye nguo tulipigana kwa pamoja. Hata hili janga la Corona ni vita. Haiwezekani wala haiingii akilini ambaye ana dhamana anatoa maelekezo, sisi ambaao tunapaswa tuungane naye katika vita hii tunafanya utabiri wa vifo. Haiwezekani, haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Rais Dkt. Magufuli ninafahamu kwamba wote mnakutana name, mnaniita Baba Paroko na ninajisikia; na huwa nikikutana na Maaskofu wangu huwa wananiambia, wewe ni Paroko wa nchi kavu, nawaambia sawasawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, janga hili limeangukia katika kipindi cha Kwaresma, Wakristu tukiwa tunafunga, tukamaliza Kwaresma tukiombea jambo hili; lakini cha ajabu likaangukia kwenye Ramadhani, Waislamu wakafunga kuombea jambo hili. Waislamu mnajua, katika mafundisho yenu Waislamu mmeambiwa janga likitokea Tabora usilifuate, lakini likitokea Dodoma ulipo usilikimbi. Hicho ndicho Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alichokuwa anawaambia Watanzania. Tuko na janga, tusilikimbi, tumkimbilie Mwenyezi Mungu. (*Makofi/Vigelegele*)

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Wakristo mnajua, Biblia imeandika, "amtumainiye Bwana hataaibika milele." Nataka nirudie, "amtumainiye Bwana hataaibika milele." Hiyo ni Zaburi ya 125. Narudia, inasema, "amtumainiye bwana hataaibika milele" (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, alichofanya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ni kuwaambia Watanzania mtumainieni Bwana msiaibike milele; na tumemtumainia Bwana hatujaibika. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa Kanisa Kuu Katoliki Dodoma, tulikuwa na Msiba, Katibu wa Askofu Mkuu wa Wakatoliki Dodoma alifariki Ijumaa. Leo tulikuwa tunafanya ibada kumsindikiza. Katika mahubiri, Askofu alikemea jambo na naona niliseme hapa, kwa sababu wapo wanaoweka maneno katika hotuba za Mheshimiwa Rais. Wako watu mtaani wanatangaza Mheshimiwa Rais kasema *Corona* imekwisha, siyo kweli. Ndicho alichosema Baba Askofu.

Mheshimiwa Spika, Baba Askofu kasema, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuruhusu ibada kufanyika; lakini kasema, Mheshimiwa Rais katuambia tuchukue tahadhari. Kwa hiyo, nawaambia Wakristu kwamba chukueni tahadhari. Kwa hiyo, wale mnaomwekea Mheshimiwa Rais maneno mdomoni kwamba kasema *Corona* imekwisha, siyo kweli, nyie ni warongo. (*Makofi/ Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Warongo!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Lazima tuchukue tahadhari na wakati tunachukua tahadhari tuendelee kumkimbilia Mungu.

**MBUNGE FULANI:** Amen.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, la mwisho, najiuliza; na nikisema hivyo wako wachochazi wanasema eeh, umeunga mkono kule Rombo hupati kura. Ahaa, tutaona itakavyokuwa. Yaani wewe unataka mtu wa Rombo anayekata ndizi Ushiri kupeleka Mamsera aiuze, arudi nyumbani na kilo ya nyama au kilo ya sukari leo unamzuia ndizi yake isiuzwe iozee shambani halafu unasema sitapata kura! Hapana. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Haiwezekani, haiwezekani!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanya jambo la maana kabisa kuhakikisha kwamba nchi hii haifungwi. Ingefungwa siyo

kwamba watu wangepoteza maisha kwa *Corona* tu na kwa njaa vilevile. Mheshimiwa Rais ameonyesha kwamba yeye ni kat i ya Marais Afrika ambao hawapokei amri kutoka huko juu. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, sifa ya viongozi wote duniani ni kuamua na kusimamia ulichoamua. Kwa hili aliamua akasimamia alichoamua na anaendelea kukisimamia kwa kutupa tahadhari, hatuna sababu yoyote ya kutokumpongeza. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kichekesho kidogo ni kwamba yupo Mbunge mmoja alisimama hapa akasema baada ya Marehemu wetu wale ambao tulipata hapa, kama tusipofunga Bunge wataondoka Wabunge wengine kadhaa; na kweli tulikuwa tunaingia hapa kwa wasiwasi sana. Msimamo wako Mheshimiwa Spika wa kuendelea pamoja na ushauri uliopata kwa Mheshimiwa Rais umetufanya sisi leo tuko hapa. Kwa sababu hiyo aliyekuwa anatabiri kwamba kuna Mbunge au Wabunge wataondoka baada ya wale, ameaibika. Uhai ni zawadi ya kwanza kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lazima utetewe. Hata hivyo nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Mungu ni mwenye huruma na huruma ya Mungu haina mipaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wajibu wetu kama Watanzania, wajibu wetu kama viongozi pamoja na kumwomba Mungu atupe karama zinazostahili tuwe viongozi bora, lazima tuombe pia huruma yake katika haya tunayoyafanya kila siku. Kwa sababu hiyo ni ahadi yake na ni ahadi timilifu na kamilifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru asante sana (*Makof/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Selasini, Baba Paroko. Umetukumbusha kuhusu umuhimu wa kumtumainia Bwana. Hakika tumtumainie Bwana. Hapa tunapoelekea mwisho wa shughuli zetu za Bunge la Kumi na Moja, tumtumainie Bwana.

**MBUNGE FULANI:** Amen. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere na Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa Namna Alivyoongoza Taifa katika Kupambana Dhidi ya Janga la Ugonjwa wa *Corona (Covid 19)*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa nguvu na uhai kunisimamisha hapa leo kuweza kuongea humu Bungeni. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuwalinda Wabunge wote mpaka sasa hivi. Bwana Yesu ashukuriwe.

**WABUNGE FULANI:** Amen.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, *Corona* ilivyotokea Mheshimiwa Rais alisimama pamoja na wananchi wake. Mheshimiwa Rais ni muungwana, anatupenda, anakumbatia wananchi wake, ni mcha Mungu na kweli tumepata Rais Tanzania, tunampenda sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Corona* Mheshimiwa Rais ilivyotokea alituwezesha tusiwe na hofu na kweli tupo hapa tunachapa kazi ndani ya Bunge lako. Kwa kweli hatuna hofu, unatuona tunaendelea, tunafurahi, tunafanya kazi kwa bidii. Mheshimiwa Rais alituambia tuchukue tahadhari na kweli tufuate ushauri wa wataalamu wa afya. Ushauri huo umechukuliwa, tumeava barakoa, tumejfukiza, tumejisaniitize tumefanya kila kitu mpaka sasa hivi tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alisema tusijifungie ndani, fanyeni kazi nchi yetu bado ni changa, nchi yetu inataka kukuza uchumi na tusifunge mipaka. Tanzania tumefanya hivyo. Mheshimiwa Rais wanampenda watu wote.

Nikisema watu wote, naamanisha kutoka watoto wadogo mpaka wa kati, mpaka wasomi, watu wote wanampenda Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Dkt. Magufuli Mwenyezi Mungu akubariki kwa jinsi wewe ulivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa kuona hiyo *Corona* aliruhusu ibada. Shule na vyuo vilifungwa kwa tahadhari, lakini kwa kuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu akasema ibada iendelee; na kweli tumesali tumeomba. (*Vigelegele/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Rais alisema tufunge na tuombe kwa siku tatu na kweli kwa kutojali kila mmoja na dini yake, kila mmoja alivyo, watu waliweza kufunga na kumwomba Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna maandiko matakatifu ya vitabu vitakatifu yanasema hivi, ombeni mtapewa, bisheni hodi mtafunguliwa. Kweli tumeomba tumepeewa; *Corona* imepungua, siwezi kusema kuwa imekwisha. Tumwombe Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ni Mwanasayansi, hakuachia hapo, akachukua *samples* akawapelekea watu wa maabara akawaambia pimeni *Corona*. Wakapima *Corona*; papai lina *Corona*, mbuzi ina *Corona* na watu wote wakamuunga mkono. Marais nchi jirani hata Wazungu wakamuunga mkono, kuwa kweli twenda na Rais huyu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kweli tunajivunia tunaye baba wa nchi ambaye Mwenyezi Mungu ametupatia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais akaambiya tuchukue mkopo akakataa mikopo yao. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kweli mwenyewe nasema kuwa nawapongeza wazazi wake waliomzaa na kumleta hapa duniani. Tunashukuru wametuletea kiongozi shupavu na kiongozi mwema. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais baada ya Corona kupungua akasema kuwa tufunge tena siku tatu, tumshukuru Mwenyezi Mungu. Ukipewa kumbuka kushukuru. Kwa hiyo, tukafunga tukamshukuru Mwenyezi Mungu; tunashukuru kwa hayo. Mheshimiwa Rais tunapewa kwasababu yuko karibu na Mwenyezi Mungu na sisi ametukumbatia kama kuku anavyokumbatia vifaranga vyake, tunakwenda naye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais baada ya kuona hilo akasema maendeleo lazima yaje na yaendeleee, tuendeleee tunachapa kazi lakini na vyuo pia vifunguliwe, wanafunzi wetu waendeleee kusoma; vyuo vimefunguliwa, *form six wamefungua wanaendelea kusoma*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais yuko mbioni pia kufungua shule zingine ambazo bado hazijafunguliwa, kufungua michezo, bado tuko pamoja. Mheshimiwa Rais kwa kweli amefanya mambo ya kihistora ambayo nchi jirani wote wanatamani kuwa na Mheshimiwa Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametuondoa katika hofu. Watu wote sasa hivi hawana hofu na Corona, amesema jifunze kuishi na Corona, na kweli sasa hivi tunachapa kazi. Mheshimiwa Rais unatuona tuko Bungeni, kuna wenzetu waliosema tustishe Bunge. Lakini Mheshimiwa Spika ulisema tuendelee na Bunge; je tungelisitisha hilli Bunge bajeti ingelipitishwa na nani? Miradi ya maendeleo ingefanya kazi kwa vipi? Lakini baada ya kusema hivyo tumewaona wanarudi Bungeni. (*Makof/Vigelegele*)

### **WABUNGE FULANI:** Nashangaaa!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza na wewe. Mheshimiwa Rais anasema pale palipo na Mwenyezi Mungu kuna njia, palipo na Mwenyezi Mungu hapaharibiki kitu, palipo Mwenyezi Mungu kila kitu kinawezekana. Nendeni Wakristo mkasome Zaburi ya 23 mtamuona Mwenyezi Mungu anavyotenda maajabu.

Mwenyezi Mungu ni mkubwa, naomba tuwe naye, na ninaamini Tanzania bila Corona inawezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anafanya mambo makubwa, Mheshimiwa Rais anatupenda, Mheshimiwa Rais tuwe wote. Kwa hiyo vita hivi nya Corona tushirikiane kwa pamoja, janga likitokea tushirikiane kwa pamoja tuwe kwa pamoja tutashinda hii Corona. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, najua mikoa yote inashirikiana kwa kupunguza hii Corona. Tumejifukiza, tumekula malimao, tumefanya nini, lakini hata mikaritusi, hata kashwagara vyote vimepata umuhimu. Lakini tunajua Corona itakwisha, wanamorogoro nawaambia Corona itakwisha, wananchi wote wa mikoa yote Corona itakwisha, tumtumaini Bwana kwa kila jambo hata ukiwa na tatizo Mwenyezi Mungu atakubariki na atakuvusha Corona itakwisha. Amen. (*Makof*)

### **WABUNGE FULANI:** Amina!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ambayo nimeweza kuyasema naunga mkono azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais dhidi ya Ugonjwa huu wa Corona, lakini tumtumaini Bwana kwa kila jambo Bwana atatenda. Ahsante. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Sikujua kama kumbe Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na yeye ni mchungaji, tena mchungaji hasa, siyo kama baadhi ya wachungaji walio humu Bungeni kama rafiki yangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

Rafiki yangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa akisimama humu Bungeni anaropoka sana. Mnajua Waheshimiwa Wabunge uongozi ni jambo gumu sana kwasababu unamuangalia mtu halafu jinsi unavyomjua na

yale unayoyajua kumhusu unatamani utoke na ukitoka sijui ataweka wapi uso wake kwasababu ni mchafu kabisa hastahili kuitwa mchungaji, lakini kuropoka, sijui wamezaliwaje watu.

Hawezi kujiona jinsi alivyo na mapungufu, tena mengine anajua ninajua, maana nilishamuita mara mbili tatu bwana kuna hili na hili. Kwa mwanadamu wa kawaida ukijua hilo unakuwa na aibu kidogo, lakini jinsi asivyokuwa na aibu yaani bado unaropoka tena kwa yuleyule ambaye amebeba mafurushi yako. Yaani unakaa unamuangalia unasema yaani duniani kuna watu. Lakini twendeni, bado siku nne tano, mengine yakinizidi nta-*offload* baadhi yake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Najma Giga halafu Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuunga mkono azimio la kumshukuru Rais.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze mambo kama matatu hivi; la kwanza ninataka kuona hizo kauli ambazo watu wanasema Rais amesema Corona imeisha. Tamko la Rais ambalo nimelisikia na analoendelea kuliongelea ni kwamba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuepusha na maafa yaliyotarajiwa, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuepusha na maafa yaliyotarajiwa. Kwamba huku tulikokuwa tunakwenda walikuwa wanasema kwamba huku Tanzania watu watakufa kama nzige, mpaka leo tuko jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anajua Corona ipo ndiyo maana tumefungua vyuo kwa nusunusu, shule za msingi hazijafunguliwa, anasema tunacheiki hali inavyoendelea, ikiendelea kuwa vizuri tunaendelea kufungua shule za msingi. Tunajua Corona ipo ndiyo maana tunaambiwa tuendelee kufanya yale ambayo yanastahili. Lakini ukweli ni kwamba Corona ni ugonjwa utakuwepo na utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninachowashangaa watu siku za karibuni kila mtu anayekufa *as if*sasa Corona imekuwa ndiyo imeleta kifo duniani. Wakati watu wanakufa duniani hata kabla ya Corona zaidi ya watu milioni moja duniani, leo Corona waliokufa ni asilimia 61. Watu waliokuwa wanakufa kabla ya Corona ni asilimia 35. Sasa leo mtu akifa wanasema amekufa na Corona. Kila kitu kimekuwa Corona *as if*kwamba Corona ikiisha kifo nacho kitaisha. Hawa wanakuwa wanakosea. Mungu alileta kifo kipo na kitaendelea kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namuona Rais Dkt. Magufuli tofauti na nilivyokuwa huko nyuma. Leo mtu akiniambia nimchague Rais, leo, Dkt. Magufuli amenifundisha kwamba kuchagua Rais kunatakiwa uangalie sana. Baada ya Mwalimu Nyerere kutoka na baada ya Mwinyi kuwepo, kuanzia chaguzi zillizokuwa zinakuja za Urais tulikuwa na dhana tofauti sana ya uchaguzi wa Rais.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Rais ulikuwa na mambo mwili; la kwanza unayepiga kampeni unaahidiwa kwamba unapewa nini, kama ni mfanyabiashara unaahidiwa kupewa tenda, kama ni msomi na mambo mengine ya kisiasa unaahidiwa kupewa vyeo. Kwa hiyo, tulikuwa na malengo mawili tu katika kuchagua Rais unaahidiwa cheo au unaahidiwa kupewa tenda za biashara.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ametufundisha kumbe mpate Rais anayewatumikia Watanzania walio wanyonge. Leo ukiniambia nipige kura namuangalia mtu hati yake, moyo wake wa kuvumilia Watanzania, moyo wake wa kuchunguza shida, moyo wake wa kuепusha marafiki zake, siyo kupiga kelele wala siyo kutembea na furushi la hela. Leo ukiniambia nichague Rais ntachagua mtu tofauti sana, kinyume na ilivyokuwa huko nyuma. Mheshimiwa Dkt. Magufuli ametupa somo kwamba Watanzania tunatakiwa tuijandae kutawala Watanzania kwa imani yetu sisi siyo kwa imani ya hela wala imani ya vyeo. Kwa hiyo, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa huo uongozi aliotuonesha. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, niombe Tanzania tusiige mambo ya kulipiza visasi. Tusirudishe madereva wa nchi zingine, tuiswanyanyase watu wa nchi zingine, Mungu ametusaidia sisi hawa wanaoturudisha huku nyuma watakuja tu hawana mahali pa kwenda. Tusilipize visasi, tuendelee kuweka uongozi, diplomasia iwepo ili watu wetu na Mungu aendelee kutukinga, kwasababu Mungu anasema usilipize kisasi. Omba tuwaombee wale ambao wanatufanya fujo watarudi kwenye nafasi yetu.

Mheshimiwa Spika, na wewe nikushukuru. Unajua haya mambo kwa kweli bila kuwa na wewe misimamo hapo, bila kuwa na msimamo thabitii vifo vilivyotokea hapa ghafla ghafla humu ndani watu walikuwa wanakuja, hata mimi nilikuwa nafika hapa nilikuwa naona watu wana *sanitizers* zile makopo makubwamakubwa anapiga *sanitizer* mpaka jasho linatoka. Hali ilikuwa ngumu, bila kuwepo wewe hapo usimame ututulize humu ndani tungekimbia. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, bila kuwepo hapo ututulize humu ndani tungekimbia, hata kama Rais angesema tuendelee watu wangekimbia. Tunakushukuru wewe sana kwa misimamo yako, hiyo misimamo imetufanya tumekuwa humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unajua kuna jambo lingine naita la kijinga, la kijinga kabisa. Hivi kwa mfano, nitoe mfano, hapa Dodoma tulipo kabla ya Corona *General Hospital* ilikuwa imejaa watu, uende hapa Makole pamejaa, Benjamin Mkapa pamejaa, *DCMC* pamejaa, vituo vyya afya vyote vimejaa, hospitali hapa watu wamejaa. Sasa leo uambie hii Dodoma *lockdown*, unajua maana yake nini? *Lockdown* maana yake watu wote wakae ndani; anayeumwa kichwa apige simu *ambulance* iende, anayeumwa tumbo apige simu *ambulance* iende, anayetaka kujifungua afuatwe na *ambulance* hivi inakuaje halafu picha zinaonesha sasa Dodoma yote imejaa Corona. Mambo ya kijinga kabisa haya; unafungia watu halafu unatengeneza mpango mgonjwa

yeote wewe ndio umfate. Tuna *ambulance* ngapi, tuna watu wangapi wanaenda hospitali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ana akili sana kwa kweli. Ametufanya kwamba kumbe sasa tunatakiwa kuwa na uwezo wetu wa kufikiri, siyo uwezo wa kufikiri kwa ajili ya migongo ya watu. Leo nilikuwa naona watu wengine humu ndani watu wachungaji kabisa wengine makatekista kabisa nawaona humu ndani, nimeona watu ndani hata Mheshimiwa Lema ni mtu wa dini sana lakini utaona woga wake umekuwa mkubwa, watu wanafuata mambo ya nje. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, Unajua nchi hii ina mambo ya ajabu sana. Ndiyo maana Mungu alivyotuumba Taifa la Tanzania halijawahi kupata Rais aliyetoka nje ambaye Wazungu wanasema huyo awe Rais anakuwa. Sisi hatujawahi kufanya, sisi tunapata Rais kutokana na watu wetu waliozaliwa humu ndani. Sasa hivyo vyama vinavyopanga Rais atoke nje aagizwe aje kutawala Tanzania hiyo haipo, ni ndoto, hiyo ni ndoto kwa Watanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ametuonesha nini cha kufanya Watanzania. Amekuwa mvumilivu sana. Ningeshangaa usingeleta hili azimio ningejuliza hapa kuna nini. Sasa na wewe kumbe unaona mbali, unatengeneza miyanda mikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kusema kweli na wewe inatakiwa tukulinde kama mboni, hakuna haja ya kukuachia, wewe na Rais tuwalinde kama mboni muwepo kwenye Taifa hili muongoze watu. Vinginevyo tutakuwa tunaleta walaji tu. Na leo tukatae watu wanaotembea na mifuko ya hela kununua Urais, leo tuwakatae watu wanaotafuta Uspika kwa nguvu, haipo hiyo, tuwatafute watu wenye imani ambaa wanaweza kufaya kazi hii. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere kwa mchango wako. Mheshimiwa Najma Giga, utafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye azimio hili muhimu sana la kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwenye mapambano dhidi ya hili janga kubwa la Corona au kwa lugha ya kitaalam *COVID-19*.

Mheshimiwa Spika, niungane mkono na wenzangu wote waliotangulia kutoa pongezi zao kwasababu tofauti lakini pia na namna ambavyo Mheshimiwa Mmasi alivyoelezea yote katika taarifa hii ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kuhusiana na suala hili.

Naomba tu niwaeleweshe au niwafahamishe Watanzania yale ambayo nimeyaona binafsi yaliyosababisha Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni jemedari wa Taifa letu kuweza kulisimamia Taifa letu la Tanzania kwenye mapambano dhidi ya hili Corona. Sababu hizo zimeweza kutajwa pengine na Waheshimiwa wengine hapa lakini nitazitaja kwa namna tofauti au ntaeleza kwa namna tofauti.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni ucha Mungu wa kweli, limezungumzwa hapa. Na ili umjue mtu ni mcha mungu wa kweli anakuwa na sifa za ziada tatu; kwanza anakuwa ni mwenye kujiamini, anakuwa *very confident*, lakini la pili anakuwa ni jasiri, na la tatu anakuwa ni mtu mwenye msimamo asiyeyumba. Hizo ni sifa za mcha Mungu wa kweli. (*Makofivigelegele*)

Mheshimiwa Spika, sasa mbali na hizo sifa za kuwa mcha Mungu wa kweli ambapo baadaye ntataja kwa nini sasa ameweza kufanikiwa zaidi, la pili ni uzalendo kwa Taifa la Tanzania. Hilo jamani msilione dogo; uzalendo kwa nchi yake mtu anaweza kujitolea kwa namna yoyote na nguvu zozote. Kwa hiyo, hayo mawili ndiyo nimeyaona binafsi kwamba yamemsababisha Mheshimiwa Rais wetu kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, na lingine ambalo ni la ziada, Mheshimiwa Kitwanga juzi alizungumza neno hapa akasema kuna watu wenyе akili kubwa na kuna watu wenyе akili ndogo lakini unapokuwa mcha Mungu wa kweli unakuwa *genius by nature*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais wetu ana akili za ziada kutohana na ucha Mungu wake, hilo lazima tulikubali. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa nini kimetokea baada ya Rais wetu huyu ambaye ni jemedari wetu ambaye anayafanya mengi kwa Taifa hili, ameweza vipi kusimamia janga hili la Corona, tumeweza kuona mambo matatu makubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza uchumi wa Tanzania haujayumba kama wenzetu wengine, yamesemwa kwa mtazamo tofauti na naelezea kwa uwezo wangu ambao nimeweza kuelewa. Uchumi haukuyumba na kwa taarifa tu wale ambao hawajui Tanzania ni mionganoni mwa nchi kumi zenye uchumi unaokuwa vizuri katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, hii naamini bado kwa uongozi thabiti wa jemedari huyu tulienyane ambaye watu wengi wanamtamani awe Rais wao katika ulimwengu huu, sisi Watanzania tunaye. Kwa hiyo, hili ni moja la uchumi. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ukiwaweka wananchi wako katika Taifa lako bila taharuki jambo baya linapotokea au janga, ni sifa ya pekee ya kiongozi. Amekuwa thabiti, amesimama imara hakuyumba, sifa zote za ucha Mungu nimeshazitoa, na sisi tumekuwa nyuma yake ukiwemo na wewe mwenyewe umeweza kusimamia Bunge hili bila kuyumba na sisi tuko nyuma yako tumekaa na wewe tuliokuwa tumeamini hayo ambayo Mheshimiwa Rais ameaminu na wewe ukawa umesimamia na sisi kuendelea kufanya kazi yetu, bajeti tuepitisha mambo yamekwenda Taifa linaendelea. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kabla sijamaliza la mwisho ambalo kubwa lao nitalisema mwisho wakati nahitimisha ni kwamba tunaendelea katika mapambano

dhidi ya Corona tukiwa bado tunashika mshiko uleule aliotuambia Mheshimiwa Rais, tunaendelea kumuomba Mungu tusiache kwasababu hata janga likiisha kumuomba Mungu kuko palepale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, juzi nilisema kuna mambo mawili katika dunia; kuna sheria za duniani ambazo zinatungwa na sisi Wabunge katika mataifa mbalimbali pia wanafanya hivyo, lakini kuna sheria za Mwenyezi Mungu kuitia vitabu vyetu vitukufu au vitakatifu ambavyo vinatutaka tuendelee kuwa na imani ya Mungu pale ambapo matatizo yanayotokea katika nchi yetu au katika Taifa letu tuweze kusimama naye ili atusaidie. Kwa hiyo, yote haya tunazunguka palepale lakini bado tunaendelea kusema kwamba kiongozi huyu ambaye tumempata katikaT hili la Tanzania ni kiongozi mwenye sifa za pekee.

Mheshimiwa Spika, ucha Mungu ni jambo kubwa kuliko kitu chochote duniani kwasababu mwisho wa siku tunakwenda kujibu mbele ya Mwenyezi Mungu ambaye yeye ndio anataka tuwe wacha Mungu. Mbali na mambo ya duniani tunayoyafanya katika kusimamia mambo yetu lakini pia ucha Mungu unachangia asilimia kubwa ya maisha yetu katika dunia hii.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Watanzania wote kwa hiyo, niseme tu nawaheshimu sana na Wabunge wote mliomo humu tuendelee kumuombea dua Mheshimiwa Rais wetu pamoja na viongozi wote wakuu wa mihimili ukiwemo wewe Mheshimiwa Spika ili imani yenu juu ya Watanzania wenzetu pamoja na ucha Mungu wenu, pamoja na mapenzi yenu, pamoja na uzalendo wenu visiishe ili muendelee na kuendelea kutusaidia Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nasema tu kwamba wale ambao wanahisi kwamba Rais huyu hatoshi waone aibu. Hilo ndilo nilisema la mwisho; kwasababu mataifa yote duniani yanaiga sasa kile alichokifanya kwa Tanzania kuhusiana na hii Corona, kwa hiyo, wao wanakuja

kuiga mtu ambaye sisi tusione thamani yake tutakuwa ni watu wa ajabu sana kabisa katika Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nakushukuru kwa hilo lakini kwa niaba pia ya Zanzibar nzima niseme kwamba Mheshimiwa Rais tunampongeza sana kulisimamia janga hili na ninaamini kwa imani yake hiyo aliyonayo kwa Watanzania wote na sisi tulio nyuma yake ukiwemo na wewe na viongozi wote tulio humu basi tuendelee kumuunga mkono ili tusaidiane naye.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kama nilivyo sema katika mchango wangu wa mwisho, hii *Corona* itaondoka leo kabla ya kesho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na nilaunga mkono Azimio hili mia kwa mia. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Giga. Nakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri sote tunafahamu kwamba, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe, amepata tatizo. Kwa hiyo, yuko kwenye Kituo cha Afya ambacho kinaitwa Ntyuka na wengine wanaita *DCMC*. Nimepata nafasi ya kumtembelea leo asubuhi na nikaongea naye. Kwa ujumla hayuko kwenye hali mbaya, yuko kwenye hali nzuri tu, alikuwa akipata *breakfast* wakati nimefika pale. (*Makof*)

Amepata tatizo la mguu wa kulia, amepata kitu kama *dislocation* hivi, siyo kuvunjika kwa mfupa mkubwa huu. Unajua kwenye mguu kuna mfupa mkubwa, halafu kuna hivi mishipa mingine kwa nyuma hapa. Sasa huu wa nyuma ndiyo umeleta taabu huku mwanzo. Ni kama mtu ambaye hata unaweza ukakanyaga vibaya hivi halafu ule mshipa wa nyuma ukafyatuka, kitu cha namna hiyo, lakini siyo kuvunjika kwa mfupa, hapana. Ni huu mshipa wa nyuma. Tunao

Madaktari hapa, wao wanajua vizuri, sijui mnaita *ligament*, sijui mnaita nini?

Kwa hiyo, yupo, Madaktari wanamwangalia, wameniambia kwamba watatupatia ushauri wao. Pia wameniambia *surgeon* wao anaweza kabisa kufanya hiyo kazi, lakini wakasema watatupa ushauri wao badaye kidogo. Sasa kwa kuwa jambo lenyewe lina hadithi nyingi la jinsi liliyyotokea, maana yake inasemekana mpaka saa sita usiku jana alikuwa mahali pengine, kwa hiyo, lina hadithi nyingi. Inaniwia ugumu kusema chochote kwa hatua hii, lakini niseme tu msichukulie kama hivyo mnavyosikiasikia, lakini watakaosema halisi ni vyombo nya ulinzi na usalama. (*Makof!*)

Nawaomba basi vyombo nya ulinzi na usalama watoke mapema iwezekanavyo, waeleze kilitokea nini kadiri wanavyojua, isiwe ni kazi yangu. Kwa sababu ni kazi zaidi ya vyombo nya ulinzi na usalama. Kwa sababu wanavyozidi kuchelewa hadithi zinakuwa nyingi. Basi wanachokjua waseme, kama kuna *part* ya upelelezi, basi wabakize hiyo *party* ya upelelezi waifanyie kazi. Kwa hiyo, naamini kesho jioni saa hizi tutakuwa kiasi fulani na cha kusema na kuambiana hapa kuhusu jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie kwa mara nyingine, Dodoma ni salama kabisa, kabisa, kabisa. Mmekaa hapa toka tumeanza mwezi wa Nne mwanzoni, mpaka sasa tuko mwezi wa Sita hakuna aliye poteza sikio, hakuna aliye poteza jicho, hakuna aliye chomoka mkono, hakuna aliye katika kidole, Dodoma ni salama ndugu zangu. (*Makof!*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mmasi kwa kuleta Azimio hili. Umefanya kazi nzuri, nakupongeza sana dada yangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la *Corona* liliyyokuja limetusaidia kujua aina za viongozi waliopo duniani. Wana

zuoni wanasema, unapopata janga ndiyo wakati ambapo kama kiongozi unatakiwa uwe mtulivu sana. Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli baada ya janga hili alithibitisha alivyo mtulivu kwenye kupambana na jambo hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Rais Magufuli ni Rais wa Watanzania, aliyetokana na Watanzania wenyewe, kwa hiyo basi, anawaelewa Watanzania kwa namna ya dini zetu, makabila yetu na tamaduni zetu. Mheshimiwa Rais akaamua, sasa anapambana na ugonjwa huu namna gani? Akaamua kupambana na ugonjwa huu alivyoona yeye, Mungu alivyomjalia karama za kuona mbali, Mungu alivyomjalia maono yake na aka-stick to it. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, halikuwa jambo rahisi hata kidogo. Katika mazingira ambayo dunia yote ime-*panic*, dunia yote kuna tataruki, unaweza ukaona Rais utulivu wake ulipitiliza, alitulia sana. Alitulia kwa sababu ya Mungu kumjalia maono ya kuona mbali na akaamua kupambana na ugonjwa huu kwa namna na kwa jinsi alivyo yeye na Watanzania wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nami kwa kweli, namwomba Mungu amjalie sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. Ni mara chache sana, kama hukujaliwa karama za uongozi; viongozi wote waliofanikiwa duniani ni wale ambao wanaona ambako wengine wote hawaoni. Wakati fulani watu unaweza wakaanza kukulaumu, mbona huyu haoni? Kumbe naye akikaa peke yake anawalaumu, mbona wenzangu hawaoni? Mbona *route* hii ndiyo sawasawa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwanza alikuwa anatushangaa Watanzania; tulipata tataruki, tulipata hofu, lakini yeye alitulia, akawa anaona anakoenda. Kwa kweli, ametufikisha alikokuwa anataka twende. Wazungu wanasema, Rais kwenye jambo hili amekwenda *against all odds*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, *predictions* za WHO kwa Tanzania hazikuwa sawasawa na *predictions* za watu wote na

wanasayansi kwa Tanzania hazikuwa sawasawa. Ni kwa sababu, Mungu alitujalia kiongozi anayeweza kuona mbali na mwenye maono makubwa sana kwa kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge aliona wapi? Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli cha kwanza alidhibiti hofu. Ugonjwa huu hata waliopata matatizo kwa kweli, wengi ilikuwa ni hofu. Yeye ndio wakati ambapo akazidi kututhibitishia tusiogope, huu ni ugonjwa kama ugonjwa mwininge, tuchukue tahadhari. Wako watu walisema tu-*lock down*, kwa sababu yeye alikuwa anajua tunakoenda alikataa ku-*lock down*. Alikataa kwa sababu, hivi ange-*lock down* mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa Watanzania wetu na uchumi wetu ange-*lock down* tungeenda kwenye *Corona* ya umasikini. Huko amekataa kwenda, ndiyo maana tukaendelea kufanya kazi, ndiyo maana bajeti yetu ya 2019/2020 ikaendelea kutekelezwa, ndiyo maana Vituo vya Afya vikaendelea kujengwa, barabara zimeendelea kujengwa, ndege zimeendelea kununuliwa, reli imeendelea kujengwa na *Stiegler's* imeendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, maana tunge-*lock down* watu wangemwuliza, kama ume-*lock down* mbona watu wanaenda kujenga reli? Maana yake unge-*lock down* miradi yetu yote ingesimama na maendeleo yetu yangesimama. Jambo hili Mheshimiwa Rais alilikataa kwa nguvu zake zote. Kwa kweli, kwa hili Mheshimiwa Rais Mungu ambariki sana, ametusaidia sana Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli, ugonjwa bado upo, lakini unapungua, tunaendelea kuchukua tahadhari. Ilikuwa lazima maisha yaendelee. Leo hii ukisoma Marekani kabla ya maandamano haya kulikuwa kuna *pressure* kubwa kwamba fungua uchumi na hawa ndio watu ambao chumi zao zina *resilience*, zinaweza zika-*absorb shocks*. Uchumi namba moja duniani wakaanza kumwambia Rais wao fungua uchumi, kwa sababu hali ilikuwa inaenda kuwa mbaya zaidi. Sasa je, kwa sisi ambao uchumi wetu hauna *resilience*, hatuwezi tuka-

*absorb shocks!* Kuna watu ili ale, lazima afanye kazi leo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasema nakupongeza Mheshimiwa mama Mmasi kwa kuleta Azimio hili, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli anastahili kupongezwa sana kwa jinsi ambavyo alipambana na ugonjwa wa *Corona*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo duniani nilikuwa nasikiliza, kuna watu wanatamani kuja kujifunza ni kwa sababu Mheshimiwa Rais alliona mbali. Kwa kweli, moja ya jambo kubwa; na hii ndiyo sifa ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. Kama mmeangalia Waheshimiwa Wabunge, maamuzi yake ni *against the tradition*. Haamui kwa sababu wengine wote wanaamua namna hii, hapana. Anaamua kwa *conviction* yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo hii, sijui kama mnakumbuka vizuri, wako watu wanamlamu Mheshimiwa Rais kununua ndege kwa *cash*. Ukiiliangalia haraka haraka unaweza ukalaamu, lakini mnajua ame-save nini? Kwa kununua kwa *cash* amekimbia kulipa *interests* ambazo ni kubwa sana. Mashirika yote yanapata matatizo kwenye *interest* kwa sababu unanunua kwa dola; ndege zako unatoza shilingi, inabidi utafute mashillingi ukalipe na *on top of it* ulipe na *interest*. Huyu ni Rais anayeona mbali sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli aliamua *against the whole world* kwamba lazima tutekeleze mradi wa umeme wa Stiegler's. Haikuwa *decision* rahisi, lakini ye ye mwenyewe akakaa akaamua tukasema tutekeleze. Leo wote, hata waliokuwa wanapinga wanaanza kuona mwanga mwishoni, lakini kwa sababu, Mungu alimjalia kipaji cha kuona mbali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliamua hapa tujenge reli kwa pesa zetu wenyewe, hela ndogo hizi za kodi. Ni kweli, tumejfunga mkanda, lakini hakuna Taifa limeendelea bila kujifunga mkanda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa alivyopambana na ugonjwa huu wa *Covid 19*. Mpaka Mheshimiwa Rais ananikumbusha Jack Welsh, alikuwa *the best CEO* wa *GE* kwa miaka 20. Siku zote anasema sifa kubwa za kiongozi ni tatu. Sifa ya kwanza, ni lazima awe *Chief Meaning Officer* aweze kuwaambia kwa nini nawapeleka huko? Huko ninakowapeleka kuna nini? Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ame-*demonstrate* hilo. Pia lazima *a leader* awe *chief blomer*; ye ye mwenyewe aongoze kwa matendo. Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ameongoza kwa matendo kwenye mambo yote ambayo ameyaamua kama nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kubwa zaidi, lazima Rais awe na *generosity gene*. Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli Mungu amemjalia, ana *generosity gene*, anajali wanyonge. Maamuzi yake yote ukiyaangalia, haangalii kundi dogo, anaamua kwa kuangalia kundi kubwa saidi lita-*benefit* namna gani. Hamna namna nyingine ya kulielezea, huu ni uzalendo mkubwa sana kwa kiongozi Mungu aliyetupatia. Nami ninamwamini kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa namna ya alivytuongoza kwenye ugonjwa huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, kama walivyosema wengine, name nakupongeza sana wewe. Spika usingekuwa na msimamo baada ya watu kupata vifo hapa ndani, ungetuongoza kufunga Bunge, lakini wewe na Mheshimiwa Rais mlikataa. Kwa wale ambao tumekaa hapa muda mrefu, mnakumbuka, huwa vifo vinatokea, maana sisi ni binadamu. Tuwaombee Mungu wale waliotangulia mbele ya haki, lakini mmetuongoza vizuri, tumeweza kupambana, tumeweza kuvuka, lakini yote haya tumefanikiwa kwa sababu tulimweka Mungu mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ile Kamati iliyokuwa inaongozwa na Waziri Mkuu, Rais mwenyewe, siku zote mlitukumbusha umuhimu wa kumwomba Mungu na Mungu amejibu sala zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, nami nampongeza sana tena aliyeleta azimio hili, naliunga mkono na kwa kweli, tungemaliza Bunge lako hili bila kumpongeza Rais kwa kitendo cha kishujaa, cha kizalendo, cha kusimamia ugonjwa huu kwa namna alivyoona kwa maono yake, leo hii tungekuwa tumebaranganyika, lakini Mungu amemsaidia, kampa karama za kuona mbali.

Mheshimiwa Rais tunakushukuru, unakotupeleka ni kwenyewe na nina hakika unaposema unataka Taifa hili liende kuwa la uchumi wa katiba, unamaanisha na nina hakika utatufikisha huko.

Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki sana Mheshimiwa Rais, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba kwa mchango wako huo mzuri sana. Sasa tumsikie Mheshimiwa Margaret Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na baada yake Mheshimiwa Peter Lijualikali ajiandae.

Mheshimiwa Mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mezani ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupambana na tatizo lililotupata la *Corona*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhaitangu nilipoingia Bungeni mwaka 2015 mpaka sasa hivi, amenipa uhai ambao namshukuru sana. Pia nawashukuru sana wananchi wa Urambo ambao wamenipa ushirikiano wa hali ya juu na ninaamini kabisa wataendelea kunipa ushirikiano huo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Urambo, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha tatizo kubwa lilitotukumba duniani la Corona.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu katika kupambana na suala hili alifanya kazi kubwa sana ya kuunganisha Serikali yake ya Awamu ya Tano akiwemo Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote katika Serikali yake amba walifanya kazi kama timu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia aliunda Kamati Maalum ya kushughulikia suala hili, lakini wakati huo, pamoja na kuunda Kamati jambo kubwa alilofanya ni kumtegemea Mungu. Ninaamini kabisa aliongozwa pia na neno la Mungu likiwemo Zaburi ya 116 mstari wa 1 - 8 amba unasema hivi, naomba kunukuu kwamba, "Nampenda Bwana kwa kuwa anasikiliza sauti ya dua zangu."

Mheshimiwa Spika, kweli imeonesha wazi kabisa Mheshimiwa Rais Mungu amesikiliza dua zake na kweli tumepitia wakati huu kwa kweli na hatukupata madhara makubwa kama walivyopata nchi nyingine. Mwenyezi Mungu ambariki sana Rais wetu kwa kumwamini Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunda kamati ya kushughulikia janga hili alituambia tusali kwa siku tatu, tumuombe Mungu Misikitini, Makansani na nyumbani; na kweli tulimwomba Mungu kwa siku tatu akiamini kwamba anayemtegemea Bwana hawezi kuanguka. Pia akatupa maelekezo ya kufuata wakati huo huo akahimiza tufanye kazi na wakati huohuo akasema tuondoe hofu, tunamshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yote haya yaliyotendeka kipindi hiki kwa kuongozwa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi kama kiongozi na nina amini viongozi wengine pia tumejifunza yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, kwanza kiongozi lazima ajiamini lakini pia kiongozi lazima awe anayethubutu na pia ametuonesha kwamba kiongozi lazima awe jasiri, halafu pia kufanya maamuzi kwa wakati, kufanya kazi kwa bidii na lakini wakati huohuo ametufundisha kwamba kuna umuhimu wa kufanya utafiti kama aliofanya yeye. Pia ametusaidia sisi kwamba lazima Watanzania tuwe na uzalendo ambao ameuonesha sana katika kushughulikia suala lote hili la corona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais wetu kama walivyotangulia kusema wenzetu, amekuwa mfano mkubwa sana nchini kwetu sisi lakini pia amekuwa mfano mkubwa sana duniani kwa kuwa na misimamo. Kwa kweli anastahili sifa na ndiyo maana naunga mkono kwa dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Urambo kwamba anastahili kuungwa mkono, kusifiwa na kupongezwa kwa sababu ametuonesha kabisa kwamba kiongozi lazima awe kama alivyokuwa yeye, kuwa jasiri, misimamo na kutuongoza. Tumeondoa hofu, tumefanya kazi kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Rais na Serikali yake kwa ujumla narudi kwako wewe. Ulisema Bunge linaendelea, ukaungana na Serikali kwa ujumla mkasema Bunge linaendelea na kweli ukasimamia, Tukawa tumegawanywa katika vyumba mbalimbali kwamba hakuna lisilowezekana pale mtu anapokuwa na nia. Asante sana tunakushukuru, endelea na kazi hiyo hiyo Mungu akubariki na nadhani huko mbele njia ni nyeupe kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kwa niaba ya wenzangu Waheshimiwa Wabunge hasa wanawake ndani ya Umoja wetu wa Wanawake wa Bunge hapa Bungeni tunakushukuru kwa jinsi ambavyo umekuwa ukifanya kazi karibu na sisi,

tunakushukuru sana. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wakiume ambao mmekuwa mkituunga sana mkono sisi wa Umoja wa Wanawake (*TWPG*), kwa hiyo tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nitaje hapa; sisi kama wanawake kwa kupitia *TWPG* tumekuwa tukiomba kwamba wanawake wanaoweza wapewe nafasi, kweli sio kweli? Na tumeona Mheshimiwa Ummy amepewa nafasi ya Uwaziri wa Afya, ameitendea haki tumpigie makofi. Kwa hiyo, chini ya uongozi wa Jemedari wetu Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Ummy amefuata maelekezo ya Rais na kamati iliyoundwa ameonesha kweli wanawake wakipewa kazi wanaweza. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Ummy kwa vile ambavyo ameitendea haki nafasi aliyopewa kwa kufuata miongozo yote aliyokuwa anapewa na Mheshimiwa Rais. (*Makofi/ vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa nafikiria kwamba baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoshughulikia suala la corona lazima nimshukuru pia Rais kwa jinsi ambavyo ametusaidia Wilaya ya Urambo kupata maendeleo katika kipindi chake cha awamu ya tano. Ametuahidi maji kutoka Lake Victoria tutapata, ametusaidia barabara za lami, tumeposta kituo cha kupoozea umeme, umeme wa *REA*, kupata kupata Kituo cha *VETA* na mambo mengine ya elimu, ya kupata mabweni, madarasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kupitia Serikali yake ya Awamu ya Tano kwa mambo mengi ambayo tulimuomba sisi kama wananchi wa Urambo na akatutendea. Kwa hiyo tunaamini kwamba ataendelea kutawala na tutapata mengi zaidi, tutaongezewa yote ambayo tumeomba, vituo vyta afya na mengine mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba kwa niaba ya wananchi wa Urambo nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, na kwa msingi huo

naunga mkono hoja iliyopo mezani ya kuunga mkono Azimio linalompongeza Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyosimamia na sasa tunajivuna tuna Rais anayejiamini na mwenye maamuzi; Magufuli Oyeee. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margareth Sitta tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Lijualikali.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kuniweka katika list ya watu ambao wanaunga mkono Azimio hili la kumpongeza Rais wetu kwa kazi nzuri anazozifanya hususan hii ya kusaidia kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mungu kwa yote mema, na kati ya mambo mema ambayo ameipatia Tanzania ni kutupatia Rais tunayemtegemea mwenye uwezo, umakini na umaarufu wa kuifanya nchi hii kuwa ya pekee. Na kwa hivyo nampongeza sana kwa kuweza kutumia vipaji alivyopewa na Mwenyezi Mungu; unaweza ukapewa vipaji vikubwa na vizuri, mimi nimepewa sauti nzuri lakini naweza kukaa kimya nisitumie kipaji hicho.

Mheshimiwa Spika, sasa Rais vipaji alivyopewa kwa kweli kavitungia vizuri, ninampongeza sana na hii imemfanya kutumia uwezo wake unaotokana na vipaji hivyo kuweza kukabiliana na ugonjwa huu hatari ambao hauna dawa ya kinga wala kutibu. Kwa hiyo tunamshukuru sana kuongoza taifa letu kwa umahiri, uwezo, upendo na umakini mkubwa na matatizo kama hayo bila vipaji hivyo si rahisi sana. Rais ameweza jitihada katika kujenga Hospitali za Taifa, Mkoa, Wilaya mpaka zahanati za Vijiji na Vituo vy'a Afya vy'a Kata.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hivyo, kuwepo na hospitali hizi za ngazi mbalimbali nina hakika zimesaidia sana katika kukabiliana na ugonjwa huu. Jitihada hizi hazikujua kwamba corona itatufikia lakini amejua kwamba wananchi

wanahitaji hospitali kwaajili ya kinga, tiba na mambo yote ya afya. Nampongeza sana Rais kuweza kufanya hayo na ndiyo maana leo Tanzania imekuwa nchi ya pekee. Linganisha Tanzania na Marekani, linganisha Tanzania na Uchina lakini sisi katika muda mfupi kwa Rais huyu kuwa imara na kutoa maelekezo ambayo yanakubalika na kuwa na wasaidizi wanaokubali, leo tumefika hapa corona haijaondoka lakini *speed* ya kuongeza corona na watu kuugua imepungua. Kwakweli tumshukuru Mungu kwa sababu na Rais huyu anamwamini Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa watu ambao wamefanya kazi na Mheshimiwa Rais wetu Magufuli, nimekuwa naye Uwaziri miaka 20, kila anapopewa kazi kwenye sekta amefanya kwa bidii na hiyo ndiyo imetufanya sisi tukamchagua kuwa Rais wetu. Umahiri huu sasa umetutoa kwenye huu ugonjwa na mimi naamini kama tutakubali masharti, maelekezo yake pamoja na kumuomba Mwenyezi Mungu aliyetupa Rais huyu, mimi nina hakika tutaondokana na corona. Tulikuwa na hofu kubwa Wahanang' walikuwa na hofu kubwa sana lakini sasa hofu imepungua na watu wameanza kutekeleza masharti waliyopewa na hiyo ndiyo itatufanya tutokomeze ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kuwa na kujiamini Rais ni nchi kuaminika vilevile. Fikiria maamuzi yake yalivyosaidia kuendeleza uchumi, shughuli za kijamii na mambo mengine ya binafsi alivyosema kwamba jamani tusijifungie ndani na wala tusifunge nchi yetu, mipaka isifungwe uchumi umeendelea, shughuli za kijamii zimeendelea, watu wa Hanang' wanajenga shule, zahanati na vituo vyaya afya. Hayo yote hayajaachwa na kama tusingekuwa na maelekezo hayo watu wangejifungia ndani, unawezaje kukaa ndani ule jamani, inawezekana? Haiwezekani kwa sababu kwanza vyakula vyenyewe ama uende shambani ama sokoni, maelekezo yake katoa hofu na watu wakaendelea kufanya yote yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, maelekezo hayo yaliyoimarisha uchumi wetu hayajaturudisha nyuma, imekuwa ni hekima

kwa Watanzania kufanya kazi kwa bidii huku wakifuata masharti tuliyopewa ya kuweza kunawa. Ukienda Tanzania leo kuna ndoo nchi nzima, ukienda kwenye taasisi zote kuna ndoo za kunawia na dawa ya kuondoa virusi via corona. Sasa si kawaida kwa watu kuwa watiifu hivi, maana yake wanamuamini Rais wao na anastahili kupongezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa pamoja na Rais, niwapongeze wasaidizi wake, Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Afya pamoja na wale ambao wamewekwa kwenye kamati maalum na wataalam wote wa afya. Tumeweza kufikia hapo Rais ameoaa maelekezo, anayasimamia lakini kuna wale wanaotekeleza wanastahili nao kupongezwa na pongezi hizi zinampa pongezi Rais kwa sababu alioyaweka kwenye kamati lazima ni watu wenye uwezo na amemuacha Waziri pale akijua kwamba anafanya kazi kubwa. Mheshimiwa Ummy tunakupongeza kwa sababu na wewe umetufanya tumuone Rais maelekezo yake ni mazuri, usingeyatekeleza vizuri tusingewenza kuona kazi nzuri ambayo ameifanya Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa ni kutenga hospitali maalum, tungewachanganya wagonjwa wa corona wangeambukiza watu wengine jamani, wale waliolala wasioweza kujisogezza. Sasa kuwa na hospitali maalum ni moja ya namna ya kupunguza ugonjwa huo, unapotoka hujamuambukiza mtu, unapotoka unarudi nyumbani na wala huwezi kuwaambukiza wa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kufunga shule imeleta *off course* upungufu wa elimu lakini umewafanya watoto wasiugue. Amefunga lakini muda ulipofika corona inavyokwenda chini kwa maambukizi amefungua vyuo na *form six* waende kufanya mitihani. Yote haya yanaonesha Rais anapofanya kazi kwa maamuzi jamani mazuri na umakini wake unaonekana hapo.

Mheshimiwa Spika, kutukumbusha nafasi ya Mwenyezi Mungu si jambo dogo; Mheshimiwa Rais anasali, mimi nimekuwa nikisali naye St. Peters na kila saa 12 anaanza. Siku

moja tukawa tunaongea pale akaniambia mama Nagu kabla ya mambo mengine anza na Mungu ili mambo yaende vizuri; na hili la corona limeenda vizuri. Ninampongeza tuendelee kumuabudu na kumuona Mwenyezi Mungu kwamba ana uwezo, kuwaachia uwezo wengine kuleta dawa mbadala nayo ni kipaji jamani; wengine wangesema tutulie kwenye hizi dawa za kitaalam. Kati ya madawa haya lazima kuna yanayosaidia hata mimi nina hakika tunakunywa ile chai ya tangawizi ambayo inaondoa virusi kwenye nafasi hii ya kumeza. Kwa hiyo huwezi kulinyamazia kitu kimoja ambacho kwanza hakuna dawa ya tiba/kinga sasa wenye uwezo wasieze kuonesha uwezo wao ila tusumie.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli mimi nipo na fahari kubwa na Rais Magufuli aliyefanya kazi na mimi, kwanza nimefurahi amekuwa Rais na ninaomba kuunga mkono hoja iliyoletwala na Mheshimiwa Esther Mmasi na nampongeza sana yeeye, amethubutu kufanya hivyo.

Ninaomba kupitisha Azimio hili la kumpongeza Rais wetu John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri inayofanyika na kuionesha Tanzania ni nchi tofauti iliyona Rais imara mwenye uwezo, hekima, umakini na ndiyo maana nchi yetu inazidi kuonekana. Tumuombe Mungu tuutokomeze ugonjwa huu ndani ya nchi yetu kabla ya nchi zingine ili waendelee kufuata mfano wa mambo mazuri aliyoayaamua Rais wetu na Mungu ampe afya njema aendelee kuongoza nchi hii kwa namna ambavyo Mwenyezi Mungu amemuelekeza na kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Hanang' ninampongeza, ninampenda na naomba Mungu tuendelee nae na uchaguzi huu usiwe na mtu mwengine wa bugudha aendelee bila kupingwa na ili tuweze kuendelea na jitihada zake kadri inavyowezekana. Ahsante sana, Mungu akubariki wewe na tumekupongeza jana na pongezi hizo uzipokee na utusaidie Bunge hili liendelee na wewe muda utakaokuja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Ahsanteni kwa makofi jamani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Peter Lijualikali atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian, Mbunge wa Kiteto.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, leo tuna Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi nzuri aliyoifanya katika pambano la corona. Sisi wengine tulishi kwa imani sana baada ya kukataa maagizo ya hovskyo, tukaishi kwa imani ya kumtegemea Mungu kama ambavyo Mheshimiwa Rais Magufuli alituongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi na familia yangu wazima, tupo salama kabisa, ingawa kuna watu walikuwa wanasesemasema kwamba nimeoa kwako ingawa huu ni uongo kabisa. Mimi na familia yangu tupo salama kabisa, tunamshukuru Mungu kabisa katika hili.

Mheshimiwa Spika, umezungumza kitu ambacho kimetokea leo cha Mheshimiwa Mbewe na kwa sababu tunataka kusema ukweli na ukweli utatuweka huru kama taifa, tutasema ukweli. Tupo katika corona kwa hiyo tunajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chama cha CHADEMA kikiongozwa na Mheshimiwa Mbewe kimekuwa kikijifanya kinafanya vitu vyake kitaalam kwa ajili ya kupambana na corona, utaona wanafanya vikao sijui kwenye *computer sijui* kwenye nini, hawataki sijui wawe wanagusana na nini kwa sababu ya corona. Lakini chama hiki hiki na mambo hayahaya jana limetokea jambo; na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Msigwa kuna wakati huwa anaongea ukweli sana. Mheshimiwa Msigwa anasema jana mpaka saa tatu alikuwa kwa Mwenyekiti, baadaye Mwenyekiti akatoka

wakaenda, ukweli unafahamika walikuwa wanakunywa pombe; huu ni ukweli walikwenda kulewa. (*Makofi/Vigelegele*)

**WABUNGE FULANI:** Rudia rudia...

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Walikwenda kulewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niseme vizuri, jana Mheshimiwa Msigwa amenukuliwa leo anasema tangu saa moja usiku walikuwa na Mwenyekiti, yeye, Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Mbewe mwenyewe baadaye wakaachana, Mheshimiwa Mbewe akamfuata Medeli; sisi tunajua alikwenda kunywa. Hata hili tukio la leo hilli jamani sisi tunajua, Mheshimiwa Mbewe kapanda ngazi kaanguka kateleza, kavunjika, huu ni ukweli kabisa.

Mheshimiwa Spika, na ukimsikia Mheshimiwa Msigwa analalamika kwamba Mheshimiwa Mbewe alinyimwa sijui wale walinzi waliondolewa. Mheshimiwa Lisu ameshambuliwa hapa wakasema ameshambuliwa na *system*, leo wanalamika eti walinzi wa Serikali wameondolewa walewale *system*. *System* walewale waliolalamika kwamba wamempiga sijui Mheshimiwa Lissu, ni uongo lakini leo wameondolewa sababu ya *Issue* ya corona baada ya kuwa wamegoma leo wanalamika eti Mheshimiwa Mbewe ameondolewa walinzi wake walewale *system*, uongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tupo kwenye corona Mheshimiwa Mbewe anatuambia *lockdown* mchana anajifanya *lockdown* usiku anakwenda bar kulewa, mchana *lockdown* usiku...

## TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Lijualikali kwamba Medeli inayotajwa ndiyo anayokaa Joyce Mukya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali endelea unapokea taarifa?

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea.

Mheshimiwa Spika, jiulize, na nataka watu wajiulize, CHADEMA imekuwa ikilalamika kwamba Dodoma hatuko salama, Lissu Kashambuliwa. Hivi inawezekanaje KUB atembee usiku peke yake hana ulinzi? Usiku wa manane wala hana mtu yejote wa kumsaidia? usiku KUB anatembea usiku saa saba peke yake? Na watu wanasema kwamba wao ni chama chenye umakini chama ambacho kinajienda kushika dola kuwa ni makini. Hivi unawezaje kuwa makini unashindwa kulinda uhai wako mwenyewe, ni umakini gani huo? Umakini upi huo? Na umeshasema Lissu ameshambuliwa Dodoma wewe kiongozi mkubwa unatembea peke yako usiku, peke yako, halafu unasema hizi ndizo akili mbadala! yaani akili mbadala ndiyo hii sasa! hii ndiyo akili mbadala hii ya kujifanya kwenye vikao unajifanya *live* hutaki sijui watu tuwe tunagusana usiku unakwenda *barna* wenzako mnakunyuwa mnalewa.

Mheshimiwa Spika, tungeweza kukaa kimya lakini kwasababu wameisingizia Serikali kwamba eti ameshambuliwa kisiasa, kwasababu wameingiza siasa yeye mwenyewe kwa kusema kwamba eti Serikali ama sijui mtu anataka akuzuie kwaajili ya uchaguzi akuvunje leo? yaani uvunjwe leo uchaguzi wa mwezi wa kumi uvunjwe leo kweli? halafu Serikali imekupa askari wanakaa kwenye mlango wako wanakulinda miezi yote hii yaani leo wasubirie eti ndiyo uvunjwe kimguu leo!. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania naomba mfahamu, natamani ku-*confess* hapa, hii michezo inafanyika, hii

michezo inafanyika. Ukitaka kujua ni usanii kwanini kaenda Nyuka na si *General* kaogopa nini kwenda *General?* alijua akienda Serikalini pale watamuonesha kwamba ameleta watasema tu wale jamaa kwahiyoo mzee alikuwa ameleta watasema tu ndio maana akaona akimbilie kule *private* ili akidhani kwamba atafichiwa siri.

Mheshimiwa Spika, mimi Morogoro nimewahi kuwa na kesi baada ya kuona jambo halijakaa sawa tukaenda hospitalini pale basi tunaumwa. Kwahiyoo haya mambo jamani huwa tunayafanya. Kwahiyoo niwaombe, na kama unavyoona hapa kuko kutupu, hivi ninavyokuambia nimeambiwa kaenda kupanda ndege anaenda Dar es Salaam, wala hata hapa hayupo tena. Hivi ninavyoongea sasa hivi Nyuka pale hayupo, kakimbia tayari, hivi ninavyoongea sasa hivi hayupo hospitalini.

Mheshimiwa Spika, wanasema kavunjwa miguu amekanyagwa kanyagwa; hivi wewe wanaume wakukanyage kanyage Mbowe wewe uinuke wewe! Kwelii!

Mheshimiwa Rais Magufuli na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi nataka niwaambie mko sehemu sahihi na salama. huu ujanja ujanja huu hautawafikisha sehemu yejote ni kujipotezea muda. Mimi huwa nasema huku ni sehemu ya watu kufanya dili zao tu, dili tu, hawana nia yoyote ya kusaidia nchi hii, hakuna nia yoyote, ni dili za watu. Vijana wanachama wa CHADEMA wananchi wa kawaida wanadhani kwamba watu wana imani na kuikomboa nchi. Watu wanatumia vibaya imani yenu. Yaani hiyo imani ambayo mnayo ambayo mnadhani kwamba sijui CCM haiwezi kuwasaidia, hiyo imani ambayo mnayo wenzenu akina Mbowe na wenzake wanaitumia vibaya kupiga fedha, hicho kitu hakipo. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwahiyoo mimi ninakwambia ukweli huyu mzee haumwi huyu mzee hajapigwa hajakanyagwa kanyagwa huyu mzee alilewa kaanguka kavunjika kifundo cha mguu *full stop*.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono azimio, nashukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huo ni mchango wa Mheshimiwa Peter Lijualikali. Mambo haya yanatuhusu sisi Wabunge wenyewe kwa wenyewe ndiyo maana kunakuwa kidogo, nilishindwa kueleza nafikiri mmeelewa kwanini nilishindwa kueleza. Kwasababu mtu aliyepigwa na kujeruhiwa sana kwa kweli hawezikupelekwa kituo cha afya ninyi wote si mnajua jamanii tofauti ya vituo vyaa afya na hospitali na nini sasa mtu uliyeumia namna hiyo utapelekwa kituo cha afya? Hilo swalii la kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Hapa nina barua, imenikuta hapa hapa nikiwa nimekaa hapa ya Halima Mdee anaomba usafiri wa ndege ili tumsafirishe Mheshimiwa Mbowe kwenda Dar es Salaam, ndiyo naipata sasa hivi. Sasa utaratibu wetu ni kwamba *referral* za namna hii huwa ni lazima ziwe zimetokana na hospitali ya Serikali tena ni ya ngazi kwa hapa Dodoma hii ya mkoa au Benjamin Mkapa. Ni vigumu ya kupata *referral* ya kituo cha afya halafu Bunge likaagiza ndege. Na wakati naipata hapa tayari wameshaagiza ndege wao wenyewe tayari wanampakia huko kwenda Dar es Salaam. Mwenzetu ameumia *we are not daring making a joke out of it*; lakini kinachoendelea kidogo kinafanya... lakini pamoja na yote kama nilivyo sema nimeenda kumuona, Mheshimiwa Waziri Mkuu amepata nafasi ya kwenda kule na kumuona na Mheshimiwa Rais mwenyewe amepata nafasi ya kwenda kule na kumjulia hali. Kwahiyoo kwa upande wetu tumetekeleza wajibu wetu na tutaendelea kumsaidia kwa lolote lile ambalo linahitajika; lakini isiingizwe siasa katika jambo ambalo kumbe wala siasa haimo kabisa kabisa.

Kwahiyoo ndiyo maana nikawa nasema Mheshimiwa Waziri Mkuu na hasa Waziri wa Mambo ya Ndani, alikuwa hapa ametoka nje, ni vizuri polisi wakatoa *statement* haraka tatizo la watu wetu ni *go slow* watoe *statement* haraka ya kile ambacho kile wanakijua kile kipande ambacho wanakijua kama kuna kipande bado wanafanyia kazi sisi hatuwafundishi lakini watoe kwanza. Kwasababu *society*

ikishakuwa *mislead* kuirudisha kwenye *track* huwa ni kazi kubwa sana. Kwahyo polisi watoke waeleze nini kimetokea na nini kinaendelea.

Nilikutaja Mheshimiwa Emmanuel Papian utafatiwa na Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na nishukuru kwa mleta hoja hii. Ninampongeza Easter ambaye ametuletea hii hoja ili tuweze kushukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa jinsi ambavyo Rais ameweza kubeba hili jukumu na utawala mzima wa Serikali. Nikupongeze Mheshimiwa Spika. Mimi nilikuwa na mpango kwamba kama nsingekuona kwenye hicho kiti baada ya siku tatu wakati corona inaendelea mimi nilikuwa nimepanga kukimbia. Sasa nilipokuona nikupongeze kwasababu ulipoendelea kuka a nililazimika na mimi niendelee kukaa lakini nilikuwa nimepanga kwamba nisipokuona mara tatu, Kiteto!

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Mungu kwamba Kiteto hakuna mtu ambaye amekufa kwa corona lakini tumeendelea kusali kwa kushirikiana na wenzetu ili taifa letu liweze kuondokana na janga hili la corona.

Mheshimiwa Spika, Rais ni kiongozi ambaye tumepewa na mungu kwasababu wakati anaingia madarakani tulimuomba Mungu; kwamba tunaomba Rais ambaye ataiongoza Tanzania iwe hivi ilivyo; tunamshukuru sana Mungu. Baada ya hapo tulishukuru Mungu kwasababu alipoingia madarakani ametutendea yale ambayo Mungu amemuongoza aweze kuyafanyia watanzania wote, kwahyo tunamshukuru sana Mungu.

Mheshimiwa Spika, Rais Magufuli ni kama Mfalme Suleiman, yote yaliyomkuta Mfalme Suleiman kama majaribu aliweza kuyashinda kwasababu alimuamini Mungu; na sisi Rais

wetu hata kama kutatokea majaribu ya namna gani atayashinda kwasababu Tanzania ni taifa teule la Mungu ambalo Mungu ameamua kwamba liweze kuongozwa na yeye. Kwahiyo tulipoomba akatupa na yeye akamuamini Mungu atatufikisha kule tunakotakiwa kwenda salama.

Mheshimiwa Spika, Rais Magufuli ni kama yule mama ambaye ilipotokea njaa kwenye nchi aliacha ameinjika chungu cha mawe kwenye jiko akawasha kuni watoto wakabaki na imani kwamba chakula kitaiva watakula; mama akaenda kuhemea akarudi akainjika chungu ili watoto wakapate kupata chakula. Rais wetu Magufuli alituma ndege Madagascar ikaleta dawa watu wakapata huduma. Hiyo inaonesha ni jinsi gani Rais wetu amejitolea kuhakikisha kwamba anaokoa Watanzania wetu.

Mheshimiwa Spika, ukija kuchunguza Watanzania kuna jambo ambalo tumekuwa tunalikimbia. Ukiangalia Tanzania siku za nyuma tulikuwa hatusali ipasavyo, tulikuwa hatusali ipasavyo japo tuna dini. Kwanini nasema hivyo; kama tungekuwa tunasali ipasavyo tusingeweza kuwa na historia ya kukatana vipande vya albino Tanzania. Kama tungekuwa tunasali kweli tusingefika huko. Sasa tumeanza kusali, Rais wetu ametuongoza akasema tusali Mungu atatuondoa kwenye majanga kama ya corona. Watanzania wote wamepiga magoti watu wamesali ndani ya nyumba zao, ndani ya familia zao misikitini hadi makanisani. Kipindi chote ambacho kulikuwa na Kwaresima watu wote walikuwa wanaombea corona iondoke. Kipindi chote ambacho wenzetu walikuwa kwenye Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, walikuwa wanaombea corona ili iweze kuondoka kwenye taifa letu.

Niombe kushukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa kiongozi ameonesha kwamba Watanzania sasa ni wakati wa kufungua ukurasa mpya wa kupiga magoti na kujielekeza kwa Mungu kwa yote ambayo yatatokea.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais. Ukiangalia Tanzania yetu tangu iwepo na iwe na

Watanzania hawa hawa Mungu alivyopanga alielekeza Tanzania isifungamane na upande wowote. Nchi nyangi zimewekwa *lockdown* Tanzania hatukuweka *lockdown* tumeweza kuokoa *economy* ya nchi imeweza kuendelea tuka-stabilize tunaendelea kufanyakazi tumeweza kufanyakazi watu wakaendelea kuishi maisha ambayo ni lazima watafute chakula na riziki iendelee.

Mheshimiwa Spika, Iakini corona kama ni *virus* huwezi ku-plan kwamba imekuja itaondoka mwezi Septemba kwahiylo kwasababu itaondoka Septemba tunaweka *lockdown* tunatumia bajeti tulionayo ili tuweze kuwa tumefunga *after* Septemba kwahiylo tutakuwa *free as if* ni kipindupindu. Corona tutaendelea kuishi nayo tutai-control tutai-manage, na Watanzania wataendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa na huo muono na mwisho wa siku Watanzania tutafanyakazi na bajeti zetu zitaendelea na kazi zetu zitaendelea ili maisha ya Watanzania yaweze kuwepo. Ukiweka *lockdown* kwa *virus it means virus* haitaisha nchi itaendelea kupata matatizo Iakini Watanzania wetu wameendelea kubaki salama. Wote ni kuendelea kumuomba Mungu aweze kumuongoza Mheshimiwa Rais wetu aweze kuendelea kudumu na aweze kufanyakazi kwaajili ya kuwashudumia watanzania wote kwa namna ambavyo sisi tunaendelea kumuamini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo tunakushukuru na nakushukuru kwa nafasi ambayo nimeweza kupewa ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Papian. Nilishakutaja Mheshimiwa Allan Kiula utafatiwa na Mheshimiwa Dkt Saada Mkuya.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, nami nishukuru kwa kunipa nafasi ya kusema maneno machache kuweza kuunga mkono Azimio hili muhimu ambalo limekuja wakati mwafaka kabisa. Tunatambua kwamba

tutakaochangia tutakuwa wachache lakini tutakuwa tumewawakilisha Wabunge wenzetu kwasababu wote tuna mawazo sawa na wote tunatambua kazi kubwa inayofanywa na Rais.

Mheshimiwa Spika, mimi nilijaribu kutafakari kidogo na kupitia vitabu mbalimbali ambavyo nimesoma nikiwa masomoni; nikagundua kwamba Rais wetu anazo tabia (*characteristics*) mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, moja, yeye ni *visionary leader*, anaona mbali. Janga hili la corona lillipoingia nchi zote duniani mataifa makubwa yalitaharuki, na baada ya kutaharuki yakaanza kufanya *copy and paste*; kuchukua mbinu zilizotumika nchi fulani nao wanapeleka kwenye nchi zao. Lakini Rais alikaa akatafakari na akatumia muda wake akaona ni muda mwafaka wa kuendelea kutoa uongozi; na tulipofika leo hii tunaona kwamba kweli huyu *visionary leader*.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni *charismatic leader*, ni kiongozi mwenye karama; ni viongozi wachache sana wanaoweza kuwa na karama; na jambo hili limejidhihirisha.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye chombo cha baharini kama unaenda Mafia kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dau hapa mtu yejote anaweza kuendesha mtumbwi lakini bahari inapochafuka ndipo tunajua nani mwenye leseni kamili. Sasa kwa yeye kuwa *charismatic leader* tumeweza kuona kwamba ana leseni kamili na ni kiongozi bora.

Mheshimiwa Spika, lakini Rais wetu pia amejipambanua kwamba yeye ni mwanasayansi kamili kwasababu baada ya janga hili kutokea mambo mengi yametokea alikaa chini akatafakari mpaka akawa na mashaka na vipimo vinavyopima hili janga la corona; na baadaye tunaona mataifa makubwa nayo yalikuja kufanya utafiti na kuona kwamba vipimo hivyo vina changamoto. Kwahiyo Rais wetu ni mwanasayansi lakini alikumbuka

alivyokuwa anafundisha masomo ya sayansi kabla hajawa Mbunge na kabla hajawa Rais.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ni mtafiti, ni *researcher*. Amewatangulia mbele watafiti na ameweza kufanya utafiti ili kuweza kutoa njia ya jibu hili. Rais wetu ni mchumi, *best economist*, ni mchumi mzuri. Mataifa makubwa *world bank* na *IMF* walisema watukopeshe yeye akakaa chini akasema hatuhitaji mikopo tunataka mtufutie haya madeni. Hilo ni jambo kubwa na inahitaji uwe na nguvu za ziada ili uweze kutoa kauli hiyo kwa mataifa makubwa. Mpaka leo hii tunavyozungumza ziko nchi hata za Afrika Mashariki ambazo zimechukua mkopo huo, lakini sisi Tanzania hatukuomba, Rais alisema tutapambana kama tulivyo na tutaona tutafika wapi.

Taarifa zilizotolewa na Benki Kuu zilikuwa zinaonyesha uchumi wetu ullikuwa unakua kwa asilimia 6.8 na kwaajili ya janga hili la corona nchi kubwa zenye *muscles* zilitabiri kwamba hali ya uchumi itashuka na wakatoa *statistics* za uchumi kushuka. Kwahiylo Rais wetu akakaa akatafakari akaona lazima aende njia nytingine. Wakati mwingine ukienda barabara ukiwa peke yako unaweza ukaona umekosea lakini hakuwa amekosea. Kwasababu hatua alizochukua ikiwepo kusema kwamba Tanzania hatutafanya *lockdown* ilikuwa ni hatua kubwa sana. Na alisema Dar es Salaam haiwezi kufungwa. Humu ndani Bungeni kulikuwa na hoja hata mpaka za kuahirisha Bunge kwanini tuahirishe Bunge wewe pia ulisimama imara kwa kutokuahirisha Bunge na ukatafuta mbinu mbadala.

Mheshimiwa Spika, na wenzangu wamesema wapo wa mama wanaotembea wanauzu nyanya, wanauzu mchicha hawa wajasilimali tuliowapa vitambulisho vya wajasiliamali wangekula wapi? Kwa hiyo, Rais aliona mbali akweza kuona njia sahihi namna ya kutupeleka kwa jambo hili sio kwamba alikuwa hioni shida, shida alikuwa anaiona na hatari alikuwa anaiona.

Mheshimiwa Spika, lakini aliona asimame imara na atoe uongozi na uongozi sahihi. Rais wetu pia ameonyesha

kwamba ni mcha Mungu kwasababu alisema tusali, tufunge na alimtegemea Mungu nilliona walisema *we don't need prayers*, kauli fulani ambayo ilikuwa kama inamdhihaki lakini Rais wetu alisimama imara alishirikisha madhehebu yote kusali na sasa tunapata matokeo yake ambayo ni matokeo yenye mwelekeo mzuri. Kwa ujumla wake nimejaribu kuonyesha jinsi Rais wetu ambavyo amekuwa akitoa uongozi na Rais wetu ameingia kwenye changamoto kubwa kwasababu kulikuwa na tishio la anguko la uchumi, anguko la uchumi ni tatizo kubwa sana lakini ameweza kusimamia na uchumi wetu tunakwenda ziko changamoto za hapa na pale tumezipata lakini shughuli za kiuchumi zinaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kulikuwa na suala la anguko la kisiasa kwasababu nchi zingine watu wameanza kuandamana maana yake hilo ni anguko la kisiasa kwa hiyo Rais wetu alitambua hilo ni anguko la kiuchumi na anguko la kisiasa akatafuta mbinu mbadala ya kuweza kutoa uongozi na kuweza kufanya Tanzania iweze kuvuka salama. Alisema hii pia ni vita ya kiuchumi pamoja na mengine yale hii ni vita ya kiuchumi kuna mtu mmoja mtafiti mmoja alisema chanzo ikija itagharimu kiasi gani? Kwa hiyo, Rais wetu aliweza kutoa maelekezo sahihi na timu yake ikiongonzwa pia na Mheshimiwa Wazari Mkuu waliweza kutoa uongozi sahihi kabisa ili kuweza kupambana na janga la corona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa ambayo inaendelea nchi ikiwepo ujenzi wa *Stiegler's Gorge* ungeweza kusimama, ujenzi wa reli yakisasa ungeweza kusimama watanzania wangapi wameajiriwa hivi wiki moja iliyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa takwimu za watanzania walioajiriwa kwenye ujenzi wa reli ya Mwendo Kasi, kwa hiyo, watu wote wangekuwa hawana ajira wangekuwa wapo nyumbani. Nchi zilizo endelea zilifanya *lockdown* zina uchumi mkubwa na uchumi huo unaweza kuwapa watu maisha kwa muda fulani na zenyewe zimefeli, Marekani na zenyewe sasa hivi inahangaika Rais wetu alitambua hilo jambo na kulikuwa na vitisho vingi humu ndani yupo Mbunge alisema tutakuwa tutoa jeneza moja baada ya jingine na Bunge tulisema alaniwe na amelaniwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwasababu bado tupo imara na tunaendelea na leo tunaendelea kupilisha bajeti, hii shughuli ya bajeti isingipita hii watu wangkuja kusema wapinzani kwamba tumevunja utaratibu Serikali inatumia fedha inapotaka yenyewe lakini mwenyenzi Mungu yupo amesimama na sisi na tuendelea kukamisha kazi ambayo ipo mbele yetu. Rais hakuwa peke yake walitokea majemedali wengine Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Msukuma, Mheshimiwa Mama Prof. Tibaijuka walionyesha namna ya kupiga nyungu, walionyesha namna ya kupiga nyungu. Kwa hiyo, hiyo yote iliweza kusaidia kuweza kutuimarisha kisaikolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wengi hawajui pamoja na sifa zote uki-*Google* sasa hivi utagundua kwamba katika afrika Rais Dkt. Magufuli ni mmoja ya wasomi anaweza kuwa Rais wa kwanza au wa pili kwa usomi kwa hiyo, ametumia usomi wako huo na pia mwenyekiti ambaye huwa nakusaidia alisema Rais Magufuli ni *genius* ametumia *genius* huo kuweza kubashiri mambo yanaweza kutokea lakini kutafuta mikakati kuwavusha watanzania na sisi tunaona kila dalili ya watanzania kuvuka tunapata taarifa yakupungua kwa wagojwa tunapata taarifa za hospitali kufungwa sehemu ambazo wagonjwa walikuwa wanapokelewa, lakini bado Rais amesitiza kwamba tuchukue taadhali. Vyo vimeweza kufunguliwa na tunataraji watoto ambao wapo nyumbani wa ngazi mbalimbali watafungua watarudi shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Magufuli ameweza kunusuru uchumi wa taifa, Rais Dkt. Magufuli ameweza kunusuru hali ya kisiasa Tanzania, Rais Dkt. Magufuli ameweza kutunusuru na sisi watanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo amechangia Mheshimiwa Lijualikali na wewe mwenyewe taarifa za matatizo ya wenzetu haya zinatakiwa zitolewe mapema kwa vyombo vyoma habari kwa sababu chombo cha habari kikiandika hicho kitu ndio kinaaminiwa. Hasa kama kuna jambo lingine hilo jambo lizungumzwe haraka vyombo

vya usalama na ulinzi vitoe taarifa kulikoni na kilichotokea ni kitu gani? Maana yake haya mambo ndiyo yakukemewa, amesema Mheshimiwa Lijualikali sanaa zinachezwa na hizo ndio sanaa zenyewe za kuelekea Oktoba na Rais alisema uchaguzi upo na uchanguzi utakuwepo na tutakwenda kushiriki kwenye uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hasa kama maji yameshakuwa maji marefu wasitafute sababu za maji marefu tunamuombea Rais wetu maisha marefu, Spika tunakuombea maisha marefu, Waziri Mkuu tunamuombea maisha marefu, Makamu wa Rais tunamuombea maisha marefu, na watanzania kwa ujumla tunawaombea maisha marefu, tumeposta kiongozi bora na kiongozi anayetoa uongozi na kiongozi anayejali watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimo nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiula kwa mchango wako mzuri sana Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kunipa nafasi yakuchangia hii hoja kuhusiana na Azimio la Bunge la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Tanzania Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna alivyoongoza Taifa katika mapambano dhidi ya janga la Ugonjwa wa Corona yaani COVID-19. Kwanza naunga mkono Azimio hili lakini nachukua fursa hii sana kumpongeza Mheshimiwa Esther Mmasi kwa kuja na *idea* hii ya kuleta hili Azimio katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni tulizania wakati tuko katika *critical position* Mheshimiwa Esther tulijadili jinsi gani tunaweza tukaleta Azimio. Angalau tu Azimio la Kumpongeza Waziri wa Afya kama Mwanamke ambaye alikuwa amesimama *despite all odds* yaani pamoja na changamoto lakini alisimama imara.

Mheshimiwa Spika, lakini kwasababu Mheshimiwa Waziri ni mteule wa Mheshimiwa Rais, na kwasababu yeze Mheshimiwa Rais ndiye anayeongoza hii vita. Mheshimiwa Waziri akiwa msaidizi wake, basi imekuwa busara na vyema kuleta Azimio hili katika Bunge letu hili Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, janga linapotokea katika eneo lolote, anaetizamwa ni Kiongozi jinsi gani kiongozi atakavyo-*react* ndivyo athari ya janga litakavyokuwa. Mheshimiwa Rais kwenye hili jambo la kwanza alilolifanya pamoja na nyanja zote za kuzuia ndege zisiingie, kufunga shule. Lakini alisimama imara kuona kwamba anatuondoshea hofu. Na hili ndio jambo la msingi katika kukabiliana na jambo lolote ambalo linaweza likaleta madhara. Lazima uondoshe hofu ili uweze kuondosha madhara mbele yako.

Mheshimiwa Spika, katika hili kwasababu ni jambo ambalo limeingia kisaikolojia, Mwalimu wangu wa *biology* aliwahi kuniambia katika *causes of diarrhea* yaani wakati tulipokuwa tukisoma maradhi ya kuharisha aliniambia kwamba jambo moja ambalo litakufanya wewe uharishe au utapike ni ile *desire* ya kutaka kuharisha au kutapika. Yaani *psychological* inakuja kwamba wewe una-*feel* kama unataka kufanya hivyo. Kwa hiyo, ile inajengwa na hofu, Mheshimiwa Rais alipoondosha hofu na sisi Watanzania tukaweza kusonga mbele. *Otherwise* tulipokuwa tukipata taarifa za masuala mbalimbali hizi za kutisha tulikuwa tumerudi nyuma tumeingiwa na hofu tumejengwa na hofu kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini alitupotuondoshea hofu yeze kama Kiongozi basi na sisi kama Watanzania tumeweza kusimama imara. Hata *WHO at one point of time* wakasema tujaribu sana kupunguza kuangalia ama kusikiliza taarifa mbaya zinazohusiana na ugonjwa huu. Ili kwasababu linaweza lika-*create* hofu na linaweza likarejesha nyumba mapambano dhidi ya ugonjwa huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Rais alituambia, siku za mwanzo tu katika ile dhana ya kuondosha

hofu akasema labda itabidi tuendelee kuishi na huu ugonjwa. Yaani utakuwa ni ugonjwa wa kawaida, maneno yake hayakuanguka, WHOao wakatoa hiyo taarifa kwamba hivi virusi itabidi tuendelee kuishi navyo, tutafuta *mechanism* tutafute namna ya kuendelea ku-*adopt* kuishi na hivi virusi. Kwa hivyo hili jambo limekuja tumelipokea kwasababu tulikuwa wageni nalo na tutaendelea nalo. Cha umuhimu tuendelee kuchukua tahadhari kama vile ambavyo Viongozi wetu wameendelea kuzungumza. (*Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine *economically* mara nyingi tunaweza tukaangalia changamoto katika mlango mmoja. Lakini hatuoni changamoto hizi zinaweza zikaleta fursa gani za kiuchumi. Kusimama kwa Mheshimiwa Rais kuona kwamba jamani tuendelee kujilinda lakini shughuli hizi zisisimame ni kwamba imeweza *ime-create opportunities* kwa wajasiriamali wenzetu. Sasa hivi Watanzania wanaweza kutengeneza sabuni za kunawia mikono kwa kiwango kikubwa na kiwango kizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaweza wenyewe kutengeneza masks kwa kiwango kizuri kabisa. Lakini vile vile hata *sanitizer* hizi zamani ulikuwa unakwenda unasafiri ndio unanua sasa hivi zinapatikana tu Tanzania na zinatengenezwa tu kwa kiwango kizuri. Lakini vile vile kwa mara ya kwanza hata wenzetu Madaktari wa Muhimbili, tumepewa taarifa kwamba wameweza kutengeneza *PPE*. Wenzetu Uingereza waliagiza *PPE* kutoka Uturuki na mzigo ulipokwenda kwasababu ulikuwa sio katika *quality of standard* waliyoitaka imebidi urejeshwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo wenzetu wa Muhimbili wameweza kutengeneza hizi *PPE*. Pengine kusingekuwa na changamoto hii wasingekuwa wanafikra na mawazo na teknolojia ya kutengeneza vitu kama hivi. Kwenye jambo jingine, jambo la kisiasa Mheshimiwa Rais wakati mwanzo katika janga hili alisema uchaguzi utakuwa pale pale. Maneno yake hayakuanguka wiki iliyopita *Secretary General* wa *United Nations* anatoa taarifa kwamba katika Siku ya Afrika anasema zile nchi ambazo zina uchaguzi katika mwaka

2020 zisiahirishe chaguzi hizo. Kwa hivyo ni masuala ambayo tunaendana nayo *Internationally*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini unajua mara nyingine unaweza ukafanya zuri na kila mtu asilione lakini likawa bado ni nzuri hata kama unalofanya nipeke yako na tunaweza tukafanya dhambi wote humu lakini bado itabakia dhambi hata kama sote tutafanya dhambi. Hivi kuna ubaya gani sisi Watanzania kuwa na mtazamo totauti hakuna ubaya tulikuwa na mtazamo tofauti lakini ni mtazamo ulio sahihi. Sisi waafrika tunajipambanua sisi ni maskini, sisi ni nchi zinazoendelea, sisi tuna uchumi mdogo, wenzetu ndivyo wanavyotumbanua na sisi tumekubali kuwepo tuwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini ikawa sisi tuwe tuchukue *the same line* na wenzetu ambaao wameendelea wakati sisi ni maskini tuko tofauti sisi ni watu ambaao tumekubwa na maradhi sisi ni watu chumi zetu zipo ndogo. Lakini kwenye la corana lazima tufuate wale ambaao wamekwenda kwenye njia tofauti nadhani ni jambo la kufikirika kwamba *at one point of time Africa* tunaweza kutachukua mtazamo wetu sisi tofauti usiwe sawa sawa na mtazamo mwingine wa dunia na bado tukawa *successful is high time now* tuweze kujiamini sisi wenyewe lazima tujiamini sisi wenyewe tujiamini na maamuzi yetu tunayochukua ambayo yatakuwa-fit kutokana na mazingira yetu tunayoishi hakuna dhambi Tanzania kuchukua *approach* iliyochukua kwa maslahi mapana ya Taifa ya hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jana kulikuwa na azimio la kukupongeza binafsi yangu sikupata nafasi hiyo, lakini naomba nikupongeze naomba nichukue fursa hii ni kupongeze kwasababu katika mambo ambayo pengine yanaweza kuathirika kugusana gusana hivi vitu ni pamoja na hivi kushika shika. Lakini ulifikiri *ahead* ulifikiri *ahead* hukutegemea kutakuwa na corana ambayo ita-*prohibit* sisi kuwa tunashea vitu vingi ikiwemo makaratasi lakini ulikuwa unafikiria katika njia ambazo tutaweza na ulimwengu huu wetu wa leo mambo mengi yamefanyika, mambo mengi

umeyafanya kwasababu kama usingekuwa unataka usingefanya ungetoa amri lisifanyike tu na halifanyiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ume-*think ahead*, ume-*think ahead* na hii jitihada kama hizi zimemwesha hata Mheshimiwa Rais kuchukua *approach* hii kwasababu kuna means na mechanism ya kuendelea bila ya kuchua vitu hivi makaratasi na ma-book na ma nini kumbe tungeweza kuendelea labda *thinking* ile kwamba tuahirisha Bunge what would do think yaani tungekuwaje leo hii how far tungekwenda. Lakini tumefikiri vizuri Mheshimiwa Rais amefikiri vizuri na ameliongoza Taifa katika hili. Umemsaidia Mheshimiwa Rais katika kuchukua maamuzi ya busara zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi lakini tunaomba lakini tunaomba sisi tuendelee tunamuombea sana Mheshimiwa Rais afya njema, awe na nguvu kuipeleka Tanzania ile ambayo tumekuwa tukii-dream tokea uhuru unapatikana. Hii njia tunayochukia ni positive approach na kama tutampa support Mheshimiwa Rais Tanzania katika kipindi kifupi tutafikia malengo yale ambayo tumeyafikia cha umuhimu tujiamini, tujiamini kwamba tunaweza tukafanya maamuzi sahihi tujiamini sisi kama watanzania kama sehemu ya Afrika kwamba tunaweza tukachukua approach tofauti na wenzetu na mabara mengine lakini bado tukachukua njia sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa wale wenzetu ambao sasa hivi wanahamu sana kufanya *reasech is hard time* hata tunawaambia wenzetu waliopo katika katika mataifa ya nje waandae *papers* nyangi kuwangalia jinsi gani zile *model* zao ambazo wali-predict kwamba Afrika tunaweza kukaangamia Afrika tunaweza tukafanya. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nadhani *is hard time* waangalie tena jinsi gani sasa wanaweza kui-model Afrika katika *contest* ya ulilimwengu. Maana yangu nini, sio lazima kwamba afrika tupangiwe uchumi wetu kutokana na *model* ambazo wenzetu wamezi-develop kumbe kuna vitu vingi kumbe kuna

*factors* nyingi hawaji-*consider factor* zenyewe ni pamoja na uongozi imara ni pamoja na udhabitii wa watu lakini ni pamoja na njia sahihi tunazozichukua za maisha yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mwenyenzi Mungu ametujalia tuna vitu vingi vya kujivunia, leo hii sasa tunarudi katika njia zetu za awali, leo hii tuaambiwa ili tuweze kusa-*sustain* basi tule vyakula vya asili tuwe tunafanya mazoezi ni vitu ambavyo wazee wetu walikuwa wakivifanya unaweza kijiji ukamkuta mama ana miaka tisini, mia anakwenda kulima ni *part* ya mazoezi *it's a high time* sasa akili zetu zifanye kazi sawasawa na viwiliwili vyetu Mheshimiwa Rais ametuonyesha njia basi hatuna budi sisi watanzania kuifauata njia hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia moja na ninakushukuru sana wa nafasi hii. (*Makofii/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Saada Mkunya tunakushuru sana kwa mchango wako kwa kweli Waheshimiwa Wabunge mnatukumbusha mbali ni ukweli usiopingika tumepita mapita kwenye hili janga la Corona ulikuwa ni mtihani mkubwa sana. Nani kweli wengine wanatusifia hapa lakini kwasababu tulikuwa na kiongozi ambaye tukigeuka nyuma anakuwa amesimama imara kabisa ndio maana tukapata ushujaa wa kusema hapa hii bajeti mpaka iishe na tulisema hapa hii Corona hata ikimchukua Ndugai au ndani atakayefuata, atakayefuata mpaka iishe na Inshallah itaisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulifika kipindi kile cha Corona Waziri Ummy anatoa takwimu *almost* kila siku ni sisi Bunge tulimwambia aaa hii kila siku sijui ngapi ngapi hapana sasa angalau iwe kwa wiki mara moja hivi na n.k. kwasababu ile yote tulisema namma hiyo kwasababu inaongeza hofu inawafanya watu saa zote wawe wanaangalia wangapi leo na kadhalika.

Hata watu walipopoteza maisha na kuanza kuzikwa kusiko eleweka tulipiga kelele sisi mtakumbuka na sisi kwa mfano tukaiomba Serikali tulipompoteza mchungaji

tukaiomba Serikali kwamba sisi huyu wa kwetu pamoja na yote na utaratibu unaoendelea azikwe pale familia inapotaka na ikawa.

Alipoondoka Mheshimiwa Ndassa ilikuwa bado utaratibu ni ule, tukasema sisi tunapeleka wa kwetu mpaka Sumve, tukapeleka. Alipoondoka Waziri Mahiga, tukapeleka; na imesaidia, leo hii hakuna unyanyapaa huo tena wa kuweza kumweka mtu popote tu pale na familia zinasaidiwa na wapendwa wao namna ya mahali pa kwenda kuwazika. Kwa sababu wengine ilikuwa wakipata hata homa nyingine zozote au hisia za ugonjwa wa namna hiyo, kwa hofu iliyokuwepo, ilikuwa baadhi ya familia zinawakimbia wagonjwa wao kwa sababu hofu ilikuwa kubwa sana. Kwa hiyo, watu wengine wamejfia kwa maana hiyo. Kwenye mahospitali baadhi ya Wahudumu wa Afya walikuwa wanawakimbia wagonjwa.

Baada ya hofu hii kupungua, kwa msimamo wa Rais wetu na kazi kubwa ambayo pia Waziri wetu wa Afya ameifanya, nasi Watanzania kutiana moyo, kwa kweli tumefika hapa tulipo. Leo hii unapigiza simu kabisa na mtu anayejhishi ugonjwa huo anakwambia; bwana naona kifua kinanibana, sijui *Corona* hii, sijui nini? Wanajipiga nyungu na kadhalika, anakupigia keshokutwa yake tu wala hata siyo wiki, anakwambia *hallow*, aah, niko fiti. Imeshakuwa ni moja ya magonjwa ya kawaida.

Tuendelee hivyo Watanzania. Hili la kutupunguzia hofu, Serikali mmetufanya jambo kubwa sana chini ya uongozi wa Rais wetu, tunawashukuruni sana na tuendelee nalo kuwapunguzia Watanzania hofu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ally Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. Kusema kweli hakuna Mtanzania hata mmoja hakuwa na hofu, tuseme ukweli. Ni

Rais pekee alikuwa jasiri. Tukisikia Italia 2,000 wamekufa; Spain 3,000, wote tulikuwa na *shock*. Mheshimiwa Rais peke yake uamuzi wake umetufanya namna hii katika nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tusidanganyane na tusiwe wanafiki, sisi wote tulikuwa katika hofu kubwa. Mheshimiwa Rais peke yake ndio jasiri aliye katika mpango wa kuwa sawa sawa ili tutulie. Ukitikia Italia 2,000, kulikoanzia dini kule kule Italia na Saudi Arabia wamefunga Misikiti na Makanisa, wote tulikuwa tunatetemeka. Jasiri ni Mheshimiwa Dkt. Magufuli peke yake katika nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa napata taabu sana. Mimi nina marafiki sehemu mbalimbali, wanasema baada ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli atafuata nani katika nchi yenu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leteni Azimio la kumwongezea muda, akitaka asitake. Maana Mheshimiwa Rais alipotufikisha ni pazuri. Labda nyie hamsumbuliwi. Ni Rais peke yake ametoa mfano katika dunia nzima hii. Kuna nchi nyingine wanapigwa, watu wamepigwa kwa ajili ya *Corona*. Wameuawa; wote mmesikia, mmeona kwenye Televisheni na *YouTube* mmeona wanafuatwa mpaka Makanisani, Misikitini wanapigwa tu viboko. Watu wamekufa kwa njaa. Rais wetu Mwenyezi Mungu amempa msimamo wa hali ya juu. Lazima tumpongeze kwa hali ya juu. (*Vigelegele/Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninashangaa kuna watu wengine wanafiki wanafiki. Unafiki tunao! Katiba siyo msahafu, wakati wowote inabadilishwa. Atakuwa sio Rais wa kwanza kuongezewa muda, alazimishwe, akitaka asitake, alazimishwe. Tukakwenda kubaya baada ya Rais huyu. Haiwezekani kumwachia nafasi aseme anakataa tu, nasi tuseme amekataa. Amekataa kwa vipi? Alazimishwe tu! (*Makof/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy ngoja twende kwenye Uchaguzi Mkuu, turudi, nami naamini sote tunarudi, *inshallah*. Mwenyezi atuweke, hilo ulishike uwe nalo moyoni. Tutarudi

hana salama, Azimio hilo utakuja kulileta wewe hapa Mzee Keissy na litapita kwa kishindo, atake asitake tutaongeza muda. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Endelea Mheshimiwa. (*Makofi/Vigelegele*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nimekubali maelezo yako, naunga mkono hoja yako moja kwa moja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kitendo alichofanya cha Corona tu hiki, dunia nzima hakuna, kila mtu anam-*support*. Napata shida, labda nyie hamna marafiki duniani huko na nchi nyingine, lakini mimi kila siku napigiwa simu, nani baada ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli? Sina jibu. Jibu langu nawaambia anaongeza muda. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ataongeza muda akitaka asitake, tutapiga kura ya maoni. Leo nimemsikia dada yangu wa tena wa *CUF*, hakuna aliyechangia kwa uchungu na kwa ukweli kama Mheshimiwa Lulida hapa, ndio mchangiaji wa kwanza, amechangia vizuri. Amekuja Baba Paroko, tunamwamini sana, tena ni Mpinzani. Sasa kumebaki nani wa kusema sema hapa? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Hakuna! Mheshimiwa Lulida kamaliza, Baba Paroko kamaliza, Mheshimiwa Lijualikali kaja kuwachinjia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dada Esther aliyeleta hili Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini sasa kinafuata nini hapo? Tutakuwa tunapongeza, tunapongeza tunapongeza; baada ya miaka hii tunapongeza kitu gani? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Aendelee tu. (*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Aendelee tu. Hii Katiba siyo msahafu. Tupige hata kura. Hiyo Oktoba tupige na kura ya kumtaka Mheshimiwa Rais aongeze muda. Haitakiwi gharama mara mbili, tuseme kuna gharama kwenye maoni. Maoni mtu anatumbukiza na kura kumtaka Mheshimiwa Rais au kutotaka Mheshimiwa Rais kuongeza muda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais akituletea jibu la kusema kwamba mimi hapana sitaki, tunamlazimisha. Tuna viongozi wanataka kumlazimisha kwa nguvu akitaka asitake. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, nikuhakikishie Bunge hili ndio lina mamlaka ya kutengua hicho kipengele, Bunge hili. Kwa hiyo, liko ndani ya uwezo wetu. (*Makofi/Vigelgele/Kicheko*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Azimio lije tutengue hicho kipengele haraka iwezekanavyo. Mimi mchango wangu ndio huo. Haiwezekani janga kama hili la dunia nzima, ilitetemeka dunia nzima lakini Rais wetu amekuwa na msimamo wa hali ya juu. Haiwezekani, haijatokea! Tusiwe wanafiki! Haijatokea! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi nyininge ukiangalia watu wameuawa kwa *Corona* hii; watu wanapigwa kwa *Corona* hii; wamekufa njaa kwa *Corona* hii, lakini Rais wetu alikuwa na msimamo wa ajabu kabisa. Haiwezekani Mwenyezi Mungu amemwongoza kwa hali ya juu kabisa. Kwa nini tusimwombe? Yeye amekuwa nani asiombwe akaongezewa muda? Asitusikia sisi wananchi wake kwa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunamwomba lazima aongezewe muda akitaka asitake, sisi ndio tunamwomba. Hatukubali, hamna mjadala mwengine. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keissy, ubarikiwe sana, tunakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Joseph Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Naunga mkono Azimio la Mheshimiwa Ester la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Niungane na Wabunge wenzangu kwa maneno mazuri waliyoyazungumza toka mjadala ulivyoanza. Kwa kweli hatuna budi Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa yale aliyoafanya kwenye gongwa hili la *Corona*. Hili ni fundisho kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameweza kumtegemea Mungu, lakini cha pili, akasema tutumie na akili tulizopewa na Mungu. Ndiyo maana mwanzoni hapa tulipoanza kuwaeleza Waheshimiwa tunazo kinga za *Corona* za kienyeji mkawa mnakwepa kwepa, tukaamua turudi Majimboni tukafukize wananchi wetu. Tunavyozungumza, mimi Jimbo langu ni bam bam, sijawahi kusikia mtu ameugua *Corona*, wote wamekula nyungu.

Mheshimiwa Spika, hii sasa kwa Mheshimiwa Ummey naomba kule kwenye Wizara yake kuwe na watu maalum wa kuendeleza hivi vipaji. Najua sasa hivi *Corona* itaisha kwa sababu ya nyungu. Nina imani; halafu baada ya hapo mnawatelekeza, hamna kitu kingine mnaweza kuwaendeleza hawa watu ili wajipange, linapotokea suala lingine waweze kukabiliana nalo na kuwasaidia wataalam wetu ambao walifeli kwenye kipindi hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tumejifunza mengi sana kupitia Mheshimiwa Rais, msimamo. Msimamo wa Rais ndiyo umetuponyesha *Corona*; hata kama ipo, sisi tunaamini tumeshapona. Hii siyo suala la *Corona* tu, sisi tumeona hata kwenye sheria nyingi mambo mengi ambayo Mheshimiwa Rais na timu yake ameyasimamia, watu humu ndani tulikuwa tunazodoana.

Mheshimiwa Spika, nikikueleza, sisi tumelalamika kuhusiana na kodi za migodi miaka na miaka, tawala na tawala, tumepitisha sheria hapa mwaka 2017, Geita tulikuwa tunalipwa dola 200,000 kwa mwaka, leo tunalipwa bilioni 10. Sasa ni lazima kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Geita tumtakie maisha mrefu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi sio sawa sana na Keissy, unajua tukimlazimisha kwa vifungu anaweza akatushinda kwa vifungu. Sisi Kisukuma tukikulazimisha ukashindikana, tutatumia kienyeji mpaka unakubali; tunakuita kwenye dawa. Sasa tusubiri kama alivyoeleza; na kwa kuwa tutarudi, tutatumia mbinu zozote, hakuna kuchagua silaha, ili mradi Mheshimiwa Dkt. Magufuli akubali na atakubali. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, linge ninampongeza sana kijana mwenzangu Mheshimiwa Lijualikali kwa maneno mazuri aliyozungumza. Saa nyiningine kumbe watu wenyewe akili wako wengi tu, sema wanakuwa wanafunikwa na vilaza huku. Tunampongeza sana Mheshimiwa Lijualikali kwa kutoa ile taarifa.

Mheshimiwa Spika, nami nilikuwa na mawazo kidogo, kama ulivyosema Polisi watoke watoe taarifa, lakini kabla ya Polisi; unajua mimi nasoma hapa mitandaoni Spika ameenda kusalimia, Waziri Mkuu ameenda kusalimia, Mheshimiwa Rais; hivi hamna kazi? Eeh! Mnaenda kusalimia mtu mlevi amekesha anakunywa konyagi hapa! Ma-*file* yameisha Ofisini mnaenda...

Mheshimiwa Spika, mimi sioni hata kama tuna sababu ya kufanya uchunguzi. Kama kweli tunataka kuwatendea Watanzania; na unisikilize vizuri wewe ni Mgogo; watu hawa mkiletu mchezo hawaitakii mema Dodoma. Kila saa wana-*brand* kuna majambazi, maana yake wanawatisha watu wasiamini kwamba Dodoma iko salama. Shitukeni Wagogo, hivi hili kweli lingekuwa Mikoa yao hiyo, una *brand* watu vibaya, viongozi wanatekwa; mtu amekesha anakunywa Faru John kule!

Mheshimiwa Spika, Faru John ni ile konyaji kubwa. Halafu anakuja anateleza anasema, Dodoma hakuko salama, wanatengeza *attention* wanakodisha na ndege. Lazima watu wa Dodoma mwaone watu hawa kama ukoma kwenye maendeleo ya Mkoa wa Dodoma. Haiwezekani! Njia ni nyepesi tu, tusitumie nguvu. Yule Daktari aliyempokea pale Ntyuka si upto? Hata kama hakupima, harufu ya Faru John haijui? Harufu ya konyaji? Mnasumbua viongozi wetu, mnaacha ma-file mnaliza ving'ora kwenda kumsalimia mlevi kateguka mguu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hili siyo sawa, ni lazima sisi Wabunge tufike mahali. Kama hii taarifa itatoka kwamba huyu kweli alikuwa ni mlevi, lazima kama Bunge tuseme kitu, vinginevo tunaonekana wote ni wajinga tu humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Bunge lako hili lina wataalam mbalimbali ninaomba wamrudishe Mbewe nimtibu hapa. Akimaliza siku tatu hajatembea mnivue Ubunge. Wamrudishe wasimpeleke Dar es Salaam, nitamtibu mimi kienyeji hapa. Kwani kuteguka mguu watu wangapi wanateguka? Mbona Mheshimiwa Halima Mdee aliteguka hapa na amepona kienyeji!

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri sana...

## TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma mambo mengine kwa sababu ni *serious* wala hayana utani, nikupe tu taarifa muhimu kama ulivyozungumza. Tulienda kule kwa sababu ni mwenzetu, ni binadamu mwenzetu na kadhalika. Halafu baadaye nikatuma Madaktari wangu kwenda kule ili kuzungumza na Madaktari wa kule. Majibu waliyoniletea nikiwa nimekaa hapa hapa ni kwamba ni kweli ndugu yetu alifikishwa kule Mheshimiwa Mbewe kati ya saa nane na tisa usiku na walipompokea alikuwa amelewa chakari. (*Kicheko/Makofii*)

Naomba uendelee na mchango wako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ndiyo maana tunajivuna kuwa na Spika mwerevu na mfuatilaji kama wewe. Sasa vitu kama hivi, watu hawa wamesumbua viongozi wetu leo kuliza ving'ora, ukiachilia mbali ile ya kwenda kusalimia, wame i-brand namna gani Dodoma? Halafu nyie Wagogo humu ndani mnachekacheke, Mkoa unaharibiwa huu!

Mheshimiwa Spika, lazima Polisi tuchukue hatua. Kwani kama ameteguka mguu, apigwe pingu aende huko huko akashughulikiwe kwanza kwa kuharibu *image* ya Mkoa wetu wa Dodoma. Watu wamewekeza hapa, huu ni Mji wa kibiasara kwa sasa. Tukianza kuzungumza haya mambo ya ovyo ovyo tunacheke...

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa taarifa hii. Watanzania hii taarifa waisikie, huyu mtu kaanguka, amelewa Faru John. Mnajua Faru John? Ile konyaji ya kisasa kubwa. Nami nilikuwa nawacheki tu hivi; Polisi wangejichanganya kutoa tarifa za uongo, ndiyo wangetutambua, kwa sababu mimi jana nimewona Mheshimiwa Mbowe saa saba ana Faru John na ninajua alikuwa na nani. Abishe hapa nimitaje aliyekuwa naye. Nawavizia tu.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba kwa vile hiyo ndiyo taarifa imekuja kwenye kiti chako kwamba Mheshimiwa Mbowe alikuwa amelewa, kwa hiyo, ameteleza; wewe kama Mheshimiwa Spika ambaye mhimili wako wako leo unazungumzwa duniani kwamba kuna Mbunge kashambuliwa kumbe mlevi, lazima tuwe na kauli moja ambayo watu wengine walevi kama hawa wasije wakatuchafua hata na sisi Wabunge. Tunaamini Dodoma ni salama hata ukitembea saa nane. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashukuru sana. Niseme tu kwamba kwa kweli tunapongeza sana Mheshimiwa Rais, nami naamini Tanzania ni nchi ya kwanza ambayo *Corona* yenye we inatuogopa. Niwasisitize Waheshimiwa Wabunge, msibweteke. Nyungu zipo, wale mnaohitaji huduma za

nyungu karibuni hata kwangu niwachome nyungu,  
Mheshimiwa Shekilindi ana dawa.

**WABUNGE FULANI:** Mhhh!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Msigune, dawa ipo!

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Musukuma.  
Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa  
David Ernest Silinde, halafu tutarudi kwa mtoa hoja.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika,  
nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kusema machache  
kuhusu Azimio liliioletwa mbele yetu na Mheshimiwa Ester  
Mmasi, Mbunge. Azimio hili linahusu kumpongeza Rais  
Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi  
kubwa aliyolitendea Taifa lake wakati likipita katika mtihani  
mkubwa wa ugonjwa wa *Corona*.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengi  
wamezungumza mambo mazito sana, nami nitajitahidi kadri  
ninavyoweza na ninavyojaliwa na Mungu kuacha  
kurudiarudia maneno waliyoyasema Waheshimiwa Wabunge  
ili nisije kukaharibu ladha. Nataka niseme mambo mapya  
kabisa ambayo hayajazungumzwa humu ndani.

Mheshimiwa Spika, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli  
Mungu amemjalia maono kuanzia muda mrefu.  
Kumbukumbu zangu zinaonyesha, akiwa Waziri, mchakato  
wa kuanzishwa *TANROAD*, gari ya Waziri ilichelewa,  
Mheshimiwa Dkt. Magufuli alipanda *Pick-up* kuwahi kikao na  
watu wa Denmark kujali mchakato wa kuanzishwa *TANROAD*.  
*Pick-up* ile iliendeshwa na Mfugale ambaye leo ndiyo  
Mkurugenzi Mkuu wa *TANROAD*. Unaweza kuona namna huyu  
baba ambavyo Mungu amemjalia maono makubwa. Aliona  
gari la Waziri limechelewa, akamwambia Mfugale lete *Pick-up*,  
akapanda *Pick-up* kuwahi kikao. Leo tunaona maono  
yake namna yanavyolisadia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, cha pili, wakati wa ujenzi wa Daraja la Mkapa, Mheshimiwa Magufuli alipata kero sana ya namna *Kuwait Fund* walivyokuwa wakitoa pesa, akasema siku sijazo tuanze kujenga barabara zetu kwa pesa za ndani. Leo Taifa hili linajenga karibu asilimia zote za barabara kwa kutumia pesa za ndani. Ni maono ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatusimami hapa kumpongeza mtu ambaye hajafanya jambo. Tunampongeza mtu anayetoa *vision* inasaidia nchi miaka na miaka mbele. Leo Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa msimamo wake kuhusu janga la *Corona*; tumeona Kenya watu wakifungiwa ndani, wanakataa na matokeo yake badala ya kufa na *Corona* wanakufa kwa risasi. Mheshimiwa Dkt. Magufuli amekataa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya maono ya kupambana na *Corona* aliyoafanya Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kuunganisha Wakristo na Waislam wote kwa pamoja tumilie Mungu, yameisaidia sana nchi yetu. Tumeona yakiishangaza dunia. Unajua kuna watu walikuwa wanaamini kwamba Ukristo unatoka Italy na Israel; Uislamu unatoka Urabuni. Mheshimiwa Dkt. Magufuli ame-*prove* kwamba siyo kweli. Wakristo na Waislamu wa Watanzania sisi hatusali kwa sababu Mataifa mengine yanásali, sisi tunamwamini Mungu moja kwa moja. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, waje wajifunze imani yetu. Sisi hatusali kwa sababu Kuwait wanasali; hatusali kwa sababu Italy wanasali. Maana nilimwona siku moja Mheshimiwa Mchungaji Msigwa anasema, huko walikoanza dini watu wamefunga, ninyi mnámwamini Mungu gani? Tunamwamini Mungu anayemwamini Rais wetu. Amewaonyesha duniani kwamba jamani yuko Mungu anayeweza kusaidia nchi kwa maombi ya wananchi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, unajua somo lingine jipya alilolitoa Mheshimiwa Dkt. Magufuli, watu wengi wanafikiri tunaweza

tukatumia njia za Ulaya kutatua matatizo yetu kwenye kila jambo. Hapana! Kwa sababu *Corona* imetoka nje, kwa hiyo, tutumie na mfumo wa nje kuitatua? Mheshimiwa Dkt. Magufuli amewaambia hapana, tutaondoa *Corona* kwa kutumia utaratibu wetu wa ndani ya nchi yetu. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa hapa, Dkt. Magufuli ameutetea uhuru wetu kwa vitendo ndugu zangu. Unajua watu wanafikiri kuwa huru ni kuwa na uhuru wa bendera tu, hivi unasemaje uko huru ilhali unapokea maelekezo ya kufungia wananchi wako ndani wan chi nzima na wewe unakubali. Halafu unasema Taifa lako liko huru? Dkt. Magufuli ameutetea uhuru wetu kwa vitendo. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaposimama kumpongeza hapa Mheshimiwa Rais, tunaomba apokee pongezi za Bunge zima la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa matendo makubwa aliyolifanyia Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Dkt. Magufuli kuna kitu cha ziada ambacho Mungu ametufanyia; naomba mkubaliane nami Waheshimiwa Wabunge. Kila mwaka wa mvua, iwe mvua ndogo au kubwa taifa hili huwa linakumbwa na ugonjwa wa cholera wa kipindupindu. Niambieni mwaka huu tumepata kipindupindu wapi? Kwa hiyo lazima muelewe kwamba tunaposema Dkt. Magufuli Mungu amemsimamia tunasema kwa dhati; kwa sababu leo hii na *Corona* halafu kingeingia na kipindupindu hali ingekuwaje? Ingekuwa mbaya zaidi; lakini Mungu akamuepushia akamuambia kwanza *cholera* hakuna halafu na hiyo *Corona* yenyewe naifutia kwa mbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapompongeza Dkt. Magufuli, tunampongeza kwa dhati tukiamini kwa mvua kubwa tuliyopata mwaka huu na ugonjwa wa corona halafu ingeshuka na kipindupindu, toba *Yarrabi!* sijui ingekuwaje. Kwa hiyo pongezi zetu kwa Mheshimiwa Magufuli azipokee, kwamba Bunge zima linachukua fursa hii kumpongeza

Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kutuvusha kwenye janga la corona mpaka sasa hivi tunasonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu jambo lililojitokeza mimi sitaki kusema sana kwa sababu nilikuwa nawasubiri wadanganye. Huko kwenye mitandao wameanza kusema uongo. Nimemsikia Msigwa, nimewasikia wazungumzaji wao, na nimemsikia Katibu Mkuu. Ndiyo maana niliwaambia, hivi ninyi kweli mnamathea Katibu Mkuu Mheshimiwa Mnyika akapambane na Mheshimiwa Bashiru, hivi nyie mna akili nyie? Angalieni *squadya* CCM kule! Wewe mtu kama Mheshimiwa Dkt. Bashiru akapambane na Mheshimiwa Mnyika kuna usalama jamani? Eti kasema Mheshimiwa Mbobe kakanyagwa kwenye ngazi amekanyagwa wakamuambia tuone utafanyaje kampeni mwaka huu! ninyi mnaongea maneno ya kijinga kabisa. Kwa kampeni gani? Mheshimiwa Mbobe amezunguka na helikopta nchi hii kila sehemu, hajawahi kutujeruhi hata kidogo, hiyo kampeni ya mwaka huu Mheshimiwa Mbobe angeendaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Bunge tuitake Serikali ichunguze jambo hili kwa makini. Haiwezekani mtu amepiga masanga yupo bwii anadondoka anakimbia kwenda kwenye hospitali huko ndani kwenda kujificha kwamba eti ooh wamekuja wamenikanya watu watatu. Kumbukeni ndugu zangu alipoumia Tundu Lissu, CHADEMA walisema kuanzia wakati ule wangejilinda wao wenyewe. Ndilo lililokuwa tamko lao, kwamba Viongozi wao watalindwa na wao wenyewe; walinzi wa Mheshimiwa Mbobe walikuwa wapi jana usiku? walinzi wa Mbobe walikuwa wapi Mpaka Mwenyekiti ateleze kwenye ngazi? walikuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, mimi hawa walinzi wa Serikali wala sina sababu nao, lakini CHADEMA waliapa kujilinda. Walisema viongozi wetu wakubwa wote tutawalinda; *green guard* wa CHADEMA wako wapi? Wale *red bridged* wanaita red bridged wako wapi? Wote wako tungi wamepombeka na Mwenyekiti. Sasa wanataka kulipaka matope, wanataka kulipaka matope Bunge letu, waipake matope Dodoma yetu, waipake matope Serikali haiwezekani! Hili jambo tusilichukulie

kwa mzaha. Na ninataka niwaambie, mwaka huu tukijipanga vizuri kikosi cha CCM tunakwenda kuwfutilia kwa mbali hawa watu. Hatuwezi kuwa na upinzani wa uongo uongo kila kukicha wanasema uongo (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hivi nikuulize wakati wote hawa wanasema kwamba, hata mikutano hatutafanya tutakuwa tunazungumza kwa *video call* kwaajili ya kujikinga na corona; saa saba ya usiku Mwenyekiti alikuwa anakwenda wapi na corona bado ipo; alikuwa anaenda wapi? Kwa nini Mwenyekiti atoke saa saba, kulikuwa na kikao gani ambacho video haiwezi kuwaunganisha, kulikuwa na kikao gani? (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, wamewafukuza Wabunge bila kuwaita kwa sababu wangewaambukiza corona, kwa hiyo wakatumlia *video call* Kamati Kuu ya CHADEMA kumaliza tatizo. Jana *video call* zilienda wapi mpaka Mheshimiwa Mbobe atoke saa saba ya usiku, zilienda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania leo hii si wajinga, tunajua tabia ya kila mtu. Na inavyosemekana nyumba za pale zote zina camera Mheshimiwa Mbobe hakuwa peke yake, hakuwa peke yake, hakuwa peke yake! Wakati anateleza hakuwa peke yake. Kwa hiyo sisi tunawasubiri waje hapa waseme uongo tuwalettee picha ya mtu aliyekimbia waliyekuwa na Mwenyekiti, tutawaletea hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wewe unatoka kupombeka saa saba ya usiku, umerudi una kidumu unateleza, badala ya kusema ukweli kwamba jamani mimi nimeteleza eti amekanyagwa na wanaume watatu hivi kweli jamani nyie mnatak akuleta uongo wa ajabu katika taifa hili. Nchi hii nchi huru, nchi hii Viongozi wake wana mapenzi ndiyo maana ukaona Mheshimiwa Spika, ukaenda, Mheshimiwa Waziri Mkuu akaenda, Mheshimiwa Rais akaenda kwa sababu nyinyi mnaongoza taifa, nyinyi ni viongozi wa watu kwa hiyo lazima kila mtu mumkimbilie kwa hiyo mmefanya sahihi.

Mheshimiwa Spika, azimio hili naliunga mkono lakini tunataka majibu ya kutosha kutoka Serikalini na tutaeleza mpaka alipokuwa anakunywa, tutaeleza. Safari hii tupo nao hawa mpaka mwisho, baa funika baa funua mpaka hadi ngoma ieleteke. Asante sana Mwenyekiti. (*Makof/ Vicheko*)

**SPIKA:** Huyo ni Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Anachosema ni kwamba yajayo yanafurahisha. Wanachosema watoke tu halafu sasa mtaona shughuli itakavyokuwa, hapa maana mambo yatafunguka hapa, yasiyoaminika. Mhh nani ameripoti wapi, nani amempeleka nani hospitali. Kwani ukishateguka unajipelea mwenyewe? Yatatoka hapa nyie subirini tu. Mkanda mzima utatoka; lakini mkinyamaza aah lakini mkija hapa na *story story* basi mambo yatakuwa namna hii. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa David Ernest Silinde atafuatiwa na Mtoa hoja. (*Makof/*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makof/*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa ushahidi. Miaka mitano iliyopita tukiwa humu ndani Bungeni sisi Wabunge wa Upinzani ndio tulikuwa tunaongoza kusema nchi hii inapaswa kuongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi tumeyasema na tumenukuliwa kila mahali, kwamba nchi hii akikamata mtu kama Magufuli, akikamata mtu kama Magufuli tutanyooka, tuliyasema sisi wenyewe, na mimi Silinde ni shahidi wa hilo. Niliwahi kumuambia hata Mheshimiwa Rais, nikamuambia Mheshimiwa Rais wewe unastahili kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof/*)

Mheshimiwa Spika, kwa mdomo wangu nikiwa Mbunge wa Upinzani. Sasa leo amekuwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, watu wale wale tunazungumza uongo katika mambo ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi leo tuulizane hapa mmoja baada ya mwininge, Magufuli ana kosa gani, yaani kosa gani ambalo tunaweza tukasema kweli ametukosea Watanzania kosa gani moja tu, kosa gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kosa lake kupambana na corona na dunia imebaki inaduwaa? Ndilo Kosa Lake? Kosa lake ni kujenga *flyovers*? Kosa lake ni kununua ndege? Kosa lake ni vivuko vyta meli huko tunavoona kila mahali? Kosa lake ni kujenga barabara hizo kila mahali? Kosa lake ni kuleta umeme wa Mwalimu Nyerere *Stiglers gorge*? Kosa lake ni nini, ni SGR? Yaani unajiuiliza hivi kosa la huyu mtu ni nini?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli hana kosa isipokuwa sisi Wapinzani ametuzidi hoja, tumeishiwa kabisa. (*Makofi/vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, na ninayasema haya kwa sababu moja, kwenye vikao vyetu vyta ndani tulikuwa tunakiri kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ametumaliza, ni hatari. (*Makofi/vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nimesema nitoe usuhuda kwa sababu ndio ukweli, tukikaa wenyewe tunasema mhahhi! Eee hii mashine imetudhibiti kila kona. Ndiyo maana hata KUB alipotoleza jana usiku wakajua hii ndiyo *angle* ya kuchomokea sasa wamekosea picha, hiyo ndiyo bahati mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hebu jiulize, kifundo cha mguu kinahitaji ndege? Ndege! kifundo cha mguu! Yaani mtu ameumia mguu anataka chata ya kukodiwa kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam! Kama si kufanya drama hapa ni nini? Yaani unafanya sanaa; na Mheshimiwa Spika hapo ungeingia mtego maana yake ungelifanya tukio lione kane kuubwa, wakati kumbe ni kakifundo tu ka mguu. Ukweli unajulikana, huwezi kudanganya, mimi nimekuwa namsikiliza

hapa Mheshimiwa Msigwa anasema Mheshimiwa Mbewe alivamiwa na watu watatu wakamuambia eti tumetumwa kuja kukudhuru.

Mheshimiwa Spika, anayevamia! Eti siku hizi wanatoa taarifa? Eti tumetumwa tukupige kidogo! Jamani! hii nchi kweli imefikia hatua hii jamani?! (*Makofi/vicheko*)

Mheshimiwa Spika, yaani hii nchi watu wamechoka, eti jambazi anasema eti tumetumwa tukupige kidogo, tukudhuru tu kidogo halafu wanachagua kakifundo tu kamguu. Hii nchi ina wakati mgumu sana. Sasa ndio maana mimi nilipopata ile nikasema hivyo pale alipopigwa...

## TAARIFA

**SPIKA:** Kuna taarifa Mheshimiwa Silinde, Katibu tunza muda.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nipo hapa nasikiliza hotuba ya Mheshimiwa Silinde hata mimi Mheshimiwa Mbewe ni jirani yangu sana. Anapokuwa na wageni wake akiburudika, akinywa kila kitu huwa tunasikia. Nimeshangaa kusikia anavamiwa usiku watu walikuwa wanazungumza naye, hatukusikia hayo mazungumzo hata kusikia hicho hata kishindo cha kwamba kuna mtu anavamiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naungana na Mheshimiwa Silinde, hata mimi bado najiuliza kama jirani yake. Kwa sababu kila anachokifanya sisi huwa tunasikia akianza kunywa na rafiki zake, akianza kuwa na sherehe, akiwa na jambo lolote huwa tunasikia. Ndio nilikuwa naungana na mkono wa Mheshimiwa Silinde kwamba hata mimi nashangaa kama jirani yake; na mimi nilichelewa kulala mpaka saa saba nilikuwa sijalala sikusikia jambo hili, Mheshimiwa Silinde endelea. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya hata majirani hawakuwasikia hao majambazi. (*Kicheko*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, taarifa ninaipokea, kwa sababu unajua haya ndio mambo ya kuulizana. Pale pana majrani; mimi nihavyoijua CHADEMA niliyokulia huku, yaani ingetoka hata damu tu kwenye zile ngazi ingepigwa picha hiyo na ingesambazwa Tanzania nzima. Huo ndio ukweli! lakini hatujaona picha ya damu, hatujaona picha ya mguu tumeona tu kwenye muhogo tu unaoneshwa pale lakini sisi tunajua ile ni sanaa; ni changa la macho!

Mheshimiwa Spika, hatusemi kwa sababu tunamchukia Mheshimiwa Mbowe. Tunasema kwa sababu taifa hili haliwezi kuendeshwa na dhana ya uongo kila wakati, haiwezekani; dhana ya uongo kila wakati, dhana ya kuombeana mabaya kila wakati ni dhana ya hovyo kabisa, nchi zote. (*Makofivigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge la Afrika ambako nimekuwa Mbunge kwa kipindi cha miaka mitano, yaani kila unapopita, kila Wabunge wa nchi wanasesma tunatamani Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli awe Rais wetu. Kila nchi Kenya wanasesma, Uganda wanasesma, kila nchi wanakuambia *you have the President, that is a real African President.* Wana-appreciate mimi kule nipo upinzani mpaka najisikia aibu. Sasa kama watu wa dunia nydingine wana-appreciate mchango mkubwa anaoutoa Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli halafu sisi tuko huku ndani, tunahakikisha tunamkwamisha kila kitu; haiwezekani, taifa hili haiwezekani kila mtu akawa Rais haiwezekani, hata tungepewa kila mmoja siku moja awe Rais wa nchi haiwezekani. Lazima atokee mtu mmoja atupeleke mbele, tusogee. Na aina hii ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ilipaswa iendelee kwa miaka 20 mbele; kwa aina hii ya uongozi,. (*Makofivigelegele*)

Mheshimiwa Spika, haya ndio ya ukweli lakini watu watabisha. Ninyi nyote mliona na mlikuwa ni mashahidi. Kuna Waheshimiwa Wabunge hapa walikuwa wanaombea Wabunge wafe kwa corona ili Mheshimiwa Spika aahirishe Bunge, tuahirishe walau uchaguzi mwaka mmoja. Yaani lengo tu hapo tulikuwa tunaona tumeishiwa hoja, kwa hiyo

namna gani ya kuwa-*fix* mmekuwa wajanja nyinyi mwaka huu aisee mmetuzidi kweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumewa-*fix* vizuri, lakini ulikwepa ule mtego. Lakini watu ambao ndio unasema tu watu wasiokuwa na nia njema. Na kiukweli sisi kwenye makundi yetu tuliambiana kule, jamani hii hoja haina mashiko, Mheshimiwa Mwenyekiti hoja haina mashiko hii. Tutaonekana watu wabaya, Makamanda hawakimbii mapambano. Sasa sisi wenyewe ndio tunajiita Makamanda tunavaa na Kombati, tunaenda kujificha hotelini, hao ni Makamanda au ni Mgambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa haya tunayasema kwa sababu tunaona hili taifa linapoelekea tukiendelea kuacha dhana ya uongo inatawala maana yake tunaendelea kujenga mpasuko ambao mwisho wa siku tunaweza tukagawanyika. Hebu wewe fikiria una mtu anakaa, anautangazia Umma anaomba kabisa naomba Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli afe. Sasa mtu wa namna hiyo haiwezekani hata siku moja haiwezekani hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana wewe mtu kama Mheshimiwa Lema anatangazia Umma eti Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli afe. Unaona mtu ana nia njema? Ndoto eti, ndoto yangu nimeoteshwa afe; kabisa, unaona kabisa mnajenga upinzani au mnabomoa nchi. Unaomba wananchi wafe kwa corona ili taifa lisitawalike na CCM sijui Serikali ianguke. Unaona kabisa mnajenga Upinzani au mnabomoa nchi? Sasa haya ndio mambo ambayo sisi tunasema hapana *enough is enough*; kama sanaa inatosha. Ifike mahali tuwe wa kweli. Tulikuja hapa watu tulijua tunatengeneza mawazo mbadala ili Serikali ikishindwa kuteleza mawazo mbadala watu wachague mawazo ambayo yapo sahihi. Sasa si mawazo mbadala ni kupinga.

Mheshimiwa Spika, tulisema hayo! mnakumbuka hotuba zetu za miaka mitano, tulisema nchi hii inatia aibu haina ndege. Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli akaleta ndege, tukasema ndege gani watu wanataka maji eeeh! Haya! maji

yenewe vile vile ameleta, miradi ya kutosha ikiwemo Jimbo langu la Momba. Sasa hoja gani tena? Nchi haina Umeme wa kutosha ikaja umeme wa Mwalimu Nyerere. Haya sasa Hoja gani, ooh sasa hatuna reli, reli imekufa ooo rerere! SGR hii hapa sasa tunafanyaje, sasa tunakwendaje! Jamaa anajibu kila hoja na anajibu kwa vitendo. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, sasa mtu wa namna hiyo unaachaje kumuunga mkono, mtu wa namna hiyo unaachaje? Mtu mwenye akili timamu kabisa mwenye kufikiri unaachaje kumuunga mkono mtu wa namna hiyo? Kwasababu jukumu letu ni moja tu, ni kusogeza huduma kwa wananchi kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, na ukweli, ingelikuwa sisi wapinzani tunaomba kura kule kwa wananchi tunasema mimi ukinichagua nitaenda kupinga kila kitu asingerudi mtu! Asingerudi mtu humu ndani. Na sisi tukifika kule tunadandia kwenye hoja hizi hizi za Serikali! ni mimi hapa nimefanya! haya maji ni mimi! lakini unajua kabisa yale maji ya Kitete pale si mimi ni Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ndiye aliyeayaleta. Amefanya Serikali ya CCM imefanya kiukweli mmeefanya mambo makubwa ambayo mnapaswa kupongezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini hata Manabii wote huwa hawakubaliki, hiyo ipo. Ukiangalia Mtume Muhamad alipingwa sana alipokuwa anaeneza imani yake. Nabii Issa ambaye sisi kwetu Wakristo Yesu Kristo alipingwa sana alipokuwa anaeneza Ukristo, mpaka akapelekwa msalabani akanyongwa na watu wale wale aliokuwa anawahubiria habari njema; wakamsulubu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tabia ya mwanadamu anafikiri na yeze anaweza, we imagine eti mtu anataka eti Mheshimiwa Msigwa kuwa President, eti Mheshimiwa Msigwa wa ku-*compare* na Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli jamani. Huu si mzaha huu! Yaani unaona kabisa kwamba Chama kweli kimepoteza mwelekeo; eti Mheshimiwa *Msigwa for President; Msigwa for President?* wa kupambana na

Mheshimiwa Dkt. Magufuli yule jamanil! Elimu yake tu yenyewe changa la macho sasa anaweza kupambana na Rais pale. (*Makof/vicheko/vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, yaani unabaki unaona kabisa watu hawa wamepoteza muelekeo, hawana dira, yaani ni vurugu mechii.

Mheshimiwa Spika, na siku zote sisi tumekuwa tukiwaambia hatuna nia ya kuona Upinzani unakufa nchi hii hatuna nia hiyo. Tunataka kuwa na mawazo mbadala, watu sahihi watakaosaidiana na Serikali ya wakati huo iliyopo madarakani, kuhakikisha nchi inakwenda mbele. Lakini hatupo tayari kuona Upinzani unaoshirikiana na hao watu wengine kubomoa hii nchi, hiyo kitu haiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani na ndiyo maana nimesema kwenye hili, kwenye janga la corona wakatijanga linaanza kutokea kuna rafiki yangu alinitumia kitabu anaitwa Atul. Kinaitwa *surviving the crisis*; kile kitabu kinasema wakati wa majanga yanapotokea kunakuwepo na *losers* panakuwepo na *winners*. Yaani washindi na wanaoshindwa, siku zote kwenye majanga. Kwenye hili janga wakati wa majanga makubwa kama ya corona mara nydingi huwa dunia ama watu walio wengi kunakuwa na *group thinking*, yaani mtazamo wa ujumla, yaani watu wote mnataka kuelekea upande mmoja. Yaani mtu akisema dawa ya corona ni mawe wote mnakimbilia kule kwa sababu wote mna ndiyo *thinking*. Sasa wale ambaeo huwa wanageuka kuwa washindi ni wale wanaofikiri tofauti na wengine, jambo hilo ndilo alilolifanya Rais, Mheshimiwa Rais Magufuli.

Mheshimiwa Spika, nahiki ndio maana uliona haya hatutaki kuyaingilia ya mipakani ilikuwa ni kwasababu alikuwa anaharibu siasa za nchi nydingine, watu wanaauliza mbona Tanzania wanaendelea na maisha, uchumi wao wanaendelea, kila kitu kinafanyika kwa nini sisi huku mlikuwa mnaua siasa ya Kenya, mlikuwa mnaumiza siasa ya Uganda, mlikuwa mnaumiza siasa ya Rwanda, mlikuwa mnaumiza siasa ya maeneo mengine huo ndio ukweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima mtengeneze *Cartel* na tum-fix na yeye kwasababu anatuharibia ehe! Chuma kikasimama hivi mwanzo mwisho, leo wote ni mashuhuda kwamba kihali halisi Corona ni kama imekwisha kwasababu Waziri Mkuu wa Ufaransa alisema Corona *is the mindset disease* yaani ni ugonjwa amba o kwenye akili zetu, huu ugonjwa ndio umeshaingia utakuwepo miaka nenda rudi hautakwisha, kwa hiyo, tukubaliane kuishi kuendanao yaani tuishi kama ulivyo. Kwa hiyo, na sisi tutaendelea kupambana nao mpaka pale ambapo dawa itapatikana ile dawa yao ya wazungu lakini dawa zetu sisi zinaendelea kufanya kazi nyungu pamoja na vitu vingine. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niliona niliseme hili kwasababu nimeridhishwa na Uongozi wa Mheshimiwa Rais, nimeridhishwa na Uongozi wa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa, nimeridhishwa na Uongozi wako kitu chako umekuwa imara pamoja na kwamba tumekutikisa sana kwenye miaka mitano, nimeridhishwa na uimara wa Chama Cha Mapinduzi kwamba ni Chama imara. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwasababu moja CCM ni Chama cha watu wote akijali ni nani anatoka wapi anakwenda wapi ni chama cha watu wote. Lakini sisi CCM ni Taasisi imara na ndio maana katika Afrika Taasisi namba moja imara ni Chama Cha Mapinduzi kitu kipekee ambacho nakipenda sana kwenye CCM ni uwezo wa kujisahihisha chenyewe kama chama kama Taasisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa unapokuwa na Taasisi inayoukuza vijana unaona viongozi wazuri wanapua inayosikilizana inaadhibu viongozi kwa utaratibu, wee fikiria mwanangu alikuwa anaumwa hospitali Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ali-take charge mwanzo mwisho, watoto wangu wakati wanazaliwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ali-take charge mwanzo mwisho nikiwa Mbunge wa Upinzani kama mpinzani ndio maana hata leo Mheshimiwa Mboge ameteleza lakini umeona wako pale yaani umemuona Mheshimiwa Rais,

umemuona Mheshimiwa Waziri Mkuu, umemuona Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbewe tu ameteleza yaani kuteleza tu Serikali yote imeshuka pale. Hebu wewe unataka watu wakupende kiasi gani yaani wakupende namna gani kukuonyesha kwamba tunakupenda lakini majibu mtayapata mataishia kutukanwa tu na kudharaurika nyie chapeni kazi komaeni kwasababu ndio wajibu wenu kujenga hili Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nisingependa kuendelea na dhana ya kudanganya watu na uzuri Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alisema yale ya kumsingizia Mheshimiwa Kinana akakiri ndio imekuwa tabia yetu muda mwiningi, uongozi hata hii ni uongo tu mwisho wa siku tutakuja tu jamani mtusamehe ilibidi ndio tupate kiki ya kutokea sasa hata kiki yenye we ime-*bounce* watakiri tu mtasikia mwisho wa siku. Haya yote dhana hili sasa baada ya kutafakari kwa muda mrefu nilichukua mwezi mmoja nikajiridhisha kabisa kwa nafsi yangu kwamba ninastahili kuomba kuwa mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi/Vigelegelé*)

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, umepata, umepata!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, najua wewe ni mjambe wa Kamati Kuu Mheshimiwa Waziri Mkuu najua ni mjambe wa Kamati kuu ya Chama Cha Mapinduzi na wajumbe wengine wa Kamati Kuu ambao ni Wabunge kwa nafasi zao kwa sasa.

Ninawaomba kwa mikono miwili niko tayari kikitumikia Chama Cha Mapinduzi kwa nguvu zangu zote nguvu ninayo, uwezo ninao na bahati nzuri hao watu nawajua nje ndani nitakwenda kuwaeleza Watanzania

uwongo umeendelea na tutahakikisha Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli anaendelea kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno nashukuru sana na ninaunga azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwamba yeye ni Jemedari kwenye haya mapambano Mwenyezi Mungu ambariki sana ahsante sana. (*Makofii/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde, sasa kwa taratibu za Kibunge kwa hotuba uliyoitao unatakiwa sasa usikae huko unyanyuke utembee umpe mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu ...

**MHE. JOSEPH MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, namkaribisha hapa Mheshimiwa Silinde.

**SPIKA:** ...halafu *Chief Whip* atakuonyesha mahali pa kukaa kwa muda, kwa hiyo, karibu uanze kuelekea.

*(Hapa Mhe. David E. Silinde alihama upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kuelekea upande wa Chama cha Mapinduzi kcaa)*

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM!

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi saidia mahali kiti gani akae Mheshimiwa Silinde ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kilichofanyika sasa si utani ndio taratibu zetu naomba make basi ndio taratibu zetu inaitwa *crossing the line* ehee! Unatoka upande ule una *cross* moja kwa moja hadharani kweupe na hii ndio njia nzuri zaidi ningependa kuwa-*encourage* Wabunge wote kuitumia tunakoelekea.

Sasa kabla sijamuita Mheshimiwa Ester Mmasi, Mheshimiwa Lwakatare pia ni jirani pale kwa dakika moja tu mzee ahaa sio kwa maana ya zoezi hili kule kwenye makazi kule, jirani wa Mheshimiwa au sio mmoja wapo wa majirani pale maana Mheshimiwa Makilagi Mheshimiwa Kitwanga

ndio jirani, Mheshimiwa Kitwanga ukusikia chochote usiku huo tafadhali. (*Makofi/Kiceheko/Vigelegele*)

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, mlango wa Mheshimiwa Mbewe na mlango wangu unafanana kabisa, kwa swali uliloniuliza sijasikia.

**SPIKA:** Una maana milango inatizamana!

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, inafanana naomba niseme hivi inafanana nyumba anayokaa Mheshimiwa Mbewe na nyumba ninayokaa mimi ni *floormoja* ni zile zile ni ma-*flat* yanayopakana. Mimi sijasikia vurugu yoyote na kwa utamaduni wangu saa nane huwa naamka kusali. Sasa wakati nasali sijasikia chochote na kwa bahati nzuri nikiamka asubuhi kwenda kufanya mazoezi nikipita pale huwa naona walinzi wa Mheshimiwa Mbewe na walikuwepo sasa sijui hayo mengine mimi naomba nadhani Serikali ifanye tu tupewe maelezo yanayostahili lakini...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma taarifa

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Kitwanga amesema taratibu zake saa nane huwa anafanyaje sijaikia vizuri. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kitwanga malizia kwa dakika moja. (*Kicheko*)

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, naamini usiku wa manane usiku ukiwa umetulia ni wakati mzuri sana wa kuwasiliana na Mwenyezi Mungu. Hapana kelele wala mkwaruzo uliotokea na niliendelea na Ibada yangu mpaka saa tisa nilipoenda kitandani tena. Na nichomekee

kidogo tu nampongeza sana Mheshimiwa Rais, ni Rais mwenye *vision* ni Rais anayeona mbali sana nimeshangaa leo Mheshimiwa Lusinde ameyafahamuje haya ambayo hata inawezekana siyafahamu. Lakini ni jirani yangu alininong'oneza, lakini Mheshimiwa Rais ni mcha Mungu. Mheshimiwa Rais huyu anaipenda *nchi* yake, Mheshimiwa Rais huyu anapenda *resources* za *nchi* yake zifaidiwe na wananchi wa *nchi* yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uliofanya kumsaidia jana ulijificha sasa nikasema daa jana nilikuwa nikupige kidogo kidongo kwasababu nikasema jamani Mgogo gani ana akili namna hii, sasa kwasababu hukuwepo na hilo nalichomekea nalo kweli una akili umefanya basi ahsante nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitwanga na nakushukuru sana kwa azimio la jana nilikuwa Kongwa nakushukuru sana, ahsante sana Mungu ni mwema. Mheshimiwa Ester Mmasi sasa uhitimishe tufanye dakika 15.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, nina heshima ya pekee kusimama katika Bunge lako hili Tukufu haswa...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee kupiga kura wale ambao hatujapiga kura.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, nina simama kulishukuru Bunge lako Tukufu lakini pia ninasimama kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kutoka vyama mbalimbali ninatambua mchango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi. Lakini pia ninatambua mchango lakini pia kuungwa hoja na upande wa CHADEMA ambapo Makamo Mwenyekiti wa BAVICHA mtakumbuka na tuliona mpaka kwenye *TBC* akiwa na maono haya alisimama na akampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuja na *approach* ya kuweza kulikomboa Taifa kutoka kwenye janga hili la *Covid-19*.

Mheshimiwa Spika, na azimio hili lilisomwa na ndugu Mheshimiwa Mwaifunga Hawa akiwa Tabora, kwa hiyo, tunasema ahsanteni sana pamoja na kwamba mpo tumepokea michango yenu. Lakini tunawashukuru upande wa CUF wameongea vizuri sana wamempungeza Mheshimiwa Rais na kwa namna ya pekee nimetambua michango yote ya Mheshimiwa Lijualikali lakini mchango mzuri kabisa na wa kipekee wa Mheshimiwa Keissy na niseme tu tunavyoteta hapa kwa karibu Waheshimiwa Wabunge wengi wametamani azimio hili tulichangie hata kwa siku tatu ni kiu ya kila mmoja tukeshe na azimio hili tulitendee haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe mwenyewe kwa kuona tija na umuhimu wa kuja na azimio hili la kumpungeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amesimama namna ambavyo alijizatiti na kulingoza Taifa hatimaye tumeelekea sasa kuvuka vizuri kabisa kwenye kadhia au changamoto hii ya *Covid-19*. Mheshimiwa Rais tunasimama tukikupongeza lakini tunasimama tukikushukuru ni dhahiri umetoa darasa kwa Tanzania lakini umetoa darasa kubwa kwa Afrika, umetoa darasa kubwa duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa haya uliyoayatenda Tanzania kwa mwongozo uliotupatia kwa nchi yako ya Tanzania ni dhahiri Tanzania itakukumbuka Afrika itakukumbuka na dunia itakukumbuka, umekuwa mwalimu kwa fani yako wewe ni mwalimu tunafahamu lakini umekuwa mwalimu katika kadhia ambayo wanasyansi na wabobezi wa afya kutoka nchi mbalimbali walifika mahali wakaingia kwenye mkato wa tamaa. Tunafahamu nchi ya Italy walismama wakasema walikiri kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ulisimama kututoa hofu na imeonekana kwa Waheshimiwa Wabunge walio wengi zaidi ya asilimia 9 wamekiri na sote tunafahamu hofu ni zaidi ya tiba, hofu ni adui wa haki, hofu itaweza kukunyima hata haki ya kuishi. Mheshimiwa Rais tunasimama tukisema ahsante sana. Naongea kama Mheshimiwa Ester, siku moja nilipopata taarifa hii ya mpendwa wetu

Mheshimiwa Ndassa nikawa natoka nje hivi nikakutana na Mheshimiwa Heche akaniambia wewe Mheshimiwa Mmasi wewe mnakuwa viherehere kushangilia Bunge lisifungwe tena wewe ndio ulikuwa unakaa na Mheshimiwa Ndassa pale wewe ngoja tuone.

Mheshimiwa Spika, nilitoka kesho yake baada ya kusikiliza yale maneno nilienda Sant Camilius nilienda pale nilikuwa na presha 190 chini 126 sijui sijielewi hofu imenitenda natetemeka saa zote natapika saa zote, nilikuwa mtu wa hofu siwezi kuongea, nilipata kitu ambacho siwezi ku-*express* kwenye bunge lako hili. Anafahamu msaidizi wako Joshua nilimwambia kwamba nafika mahali nashindwa ku-*handle* kwasababu ya hofu nakiri watu wengi walipoteza maisha kwasababu ya hofu, Mheshimiwa Rais tunakushukuru umeanua matanga na misiba majumbani mwetu, umetupa tiba ambayo imefanyika ni mkombozi kwa Taifa hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais tunakushukuru, lakini Mheshimiwa Spika nakushukuru zaidi, nilikuja ofisini kwako nikaongea sana na wewe nikamwambia hapana nilikuwa nafikiri pamoja na kwamba umetusaidia *sanitizerna* nini tusaidie na *mask* ile yote ilikuwa ni mihangaino ya hofu lakini ukaniambia Mheshimiwa Mmasi sikiliza pamoja na haya yote Mungu wetu ni mkubwa hebu tumwangalie Mheshimiwa Rais lazima tumalize kikao cha Bunge lazima tuwatendee Watanzania haki kwa kupitisha Bajeti, tunakushukuru sana kwa kufanyika daraja imara ahsante sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwasababu walim-enter *tight* kwa mikopo lakini hakuchukua ninapoongea hapa haijawahi kusikika mahali kokote mtumishi wa Umma amepokea mshahara zaidi ya tarehe 25 kwa mwezi husika watumishi wote wa umma walipata mshahara kwa tarehe 21, 22 mwisho ilikuwa ni 23, hii ni historia ambayo imeandikwa na hakuna wa kuifuta kwa Tanzania yetu, Mheshimiwa Rais tunakushukuru. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais umefanyika darasa na umefanyika na shule ninapoongea hapa juzi

tarehe 01 mwezi wa 06 ulisema kwamba tufungue Vyuo Vikuu kwamba pambazuko limefika tufungue Vyuo Vikuu tunakushukuru kwamba haukufungua kwa maneno au kwa kauli wala kwa maelekezo lakini ulipoongea tu ndani ya siku tatu, nne Bodi ya Mkopo walihakikisha wametoa shilingi bilioni 122, bilioni 63 ikiwa ni *meals and accommodation* na bilioni 56 ikiwa ni *tuition fee*, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi mimi nilikuwa ni Mbunge ambaye nilisimama hapa nikaongea pengine hata maneno ya kuudhi Bugando niliwasemea nikasema hata na St. Joseph nafikiri kuna mahali labda niliwaudhi lakini nia ilikuwa tufike hapa kwasababu tunafahamu wapo walimu wengi ambao kwenye Taasisi binafsi kwenye Vyuo binafsi walikuwa wanakosa mishahara na ile ilikuwa inaleta tataruki lakini nia ilikuwa tufike hapa tulipofika, kwa hiyo, nawaomba radhi kwa watu ambao nilichangia kwa kuwagusa kwenye maeneo ambayo tulikuwa nia yetu *spirit* yetu tuone mambo haya yanatembea tunakushukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninapoongea hapa, jana kupitia BBC, South Africa wamefungua Vyuo Vikuu jana imetangazwa. Mheshimiwa Rais umefanyika darasa, umefanyika Mwalimu kwa Afrika. Tunakushukuru sana, umetoa mwanga, umetuheshimisha nyumbani, umetuheshimisha katika Nchi za wenzetu, pokea shukurani zetu.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta uhalali ama uhakika wa vifaatiba vile walikuwa wanaita *test kits*, Mheshimiwa Rais wka utashi wake lakini pia kwa nguvu na karisma ambayo Mungu alimjaalia alienda beyond, elienda extra miles kutaka kupata *accuracyya* vile vifaa vya kupima na baada ya majibu yale kutoka alitangaza akawa mkweli tu akasema lakini tukaambiwa *it was unethical*/kwamba ku-test na kuambiwa pia *it was rational decision* lakini kama ile inge-stand au kama ile kweli yale maneno tuliyopewa na wenzetu hawa yalipaswa ku-stand tusingesikia nchi ya India wana-withdraw vifaa tiba, tusingesikia nchi ya Spain wamekataa vifaatiba vya China, tusingesikia Nchi ya France

walirudisha misaada ya China, tusingesikia India nao pia walikataa na waligomea vifaa hivi wakisema kwamba havina uhalali lakini pia vina mapungufu ya kiufundi.

Mheshimiwa Spika, ninasimama kumshukuru Mheshimiwa Rais, leo Esther nikiulizwa ama nikiwa naongea na wajukuu zangu nawahadithia niliwahi kubahatika kuwa Mbunge sidhani kama nitaongea neno zaidi ya hili. Nitasema kweli niliwahi kuwa Mbunge kipindi cha Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Sitarajii kama nitakuwa na utambulisho mwngine wowote ule. (*Makof/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais vijana wako tunajivunia kufanyakazi na wewe. Tumepata darasa la miaka mitano, imekuwa kama ni darasa la miaka 50 kwetu. Sisi tunajivunia kubahatika kufanyakazi na wewe, Taifa linajivunia kuwa na kiongozi kama wewe, pokea shukurani zetu za dhati.

Mheshimiwa Rais umetushika mkono ukatupitisha kwenye njia ambayo hatukutarajia kupita, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Rais ulivaa viatu vya Makasisi, ulivaa viatu vya Masheikh, ulivaa viatu vya Taasisi zote za dini ukasimama ukawa ni muhubiri, ukasimama ukawa ni Mtu wa kutoa *encouragement*, ulisimama, hatuwezi kusema. Ikiwa ni kuongea tu tutahitaji hata wiki nzima tukuongelee mazuri uliyotufanyia. (*Makof*)

Mheshimiwa Rais pokea shukurani zetu za dhati na kwa maana hii ninasimama kupokea au kukubaliana na michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliounga hoja hii mkono, waliunga Azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa namna ambavyo alivyoliongoza Taifa katika mapambano dhidi ya janga la ugonjwa wa corona yaani covid 19.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, ahsante sana. Nawapongeza wote, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri

Mkuu kama kwenye Azimio tulivyogusa, ninampongeza kwa dhati na tunakushukuru Mheshimiwa Rais kwa kumtambua Dada yetu Mpendwa Ummy kwa namna alivyosimama kama Mwanamke, alivyosimama kama kiongozi, tunakushukuru sana. Tumevuna mengi kwako, tumejifunza mengi kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja llitolewa iamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono *overwhelmingly* kabisa kabisa kabisa. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Na Dkt. Sware kasimama.

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Hoja hii ilikuwa ni yaAzimio la Bunge la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa namna alivyoliongoza Taifa katika mapambano dhidi ya janga la ugonjwa wa corona Covid-19. Kura zimeshapigwa na ninayo matokeo hapa ya moja kwa moja. Kura zote zilizopigwa zote zimeafiki Azimio hili. (*Makofi/Vigelegele*)

Kwa hiyo, ni Aazimio rasmi ambalo tunampongeza Kiongozi wetu, Rais wetu kwa kusimama imara, ulikuwa ni mtihani. Siyo mitihani ambao umepita, bado upo lakini tumevuka kipindi kile ambacho kilikuwa cha giza nene sasa inaelekea kupambazuka lakini kiongozi wetu Mkuu, Rais wetu kwa kweli alisimama, huo ndiyo ukweli. Hata sisi wengine

tulikuwa tunapata nguvu baada ya kuangalia msimamao wake na kuona jinsi alivyosimama. Angeyumba, angetereka sisi wote tungetetereka na sababu kubwa ni kwamba, kwa mfano; sisi Bunge tulitikiswa lakini msimamao wake, imani yake, utiaji koyo wake hakika una nguvu fulani siyokuwa ya kawaida kabisa. (*Makofi*)

Si nguvu ya Mwanadamu ya kawaida, lazima ina mibaraka fulani siyo rahisi katika jaribu kama hili la corona na jinsi liliivyokuja tena jaribu lenyewe la Dunia wala halikuwa la Tanzania peke yake halafu ukasimama wima, naamini ni nguvu ya Mungu. Na maajabu ya kiongozi wetu huyu ni mengi; kwa mfano; hivi katika Nchi hii ya Tanzania hii acha sasa lakini nyuma kidogo lakini hata sasa unaweza ukapata Ubalozi wa nyumba 10 bila hata Kibuku kidogo angalau watu wakapata kidogo, *is it possible?* Ukawa Mwenyekiti wa Kitongoji billa hata watu wakapata Kilauri kidogo inawezekana? Ni ngumu sana, ni ngumu sana bila hata kukatakata kidogo ni ngumu sana.

Nani asimame katika Tanzania hii ambae Mheshimiwa Magufuli katika kwenda kuwa Rais, kwenda kuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi alihongwa shilingi moja? Huwezi kuwaza tu hivi inawezekanaje. CCM ile tunayoifahamu sisi ile acha hii na wakati huo huo unashindana wewe ambaye hutoi hata shilingi unashindana na watu ambao wamekata mafungu ya uhakika. Ni nguvu ya Mungu yaani haiwezekani katika akili ya kawiada ya mwanadamu. Ni mpango tu wa Mungu kwamba Bwana hii njia inakwenda hivi, inakwenda hivi, inakwenda hivi na ukiacha sisi wanasiasa wakubwa kidogo na nini, wananchi wa kawaida kule walikuwa wanasema. Kule Vijijini ukiwakuta wale wenye wanakwambia hapa Bwana ukituletea Magufuli tunadhani hapa huyu atanyoosha nchi maana tulikuwa tumekubaliana kwamba wakati ule tulikuwa tumechanganyikiwa Watanzania. (*Makofi*)

Kule Kongwa Wazee wakawa wananiambia Mheshimiwa unajua sijui mtatuletea Kiongozi gani lakini wakaniambia sisi vingozi tumechoka, nisikilize vizuri hapo

wananchi wa kawaida hao wanasem. Wanasem viongozi tumeshakuw anao sasa tumechoka sisi tunakata mtawala. Tunataka Mtu aje nchi hii atawale yaani. Mhajua kuna tofauti ya Kiongozi na mtawala. Awe Kiongozi sawa lakini atawale, viongozi tumechoka sasa ili nchi inyooke maana mtawala akisema amesema na ndiyo maana mtawala.

Na kwa kweli tuendelee kumuombea Rais wetu, tunendelee kumtia moyo na Azimio hili naamini Mheshimiwa Rais atalipokea kwa mikono miwili kwa kweli Wabunge hwawa wamejadili kwa miyo yao, waliyoyasema ni yao kabisa na wamesema ya moyoni leo. Hata alilosema Mheshimiwa Mzee Keissy hatanii, hata sisi hatutanii, tuombe Mungu tu turudi hapa salama tutakubali wenyewe. Maana viongozi hawa hawapatikani kila Jumapili, kila Ijumaa, kila Jumamosi, kila Juma ngapi, *once and while* mkimpata mshikilieni awasogeye mbele kidogo. (*Makof*)

Ndiyo maana Mheshimiwa Keissy akasema tutafika mahali atake asitake tutamwambia Mzee unakaa kwenye kiti hiki twende sisi tuko nyuma yako twende mbele, nchi hii sionge mbele vinginevyo sisi Watanzania tunajuana tutaanza tena mambo yetu halafu tutajuta tena na kuja kurekebisha hilo kosa vizazi na vizazi. Najua wengine wakisikia maneno haya dah, wenyе nia zao wanana kwele kwele. Nchi hii Rais anakuwaga mmoja tu kama umefanya hesabu *probability* ya kuwa wewe unayewaza hayo ni ndogo sana, hesabu ya *probability*. Kwa hiyo, kwa hesabu inapokuwa ndogo namna hiyo si bora uache tu aliyepo aendelee basi na wewe Mwenyezi Mungu alipokujaalia hapo basi yatosha Inshallah!

Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge binafsi yangu nimefarijika sana kwa Azimio hili la kumpongeza Rais wetu sasa hapo maana yake na wasaidizi wake wote. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuwa Mwenyekiti wa Kamati maalum ile, Mheshimiwa Ummy pole sana sijui hata familia ilikuwa inakuona saa ngapi lakini unastahili, umejitahidi sana na wasaidizi wako wote, watumishi wote wa sekta ya afya umejitahidi sana, sana na sekta nyingine zote Watanzania tulishikana na tuendelee kushikana

namna hiyo, tuendelee kupambana na janga hili, siyo kwamba limepita tuendelee kuchukua tahadhari, Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi lakini kubwa kuliko yote tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kulilinda Taifa hili kwa vile imeandikwa ulinzi wa mwanadamu ni kukesha bure, ulinzi wa Mwenyezi Mungu ndiyo ulinzi wenye kabisa wa haki na wa uhakika. (*Makof*)

Basi baada ya maneno hayo naomba sasa nitoe matangazo machache ili tuweze kuahirihs shughuli zetu hadi siku inayofuata.

Natoa wito tena kwa Wabunge wote kokote kule waliko Nchini kurudi Dodoma. Kesho tuna Muswada ule wa Sheria mbalimbali namba ngapi ule tutaupoitia kesho, *miscellaneous amendments*. Baada ya kesho ambayo kesho ni Jumatano, keshokutwa siku ya Alhamisi tutaanza Bunge asubuhi saa tatu ratiba hii ya saa nane itabadiika kesho ndiyo mwisho wa ratiba ya saa nane. Tutaanza Saa tatu lakini siyo kwa utaratibu wa maswali wala nini ni kwamba hiyo siku ya Alhamisi tutaanza na hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu mipango ya Nchi na Saa kumi jioni Mheshimiwa Waziri wa Fedha atatoa hotuba, asubuhi Mpango na mchana Waziri wa Fedha atatoa hotuba ya Bajeti keshokutwa siku ya Alhamisi. Na ndiyo maana nasema Waheshimiwa Wabunge warudi, Ijumaa tutaanza Bunge Saa tatu asubuhi, Ijumaa keshokutwa hiyo tutakwenda mpaka saa saba halafu tutarudi hapa kwenye saa kumi na tutakwenda mpaka saa mbili usiku, mjadala. Tunaamini tutapata Wabunge wengi, tutakuwa tunawakumbusha kadri muda unavyokwenda saa hizi nawapa tu ile picha.

Jumamosi tutaanza saa tatu mpaka saa nane mchana. Naamini tutakuwa tumeppata wachangiaji karibu wote wa Bajeti kwa siku ya Ijumaa na Jumamosi. Siku ya JUmapili wanaokwenda ibada Jumapili watakwenda lakini tutawaomba Saa nane mchana Waheshimiwa Wabunge wote, Waheshimiwa Waziri tukutane kule Kikombo kule ambako tumekuwa tukijenga shule yetu ya Sekondari ile ambayo tulikuwa tunaongozwa na wenzetu wa TWPG saa

nane mchana Kikombo kwenye Bunge girls high school. Bunge hili ndiyo Bunge peke yake toka uhuru ambalo limejenga Taasisi ya aina hiyo siyo kwa fedha za Bunge, kwa michango yenu Wabunge na michango ya wadau siyo kwa fedha za Serikali. (*Makofi/Vigelegele*)

Tumejenga shule, wale wanaotudharau wafike Jumapili saa nane mchana ambao kila wakikaa kazi yao kusema Bunge hili ndiyo la hovyo kuliko Mabunge yoyote watuambie huko walifanya hiyo? Twendeni mkaone Jumapili saa nane. (*Makofi/Vigelegele*)

Na kule kila Mbunge atapata nafasi ya kupanda mti...

**MBUNGE FULANI:** Wacha

**SPIKA:** Kwa hiyo tufike wote na Katibu wa Bunge Watumishi wa Bunge wote pia kila Mtumishi atapata sehemu ya kupanda mti kwa hiyo na sisi Wabunge wote twende kule...

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Tutapanda mti.

**SPIKA:** Ambapo tutakabishi Serikalini shule na Profesa nakuomba ratiba hiyo uitunze kabisa tuwe pamoja na Waziri wa TAMISEMI pia nae arudi huko aliko maana nimeshasema watu wote warudi ili na yeye JUmapili tukukabidhini shule na Jumatatu asubuhi atahitimisha hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na tutapiga kura Jumatatu ya Mbunge mmoja mmoja na siku hiyo itakuwa na ratiba nedefu. Tunaweza tukaenda Jumatatu hata mpaka saa tatu au saa nane usiku ikibidi lakini sidhani kama itafika huko nadhani tutaishia tu kwa wakati tutapeleka tu Kisayansi.

Kwa hiyo, atahitimisha, tutapiga kura, tukishapiga kura tutapitisha *appropriation* baada ya hapo itaingia *Finance bill* baada ya *Finance bill* tutarudi kwenye saa kumi tutawaletea rasimu ya Kanuni mpya ambazo ndizo zitatumika kwa Bunge la 12 bada ya rasimu zile kuwa zimepita utamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya Jumatatu atoe

hotuba yake ile ya ku-wind up shughuli zote Jumatatu. Nadhani Jumatatu Waziri Mkuu ataongea kati ya saa kumi na mbili na saa mbili usiku kwa ratiba ilivyo inaweza ikaenda saa hizo Jumatatu tarehe 15.

Tarehe 16 Juni, 2020 kuanzia saa tatu asubuhi Mheshimiwa Rais ataingia vianja hivi, tutakuwa na magwaride na utaratibu tutawaeleza itakavyokuwa. Atawea kutoa hotuba hapa around Saa 04:00. Tunategemea akichukua kama masaa matatu maana yake ni kwamba *bysaa* saba mchana Mheshimiwa Rais atakuwa amevunja Bunge hilli la Kumi na Moja, mbona mmenyamaza sana? Tarehe 16 Juni, 2020. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, baada ya hapo nilikwishakuwaahidi kabla kwamba kila mtu ataondoka tu vizuri sasa vizuri inategemeana na mambo mengi lakini hautaondoka hapo ukimdal Spika kitu kwa hiyo, kila kitu kimepangwa vizuri, kila kitu kiko sawa sawa kiko vizuri. (*Makofi*)

Baada ya maneno hayo naomba sasa nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 12.02 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano,  
Tarehe 10 Juni, 2020 Saa Nane Mchana)*